# Nipashe

Alhamisi Desemba 8, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581153

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US





UKURASA 13






## **Mume** na mke wafariki ajali basi, bodaboda



UKURASA 3

# Vigogo chali

• **Samia** achaguliwa tena Mwenyekiti CCM, apania kukisuka chama, Dk. Mwinyi, Kinana makamu wenyeviti... *Endelea ukurasa 2 & 8*

### WALIYOTEMWA


William Lukuvi


Simbachawene


Amina Salum Alli


Abbas Tarimba


Haji Manara


Moudline Castico

## Mama amdai mkwe talaka ya bintiye mahakamani

UKURASA 3


Dk. Hussein Alli Mwinyi (Makamu Visiwani)


Rais Samia Suluhu Hassan (Mwenyekiti)


Abdulrahman Kinana (Makamu Bara)


Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, akizungumza na waandishi wa habari jana, kuhusu kushikiliwa kwa mfanyabiashara Andron Nicodemus, kwa tuhuma za mauaji ya mlinzi wake, Salum Ally. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## Mfanyabiashara mbaroni madai ya kumuua mlinzi akiwa lindoni

UKURASA 3

**MICHEZO** **YANGA YAFUNGUKA HAITABWETEKA** UK.32 **KATUNI** UK.6



Mwenyekiti wa Taifa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akipiga kura kuchagua wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) katika Mkutano wa 10 wa CCM jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Samia apania kuisuka upya CCM

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MWENYEKITI wa Taifa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Samia Suluhu Hassan, amesema amejipanga kukisuka chama kwa kufanya mageuzi makubwa kwa kipindi cha miaka mitano ijayo ili kukirudisha mikononi mwa wananchi.

Amesema Makatibu wa Siasa na Uenezi wa CCM kwenye mikoa wataajiriwa ili kuongeza ufanisi kwenye nafasi hiyo ambayo awali walikuwa wakiipata kwa kuchaguliwa.

Akifungua Mkutano Mkuu wa 10 wa chama hicho, Rais Samia ambaye ni Mwenyekiti wa kwanza wa Taifa mwanamke wa CCM, alisema mageuzi hayo ni pamoja na kuongeza idadi ya wajumbe wa NEC ili kukipa chama sura mpya ya utekelezaji bora wa mipango yake.

Alisema kuongezwa kwa idadi hiyo kunalenga kupanua wigo wa demokrasia na nafasi za uongozi ndani ya chama.

"Katika kupanua wigo na ushiriki wa wanachama ili kufanikisha jukumu la kutafuta ushindi wa chama kwenye chaguzi, Halmashauri Kuu ya CCM Taifa imeamua kuwasilisha mapendekezo ya marekebisho ya katiba ili kuongeza nafasi za wajumbe wa NEC kutoka viti 15 hadi 20 kwa kila upande Tanzania Bara na Zanzibar," alisema.

Aidha, alisema idadi ya wajumbe wa NEC wanaopatikana kwa kuteuliwa imeongezwa kutoka saba hadi 10.

"Malengo ya chama chetu katika kipindi cha miaka mitano ijayo taarifa itasema mageuzi yanayofanywa ndani ya chama chetu ya kukirudisha mikononi mwa wanachama," alisema.

**NAFASI UENEZI KUWA AJIRA**

Kuhusu nafasi ya ukatibu uenezi, Rais Samia alisema wameona ili chama kisemewe vizuri, nafasi hiyo iwe ya ajira ili awajibike vizuri kukisemea chama na itakuwa na vipimo atakayefanya vizuri ataendelea na atakayefanya vibaya mkataba utakatishwa.

"Waliokuwa wakichaguliwa kwenye hii nafasi wanaishia kuimba kwenye mikutano badala ya kubeba siasa na kuieneza, Chama kwasasa kinafanya mambo mengi serikali zinazosimamiwa na chama zinafanya mambo mengi, lakini hakuna anayeyasema, Wenezi wamejia kazi ya kuimba tu kwenye mikutano, tumeona kwa ngazi ya mkoa waanze na ajira, na pale tutakapokuwa vizuri tunaweza kushuka chini," alisema.

**MUOSHWA HUOSHWA**

Alisema ni zamu yake na wajumbe wa NEC kuoshwa baada ya kuwaosha wenzao wa kuanzia ngazi ya mashina hadi mkoa.

"Jukumu letu jingine ni uchaguzi wa ngazi ya taifa, nilipokuwa nahutubia Mkutano Mkuu wa Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT), nilitumia msemo wa muoshwa huoshwa. Mimi na wenzangu wa Halmashauri Kuu ya Taifa na Kamati Kuu, tuliosha wenzetu kutoka ngazi ya shina mpaka kufikia mkoa na leo ni zamu yetu kuoshwa."

"Ninachowaomba mtuoshe tutakate, turudi kukitumikia chama hiki, lakini kama tunavyofahamu chama chetu ni taasisi ya kidemokrasia na chimbuko la uongozi wake ni wananchi wenyewe, wanachama wa CCM," alisema.

Alisema chaguzi zinazofanyika ni kielelezo muhimu cha ukomavu wa demokrasia ndani ya chama na pia haki usawa, amani na maendeleo, mambo ambayo ni nguzo ya itikadi ya siasa.

**MALALAMIKO YA UCHAGUZI**

"Katika chaguzi zilizofanywa ngazi za jumuiya na chama, mashina hadi mikoa na leo taifa, katika ngazi zilizopita kulijitokeza malalamiko mbalimbali yaliyotokana na uvunjwaji wa kanuni za uchaguzi yakiwamo viongozi wakubwa kuingilia michakato ya uchaguzi," alisema.

Alisema malalamiko yalifanyiwa kazi kwa uzito unaostahili na katika baadhi ya maeneo chama kilifuta na kurudia chaguzi, huku baadhi ya maeneo walifutwa wagombea waliokiuka kanuni na kwingine kuondoshwa hadi watumishi au watendaji waliokoroga chaguzi hizo.

"Ikumbukwe CCM inatakiwa kuwa mfano wa kuigwa na vyama vingine, hivyo katiba sheria na kanuni lazima zifuatwe.

Kwa wote walioshiriki chaguzi hizo iwe wamechaguliwa au kura hazikutosha watambue kwamba wao bado ni wanachama wa CCM," alisema. Aliwaomba kuzingatia umuhimu na haja ya kudumisha umoja na mshikamano ndani ya chama na jumuiya zake.

Alisema kuchaguliwa kwa viongozi wapya wa chama na jumuiya kutaongeza kasi na kusonga mbele kwa ari mpya. "Umuhimu wa uchaguzi wetu wa leo (jana) hautokani tu na dhamira ya ujenzi wa CCM imara yenye kuzingatia na kuamini katika haki, usawa na maendeleo ya taifa ni nyenzo ya kuimarisha umoja, mshikamano na nguvu zetu kama chama cha siasa kilicho makini na chenye kuaminiwa na umma, kiendelee kupewa dhamana ya kuongoza taifa," alisema.

Alisema kuwa ni wajibu wa kila mwanachama aliyeteuliwa kutambua lengo la uchaguzi si kutafuta ushindi wa mtu mmoja mmoja bali ni mkakati wa kujiimarisha, kujipanga kwa ajili ya kutafuta ushindi wa chama katika chaguzi zijazo.

"Tuna uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2024 na uchaguzi mkuu mwaka 2025, wote walioteuliwa kugombea nafasi walizoomba ni washindi, kwasababu chama kimewaamini yeyote ambaye angechaguliwa ni mwanachama thabiti anayeweza kuongeza ambaye anaweza kuongeza nguvu katika kukiongoza chama, kwasababu nafasi ni chache ni vigumu wote kuchaguliwa," alisema.

**MABADILIKO YA KATIBA**

Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, alisema pamoja na kuongezwa kwa idadi ya wajumbe wa NEC wataruhusiwa kuhudhuria vikao vyote vya chama vinavyowahusu na kutoa michango yao.

Alibainisha kuwa ajira za Makatibu wa Siasa na Uenezi chama kinakamilisha taratibu za wahusika wanaopendekezwa.

"Walioshikilia nafasi hizo kwa sasa kikao cha Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa kitaitishwa kwa ajili ya kuwachagua wajumbe wa kamati ya siasa, kiongezewe muda wake kwa kipindi cha miezi mitatu hadi Machi 2023," alisema.

Akizungumzia dhumuni la mkutano huo, Chongolo alisema mkutano huo utafanya mambo matatu ambayo ni kufanya marekebisho ya Katiba ya CCM ya mwaka 1977 toleo la mwaka 2022.

Aidha, kupokea taarifa ya utekelezaji wa ilani ya CCM, serikali za pande mbili na taarifa ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa kuhusu utekelezaji wa kazi za chama na jumuiya zake kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Alisema wanachama walioomba kuteuliwa kugombea nafasi za uongozi kuanzia ngazi ya shina ni milioni 1.2, matawi ni 674,624, kata na wadi kwa Zanzibar ni 187,873, wilaya 24,439, mkoa 1,568 na 2,799 kuomba nafasi ya NEC.

## ...Wachambuzi wa siasa watoa neno

**Na Romana Mallya**

WACHAMBUZI wa siasa na uchumi wamemshauri Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Samia Suluhu Hassan, kuhakikisha analeta mageuzi ndani ya chama hicho hata kikitoka madarakani kusiwe na kilio cha haki, demokrasia, usawa na uwajibikaji.

Wakitoa maoni yao jana baada ya kupitishwa kuwa Mwenyekiti wa chama hicho, walisema chama kinachotawala lazima kiweke utaratibu ili siku kitakapotoka madarakani kiache mambo ya kuzingatiwa.

Mchambuzi wa siasa, Abdurahkim Atiki, alisema Mwenyekiti Samia ameonesha anataka kuleta mabadiliko na kutaka chama chake kimuunge mkono. "Wasione utaratibu huo utafanya watoke madarakani, wakiweka utaratibu ambao utaonyesha haki, demokrasia, usawa na uwajibikaji, wanaochaguliwa watachaguliwa kwa haki kuliko ilivyo sasa kunaonekana kuna malalamiko.

"Kwamba kuna tume isiyo huru, hata mataifa ya nje wanatuona kama watu tunaovutana, tunaweza kuwa na demokrasia kama ya India au katika nchi za Afrika, Ghana inafanya vizuri.

"Chama kinachotawala lazima kiweke utaratibu hata siku moja kitakapotoka madarakani kuna kuwa na utawala wa sheria, utawala wa haki na utakaozingatia utu na ubinadamu. Hiki ndicho kitu cha kujengwa na CCM." Kadhalika, alikumbusha kuwa wajumbe ni watu wazito hawatakiwi kununuliwa kwa posho.

"Chama kihakikishe wajumbe wanapewa heshima na hadhi. Wafahamu (wajumbe) kuwa wapo katika eneo ambalo wanakwenda kutengeneza viongozi wanaokwenda kukitumikia chama.

"Kuhakikisha maeneo ya mkutano yanakuwa na hadhi na heshima, sio watu kupita na mabango kama wapo kwenye ngoma au kwenye gulio, waangalie nchi zilizoendelea mfano China tumeona juzi walivyofanya katika mkutano mkuu wao, hii iwe kwa wajumbe kwa ngazi zote," alishauri.

Akizungumzia ukuaji wa teknolojia suala la vijana, Atiki alimshauri mwenyekiti ahakikishe katika uongozi wake makundi yote yanakuwa wanufaika.

"Lazima kuwapo kwa mkakati maalum wa kuwapa hamasa vijana kwenye siasa kunakuwa na ushirikishwaji ili kuleta mambo mapya," alishauri.

Mchambuzi wa Uchumi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Prof. Humphrey Moshi, alimshauri awe na mkakati kuhakikisha rushwa haikubaliki kuanzia katika safu za juu hadi chini.

"Akiona ni waziri au katibu mkuu, hata kule kwenye kamati kuu mtu akionekana ni wa rushwa apewe adhabu ya kutosha ili watu wajue makini.

"Kwa sasa mahali pa kuiga ni nchi ya China, wakisema suala la rushwa halikubaliki, na kweli halikubaliki, ngazi za juu ina watu saba, ya pili ina watu 25, katika ngazi hizo mtu akihusishwa na rushwa kesho yake anaondoka.

"Na sisi tufike mahali watu waadhibiwe bila kujali nafasi zao au kama yupo ndani ya chama. Lazima tuonyeshe dhamira ya kupambana na rushwa, tukifanya hivyo mama atapeta tu."

Kwenye eneo la demokrasia, Prof. Moshi alisema tangu aingie madarakani wameona amejaribu kutafuta suluhu na wapinzani kwa kukaa pamoja.

"Lazima tukubaliane sisi ni Watanzania, wote tunataka maendeleo, lakini kuna njia tofauti za kufikia maendeleo. Tukubaliane tunu za taifa za amani na utulivu, hazina chama, tukubali watu wana maoni tofauti," alisema.

Kwenye uchumi alimshauri ajitahidi kuweka mkazo ili ukuaji wa uchumi uweze kuwa jumuishi na kuwa na mapinduzi katika kilimo cha umwagiliaji na kutumia mbegu na mbolea bora.

Pia akifanye kilimo kiwe cha tija ili kiende sawa na matarajio ya Mpango wa Tatu wa Miaka Mitano wa Maendeleo, unaotaka kuweka mkazo kwenye viwanda.

HABARI KITAIFA

# M'biashara mbaroni tuhuma mauaji mlinzi

**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, linamshikilia mfanyabiashara, Andron Nicodemus (40) na wenzake (haikutajwa idadi) kwa tuhuma za kuhusika na mauaji ya mlinzi, Salum Ally.

Mlinzi huyo aliyekuwa akilinda yadi ya kuhifadhia mitungi ya gesi, eneo la Scanska -Tegeta, wilayani Kinondoni, jijini Dar es Salaam, anadaiwa kuuawa Novemba 20, mwaka huu.

Ndugu na kiongozi wa kampuni ya ulinzi aliyekuwa anafanyakazi Homasa, walifika ofisi za Nipashe Novemba 30, mwaka huu na kueleza kijana huyo mwenye mke na watoto wawili mmoja akiwa mchanga, alivyopotea.

Aidha, Desemba 3, mwaka huu, baba mdogo wa marehemu, Ramadhani Shehoza aliiambia Nipashe walipata taarifa kuna miili imeokotwa eneo la Misugusugu, Kibaha mkoani Pwani, imepelekwa Hospitali ya Tumbi na walipokwenda waliutambua mwili wa ndugu yao.

Jana Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, aliwaambia waandishi wa habari kuwa Novemba 20, mwaka huu, saa 5:00 usiku, polisi walipokea taarifa kuwa Andron, mkazi wa Salasala alifyatua risasi ndani ya yadi yake iliyoko Tegeta, Kinondoni.

Alisema pia walipokea taarifa za mtu mmoja aliyekuwa kwenye eneo hilo (yadi) hajulikani aliko.

Kwa mujibu wa Muliro, polisi walifanya uchunguzi na kubaini mlinzi Salum hakuonekana tangu Novemba 20, mwaka huu, hadi alipokutwa Kibaha Misugusugu, mwili wake ukiwa umetupwa na amefariki dunia.


"Uchunguzi wetu ulibaini Nicodemus na wenzake (hakutaja idadi) walihusika na tukio hilo la mauaji na kwenda kumtupa mlinzi huyo eneo hilo. Upelelezi unakamilishwa na watuhumiwa watafikishwa mahakamani haraka iwezekanavyo," alifafanua Muliro.

Shehoza alisema kijana huyo alikuwa nguzo ya familia na mama yake ambaye ni mgonjwa muda mrefu huku akiacha mke aliyekwenda kijijini kujifungua.

Kaka wa marehemu, Faraji Utandi, aliliambia Nipashe kuwa alikwenda Hospitali ya Tumbi akautambua mwili wa mdogo wake ukiwa na majeraha juu ya masikio yote, huku kidole gumba kikiwa kimekatika.

Desemba 5, mwaka huu, baba mdogo wa marehemu, Frank Shenkawa, aliiambia Nipashe kuwa wamekabidhiwa mwili wa ndugu yao kwa ajili ya mazishi.

Alisema wamempumzisha katika Kijiji cha Ngwelo, Bumbuli Wilaya ya Lushoto mkoani Tanga.



Mhandisi wa kituo cha kupoza umeme katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Gwamaka Thobias (kulia), akitoa maelezo kwa viongozi wa Shirika la Maendeleo la Japan (JICA), walipotembelea miradi mbalimbali iliyotekelezwa na shirika hilo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mume, mke wafariki ajali basi, bodaboda

**Na Restuta Damian, BUKOBA**

AJALI iliyohusisha basi aina ya YOUTONG lenye namba za usajili T 705 DFV mali ya Kampuni ya Happy Nation na pikipiki aina ya SANLG yenye namba T 308 CLH imesababisha mume na mke kupoteza maisha.

Wanadoa hao, Tumaini John ambaye ni Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo ya Maruku na mumewe Geoffrey John wamefariki dunia wakiwa kwenye pikipiki wakati Geoffrey akimpeleka kazini.

Ajali hiyo ilitokea juzi baada ya dereva wa pikipiki aliyekuwa amepakia magunia ya mkaa, kuisukuma pikipiki iliyokuwa ikiendeshwa na Geoffrey John (42) na kupoteza mwelekeo papo hapo na hatimaye kugongana na basi hilo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, William Mwampaghale, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea juzi majira ya 5:30 asubuhi eneo la Ijuganyondo, Manispaa ya Bukoba barabara iendayo Biharamulo wakati basi hilo likienda Dar es Salaam kutoka Bukoba.

Alisema watu waliofariki dunia walikuwa wamebebana kwenye pikipiki yenye namba za usajili T.308CLH aina ya SANLG wakitokea Maruku ndipo waliposukumwa na pikipiki iliyokuwa imebeba magunia ya mkaa, hivyo kukosa mwelekeo na kugongana na basi huku iliyobeba mkaa ikitokomea kusikojulikana.

"Waliofariki dunia katika ajali hiyo ni Geoffrey John (42) mfanyabiashara na Tumaini John (41) Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Kata Maruku wote wakiwa wakazi wa Manispaa ya Bukoba," alisema Mwampaghale.

Alisema Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi na baada ya kukamilika kwa taratibu za upelelezi, litamfikisha mahakamani dereva wa basi hilo Shabani Khatib (38) ili sheria ichukue mkondo wake.

# Mama amdai mkwe talaka ya binti yake mahakamani

**Na Kulwa Mzee**

MAMA mkwe, Rosemary Mayunga amemfikisha mahakamani mkwewe Godwin Mmbaga, akiomba Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iamuru amchukue binti yake kwa ajili ya usimamizi na kumtunza kutokana na matatizo ya afya ya akili yanayomkabili.

Shauri hilo lilifunguliwa hivi karibuni na Rosemary akimtaka mwanawe Kuyega Mmbaga (48), kuwa chini ya uangalizi wake.

Shauri hilo linasikilizwa mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Francis Mhina.

Rosemary katika madai yake anaiomba Mahakama itoe amri ya kuteuliwa kumsimamia Kuyega anayeishi katika ndoa maeneo ya Upanga, jijini Dar es Salaam anasumbuliwa na tatizo la afya ya akili.

Rosemary alidai kuwa yeye ni mama mzazi wa Kuyega Mmbaga na alimzaa mtoto huyo akiwa kwenye ndoa na mume wake Mayunga ambaye ameshafariki dunia.

Alidai mwaka 2002 Kuyega aliolewa na Mmbaga, wanaishi Upanga na walijaliwa kupata watoto watatu, lakini mmoja alifariki dunia na kubaki na watoto wawili.

Watoto waliobaki ni Kiminali Mmbaga (17) na Mariko Mmbaga (7).

"Mwanangu ni mfanyabiashara, yuko katika ndoa halali lakini maisha yake ya ndoa yametawaliwa na matatizo hakuna maelewano na mumewe Mmbaga hali inayosababisha Kuyega kuishi kwa mateso.

"Kuyega kila wakati anaumwa na kupona hali inayosababisha kushindwa kutekeleza majukumu yake, Julai 23, mwaka huu alipelekwa Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa ajili ya matibabu na ndugu yake na baada ya vipimo alibainika anaumwa.

"Katika uchunguzi alionekana ana matatizo makubwa ya akili yaliyodumu kwa miaka mitatu," alidai. Mama huyo anadai sababu za kuomba amri ya Mahakama ni kutokana na matatizo yanayomkabili Kuyega ambaye mara kadhaa amekuwa akitaka kujiua.

Mwombaji aliambatanisha ripoti ya Dk. Frank Masao, ambaye ni Mkuu wa Kitengo Hospitali ya Taifa Muhimbili inayoonesha Kuyega anasumbuliwa na afya ya akili. Alidai kwa tatizo alilokuwa nalo Kuyega, hawezi kutia saini nyaraka yoyote kisheria na tatizo lake kwa asilimia kubwa linachangiwa na mumewe Mmbaga.

Alidai kuwa Mmbaga amekuwa akimtishia kumuua kwa bastola mkewe na taarifa hizo waliziwasilisha Kituo Kikuu cha Polisi.

"Tulitoa taarifa Polisi kwa ajili ya usalama wa maisha ya Kuyega, askari alifika katika nyumba ya Mmbaga, alimkuta akataka kuchukua bastola yake, lakini Mmbaga alidai iko juu chumbani, kabla askari hajapandisha chumbani kuifata alimpekua na kumkuta nayo.

"Mmbaga alikamatwa na kupelekwa Polisi, mwanagu anapigwa, anadhalilishwa, anatishiwa bastola, ananyimwa uhuru wa kuchanganyika kwenye jamii.

"Amekuwa akimkataza kusoma Biblia badala yake anamlazimisha kusoma Kuran tukufu, kanisani haendi," alidai Rosemary katika hati yake ya madai.

Mahakama inatarajia kuanza kusikiliza shauri hilo Desemba 13, mwaka huu na mume (Mmbaga) anatakiwa ajibu madai yaliyoko dhidi yake.

## Mikakati kukabili adha ya usafiri mabasi ya mikoani wabainishwa

**Na Jenifer Gilla**

WADAU wa usafiri wa kwenda mikoani wameeleza mikakati ya kukabiliana na adha hiyo katika kipindi cha msimu wa sikukuu ambacho watu wengi husafiri.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Habibu Suluo, alisema jana kuwa wameshaanza mchakato wa kuandaa mazingira mazuri ya upatikanaji wa usafiri wa kwenda mikoani ikiwamo kutoa leseni za muda mfupi za mabasi kwa ajili ya kutoa huduma hiyo.

"Bado hatujaanza kutoa leseni. Kwa sasa tunakusanya fomu za maombi na kuna vigezo muhimu tunazingatia ikiwamo gari liwe na uwezo wa kuchukua abiria wasiopungua 40. Muda si mrefu tutaanza kupitia maombi na kutoa leseni," alisema.

Pia alisema wamezungumza na Shirika la Reli Tanzania (TRC) ili kuongeza mabehewa kwa ajili ya kusafirisha abiria wengi zaidi hasa mikoa ya kaskazini ambako changamoto huwa ni kubwa katika kipindi hiki.

"Tumeshafanya mazungumzo, kilichobaki ni kwenda kuyakagua haya mabehewa mapya yaliyoingia nchini hivi karibuni, kuangalia ubora wake. Ikiwa yako salama nayo yataongezwa ili kuongeza nguvu katika kutoa huduma hiyo," alisema Suluo.

Meneja wa Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli, Isihaka Waziri, alisema kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi na LATRA, wameandaa vikao vya siku kuanzia jana na madereva na mawakala wa mabasi ili kuweka mikakati ya kuimarisha usalama katika msimu huu wa sikukuu.

Alisema pia wanatoa elimu kwa madereva kuwakumbusha wazingatie sheria za usalama barabarani ili kuepuka ajali ikiwamo kuepuka mwendokasi, kuzingatia taratibu za alama za barabarani, na kuhakikisha abiria wote wamekaa kwenye siti.

"Tumefanya kikao juzi hapa na mawakala, kuhakikisha wanasimamia na kuzingatia taratibu za kituo na taratibu za LATRA. Pia tunawakumbusha wawapatie abiria tiketi za kielektroniki ili kuepusha utapeli hasa msimu huu ambao watu abiria ni wengi," alisema.

Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA), Abdallah Mohamed, alisema wamekaa kikao na madereva wa mabasi na kuwasisitiza wazingatie sheria za usalama wa barabarani ili kuepuka ajali.

"Tumewaambia mwaka huu hatutaki kusikia kabisa ajali za barabarani, kila dereva ahakikishe anazingatia sheria, kabla magari hayajaondoka wahakikishe yapo salama na pia abiria wote wakae kwenye siti, hakuna kusimamisha abiria," alisema.

Pia alisema ili kuhakikisha hakuna shida ya usafiri mwaka huu, wamewaambia wamiliki wenye magari mengi, kuyaandaa magari ambayo hawayatumii ili nayo yaanze safari pake watakapogundua kuna uhaba.

Meneja wa mabasi ya Tashriff, Hamis Shabani, alisema wamejiandaa vizuri kuhakikisha wanatoa huduma stahiki kwa abiria ili kuwaondolea adha ya usafiri ikiwamo kutoa tiketi za kielektroniki ili kuepuka matapeli.

"Safari hii tutahakikisha tunatoa tiketi za kielektroniki ili kuwaepusha abiria na usumbufu wa matapeli ambao wanachukua nauli zaidi, lakini wanawapeleka abiria kwenye magari ambayo yameshajaa hivyo wanasimama, jambo ambalo si zuri," alisema.

# NHC yatangaza fursa uwekezaji majengo Morocco Spuare Dar

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC) limesema mradi mkubwa wa Morocco Square ulioko Kinondoni mkoani Dar es Salaam, unatarajia kukamilika mwezi huu na kuwataka wale wanaotaka kupanga kwenye majengo hayo kuchangamkia fursa hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana kuhusu mradi huo, Meneja Habari na Uhusiano wa NHC, Muungano Saguya, alisema kazi inayofanyika ili kuukamilisha kwa ajili ya kuanza matumizi yake ni kuboresha mazingira.

Morocco Square ni miongoni mwa miradi mikubwa ya NHC ambao una ukubwa wa mita za mraba 110,000.

"Tulisema utakamilika Desemba, mwaka huu na unaendelea vizuri kwa asilimia 97 wanamalizia sehemu chache zilizobaki kuweka vitu vilivyobaki na watu wameanza kupangishwa. Zilizobaki ni kazi ndogo ndogo," alisema.

Juni, mwaka jana, Nipashe iliandika habari kuhusu kusimama kwa mradi huo kwa miaka minne ambao ulianza kutekelezwa Juni, 2014 na ukitarajiwa kukamilika mwanzoni mwa mwaka 2017.

Mradi huo ulisimama mwaka 2017 baada ya ujenzi wake kuanza kusuasua mwaka 2015 kutokana na wanunuzi wa mauzo ya kabla ya jengo kukamilika kupungua.

Mradi huo ambao unatajwa kuwa mkubwa zaidi wa nyumba Afrika Mashariki na Kati, ujenzi wake unatarajiwa kugharimu Sh. bilioni 137.5.

Miradi mingine ambayo wakati huo ilikuwa imesimama ni pamoja na wa Kawe unaoitwa Seven Eleven (711) ukiwa na thamani ya Sh. bilioni 105, ambao Saguya wakati huo alisema utelekezaji wake ulikuwa ukisubiri kukamilika kwa mradi wa Morocco ndipo nao uendelezwe.

Pia mradi mwingine wa shirika hilo uliomo kwenye orodha hiyo ni wa Golden Premier Residence (GPR) Barabara ya Mwai Kibaki wenye thamani ya Sh. bilioni 71.

Kijiografia, mradi huo uko mbele ya ule wa Kawe 711 na mradi wa nne ni ulioko kwenye Kiwanja Na. 300 (Ada Estate) wenye thamani ya Sh. bilioni 24.2.



Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Gerald Kusaya, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kukamata kilo 16.643 za dawa za kulevya zikijumuisha kilo 15.19 za heroin, gramu 654.73 za cocaine na gramu 968.67 za methamphetamine. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kilo 16.6 dawa za kulevya zanaswa Dar

**Na Gwamaka Alipipi**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), katika kipindi cha Novemba mwishoni, imekamata kilo 16.6 za dawa za kulevya zikiwamo kilo 15.19 za heroin zilizowahusisha watuhumiwa saba.

Pia mamlaka hiyo imewaonya wasanii wanaotunga nyimbo za kuhamasisha matumizi ya dawa za kulevya na kueleza kuwa hatua kali zitachukuliwa dhidi yao endapo itathibitika wanafanya hivyo.

Kamishna Jenerali wa DCEA, Gerald Kusaya, alisema hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu taarifa ya mwendelezo wa operesheni waliyoifanya ya ukamataji wa dawa za kulevya kwa kipindi cha Novemba.

Kusaya alisema kati ya dawa hizo zilizokamatwa kilo 15.19 zilikuwa aina ya heroin, gramu 655.73 aina ya cocaine na gramu 968.67 ni methamphetamine.

Alisema ukamataji wa kilo 15.9 za dawa za kulevya aina ya heroin ziliwahusisha watuhumiwa watatu ambao ni washirika wa Kambi Seif na wenzake ambao walikamatwa wakiwa na kilo 34.89 za heroin mwanzoni mwa Novemba wakiwa na kilo 34.89 za heroin.

Kiwango hicho kinafanya jumla ya dawa za kulevya zilizokamatwa kwa Kambi na washirika wake kufikia kilo 50.08.

"Watuhumiwa hawa watatu ni Suleiman Ngulangwa (36) ambaye ni mfanyabiashara na mkazi wa Salasala, Sharifa Bakar (41) na Farid Said (22) wote wakazi wa Majimatitu, Mbagala mkoani Dar es Salaam," alisema Kusaya.

Alisema watuhumiwa wengine wanne walikamatwa wakiwa na gramu 655.75 za cocaine na gramu 968.67 za methamphetamine.

Kusaya aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Hussein Mtitu (28) mkazi wa Mbagala Kibondemaji, Jaalina Chuma (31) ambaye ni mjasiriamali na mkazi wa Tandika, Shaban Said (36) mkazi wa Kilimahewa na Irene Mseluka (39) Mkazi wa Mkoa wa Shinyanga.

Kusaya alisema watuhumiwa wote wanaendelea kuhojiwa na watafikishwa mahakamani baada ya taratibu za upelelezi kukamilika.

Alisema kutokana na kuimarika kwa udhibiti wa dawa za kulevya nchini wahalifu wamekuwa wakibuni mbinu mbalimbali ili kufanikisha adhma yao.

DCEA, alisema iko macho na inaendelea kukabiliana na mabadiliko ya mbinu hizo. Alisema mamlaka inashirikiana na kampuni za usafirishaji wa vifurushi, vyombo vya ulinzi na usalama na wadau wengine katika kudhibiti ili kukabiliana na mbinu mpya za usafirishaji na uuzaji wa dawa za kulevya.

## HABARI K AIFA




Waombolezaji wakiwa wamebeba jeneza lenye mwili wa Mkurugenzi wa zamani na Mwanzilishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, marehemu John Paul Gweba (90), wakati ukitolewa nyumbani kwake eneo la Mbaramo kwenda Kanisa la Anglikana Mtaa wa Mabada kwa ajili ya ibada, kabla ya mazishi yake katika makaburi ya Mtaa wa Madaba Kanisani wilayani humo jana. Gweba, alifariki jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Jela miaka 15 kuua bila ya kukusudia

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salam imemhukumu Ismail Mohamed kifungo cha miaka 15 jela baada ya kupatikana na hatia ya kumuua bila kukusudia Beatrice Onesmo alipomfuata kumhoji kwanini amemchoma kisu mpangaji mwenzake.

Aidha, Ismail katika utetezi wake alidai Onesmo alikuwa anajiuza wakakubaliana kujamiana kwa Sh. 3,000 lakini yeye alikataa na akamvutia ndani ya chumba chake akaanza kumpapasa ndipo vurugu zilipotokea akachukua kisu kwa ajili ya kujihami na akamchoma.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Mkazi Mkuu, Pamela Mazengo, alisema upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha kuwa mshtakiwa alikuwa na nia ovu ya kuua kwa sababu yeye alimvamia mtu aliyejulikana kwa jina la Editha Alphonse kwa ajili ya kuiba.

Hakimu alisema katika ushahidi uliotolewa hasa na shahidi Ritha ambaye ndiyo alivamiwa na mshtakiwa katika chumba chake, haukuthibitisha kwamba Ismail alikuwa na nia ya kumuua Beatrice kwa sababu lengo lake lilikuwa kuiba.

"Hakuna ushahidi wa moja kwa moja wa upande wa Jamhuri unaoonyesha kuwa mshtakiwa alikuwa na nia ya kuua na kama kulikuwa na nia ovu, alitakiwa utengenezwe na shahidi namba tano ambaye ni Ritha.

"Kutokana na hali hiyo, namuachia mshtakiwa kwenye kesi ya mauaji ya kukusudia na kumtia hatiani kwa kosa la kuua bila kukusudia kwa sababu yeye alikwenda eneo la tukio kwa nia ya kuiba simu na hela," alisema.

Hakimu Mazengo alisema kisheria adhabu ya kuua bila kukusudia ni kifungo cha miaka 15, kwa hiyo mshtakiwa atatumikia kifungo hicho lakini Magereza wanajua jinsi ya kupunguza kifungo kwa kuangalia muda aliokaa mahabusu.

Kutokana na hali hiyo, mshtakiwa atatumikia kifungo cha miaka 11 jela baada ya kukaa miaka minne mahabusu.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, upande wa Jamhuri ulidai kuwa hauna kumbukumbu za nyuma za mshtakiwa za kutiwa hatiani, lakini uliomba apewe adhabu kali kwa sababu kama mashahidi walivyoeleza kuwa ana tabia ya unyang'anyi.

Hata hivyo, mshtakiwa alidai kuwa yeye ni mkosaji wa mara ya kwanza, ni kijana na anategemewa na wadogo zake wawili na pia muda aliokaa mahabusu amejifunza.

Katika ushahidi, Ritha alidai kuwa mshtakiwa alimvamia kwenye chumba chake wakati anadeki huku akiwa kashika kisu na kumwambia ampe simu na fedha na aliposema hana, akamchoma kisu na kumweleza kuwa asipige kelele.

Ilidaiwa kuwa kwa sababu tayari alishapiga kelele mwanzoni mwa tukio, Onesmo na mtu mwingine walitoka katika vyumba vyao na kwenda kwenye chumba cha Editha wakakutana na mshtakiwa akiwa ameshika kisu chenye damu.

Alipotaka kumuuliza kwa nini amefanya hivyo, aliteleza chini na kuanguka ndipo mshtakiwa akamchoma na kisu Onesmo ambaye baadaye alifariki dunia baada ya kuvuja damu nyingi. Tukio hilo lilitokea Mei 18, 2018 eneo la Tandika Azimio, Dar es Salaam.


**MWANGA HAKIKA BANK**

## MWANGA HAKIKA BANK LIMITED
## MINIMUM DICLOSURE OF CHARGES AND TARIFFS

| PRODUCTS/ SERVICES | BUSINESS CURRENT A/C | PREMIUM CURRENT A/C | PERSONAL SAVING A/C | SALARY A/C | MTOTO SAVING A/C | JIPANGE SAVING A/C | WEKEZA GROUP A/C | MALENGO SAVING A/C | FOREX ACCOUNT USD & EURO | JIWEKEE SAVING A/C | MHB PAMOJA A/C | MSOMI ACCOUNT |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Account opening | 100,000.00 | 50,000.00 | 20,000.00 | 0 | 10,000.00 | 10,000.00 | 20,000.00 | 100,000.00 | 10 | 0 | 50,000.00 | 10,000.00 |
| Minimum operating Balance | 100,000.00 | 50,000.00 | 10,000.00 | 5,000.00 | 5,000.00 | 0 | 10,000.00 | 100,000.00 | 10 | 10,000.00 | 50,000.00 | 5,000.00 |
| Interest Payable | N/A | N/A | 3.00% | 3.00% | 6.00% | 2.00% | 3.00% | 2% < 10Mil, 4%>=10Mil | 0.50% | 2.00% | 2% | 3.00% |
| Interest bearing amount | N/A | N/A | 50,000.00 | 50,000.00 | 50,000.00 | 50,000.00 | 50,000.00 | 100,000.00 | 5,000.00 | 20,000.00 | 500,000.00 | 20,000.00 |
| Monthly Mantainance fee | 20,000.00 | 10,000.00 | 2,500.00 | 2,500.00 | Free | Free | Free | Free | 2 | Free | Free | Free |
| Deposit | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free |
| Monthly Statement | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free |
| Adhock statement Per page | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 1 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 |

### OTHER CHARGES

| SERVICES | AMOUNT ( TZS) |
|---|---|
| Certificate of Balance | 30,000.00 |
| Confirmation to the Auditors | 30,000.00 |
| Search for information above 5 years | 15,000.00 |
| Cheque book cost (Per Leaf) | 600.00 |
| Status report | 30,000.00 |
| Stop payment order | 30,000.00 |
| Dishonoured cheque for lack of funds or refer to drawer or effect not cleared | 100,000.00 |
| Dishonoured cheque due to the technical error caused by customer | 60,000.00 |
| Dormant Account Activation | Free |
| Account Closing on Customer Demand | 10,000.00 |
| Counter cheque per leaf [Within the Bank] | 15,000.00 |
| Salary Processing fee [ per Transaction] | 1,000.00 |
| Customer ID | 10,000.00 |
| Pre-Mature breaking of Fixed Deposit on customer request | Minimum of 50% of the accrued interest |
| CCTV Camera footage searching request from Customer | 30,000.00 |
| Uncollected Cheque Book/Destruction | 5,000.00 |
| Visa Card Issuance-Classic | 10,000.00 |
| Visa Card Issuance-Gold | 15,000.00 |
| Replacement Visa Card-Classic | 15,000.00 |
| Replacement Visa Card-Gold | 25,000.00 |
| Umoja Card Mantainance fee | 1000 per month |
| Visa Card- Classic Mantainance fee | 3,000 per QTR |
| Visa Card-Gold Mantainance fee | 5,000 per QTR |
| Uncollected ATM Card | 5,000.00 |
| PIN reset fee | 5,000.00 |
| Withdraw fee local (Umoja ATM) | 1000-99,000=1500 100,000-400,000=1700 |
| Withdraw fee other Bank (Domestic Banks) | 3,500 |
| Withdraw fee other Bank (International) | 11,000 |
| Balance inquiry Umoja ATM | 300 |
| Balance inquiry other Domestic Banks | 950 |
| Balance inquiry other Bank (International) | 2,000 |
| Decline Domestic [Insufficient fund] | 1,000 |
| Decline International [Insufficient Balance] | 1,500 |
| QR transactions | 3% of Transaction Amt |
| POS transactions | 3% of Transaction Amt |
| E-commerce transactions | 3% of Transaction Amt |

**Cash Withdraw Over the Counter [TZS/ USD/EURO]**

| TRANSACTION AMOUNT | RATES |
|---|---|
| Wekeza/Jiwekezee | 2,000.00 |
| Bellow 10 Mil | 3,000.00 |
| Above 10Mill to 50 Mil | 0.10% |
| Above 50Mil t0 100 Mil | 0.090% |
| Above 100Mil to 300 Mil | 0.089% |
| Above 300 Mil | 0.079% |

**Cash Withdraw Over the CounterForeign Currency [USD/EURO]**

| TRANSACTION AMOUNT | RATES |
|---|---|
| Below USD/EURO 4,000 | 2 |
| Above USD/EURO 4000 | 0.1% more than USD/EURO 40 |

### AGENCY BANKING CHARGES

| TYPE OF SERVICES | RATES |
|---|---|
| Deposit | Free |
| Balance Inquiry | 500 |
| Min Statement | 700 |
| Transfer of fund within MHB | 2,000 |
| Transfer of funds to other Bank | 13,000 |

### AGENCY BANKING WITHDRAWAL FEE

| AMOUNT | FEE |
|---|---|
| | 850.00 |
| | 1,000.00 |
| | 2,000.00 |
| | 3,500.00 |
| | 4,500.00 |
| | 6,000.00 |
| | 10,000.00 |

### MOBILE BANKING CHARGES

**WITHDRAWAL CHARGES**

| MINIMUM [TZS] | MAXIMUM [TZS] | RATES [TZS] |
|---|---|---|
| 0 | 10,000 | 800 |
| 10,001 | 19,999 | 1,800 |
| 20,000 | 49,999 | 3,500 |
| 50,000 | 99,999 | 5,200 |
| 100,000 | 199,999 | 7,200 |
| 200,000 | 499,999 | 8,200 |
| 500,000 | 999,999 | 10,500 |
| 1,000,000 | 2,000,000 | 11,200 |
| 2,000,001 | 3,000,000 | 12,000 |
| 3,000,001 | 5,000,000 | 15,000 |

**FUND TRANSFER CHARGES**

| | |
|---|---|
| Transfer of Funds within MHB | 2,000.00 |
| Transfer of funds to other Banks | 13,000.00 |

### EFT/SWIFT/TISS

| | |
|---|---|
| EFT within the Bank (Incoming) | Free |
| EFT to other Banks | 1,500.00 |
| TISS Transfer | 10,000.00 |
| T.T. Transfer | - |

### STANDING ORDER

| | |
|---|---|
| Instructions within MHB | FREE |
| Standing Order to other Bank | 10,000/= |

www.mhbbank.co.tz

217183401

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kuna umuhimu wateule wa Rais kukumbushwa maadili

**KATIKA** jamii au taasisi yoyote, kuna watu wamepewa dhamana ya kuwaongoza wengine ili kufikia mipango na malengo waliyojiwekea. Kimaana hiyo, hakuna taasisi iwe ya kiserikali, kisiasa, kijamii au ya kidini isiyokuwa na kiongozi au viongozi ambao ndio washika usukani katika kuyafikia malengo hayo.

Mtu yeyote aliyechaguliwa au kuteuliwa kuongoza watu au taasisi yoyote, anapaswa kuwa mfano katika mwenendo na matendo yake katika kila jambo alitendalo na neno alinenalo mbele ya watu anaowaongoza.

Kutokana na ukweli huo, kiongozi yeyote katika taasisi au jamii yoyote, anatakiwa kuwa na maadili ambayo kwa kiasi kikubwa yatamfanya hata kujizuia katika baadhi ya mambo ambayo mengine alikuwa akiyatenda kabla ya kupewa nafasi husika ya kuongoza jamii au taasisi husika.

Kiongozi, kwa mantiki hiyo, anatakiwa kuwa na kauli njema na matendo bora yanayomtofautisha na watu wengine. Kwa maneno mengine, kiongozi hapaswi kuwa mtu wa ugomvi dhidi ya watu anaowaongoza na wengine na pia asiwe mlevi. Kila mahali na muda wote anapaswa kuwa mfano mwema katika jamii.

Tangu serikali ya awamu ya kwanza, suala la maadili kwa viongozi limekuwa likipewa uzito wa kipekee kwa viongozi na hata baadhi yao wakati wanakula kiapo, wamekuwa wakisisitiza kusimamia maadili.

Sambamba na hayo, hivi sasa watu wanapoteuliwa kuwa viongozi katika utumishi wa umma, wamekuwa wakitia saini kiapo cha maadili ambacho pamoja na mambo mengine kutotumia madaraka au nafasi walizopewa kujinufaisha au kufanya upendeleo wa aina yoyote. Hata viongozi wa dini, kama vile maaskofu wanapoingizwa kazini, wamekuwa wakila viapo kwamba wataendenda katika maadili ikiwamo kutenda haki katika kuwaongoza watu walio chini yao.

Pamoja na hayo, hivi karibuni kumeibuka mtindo wa baadhi ya watu waliopewa dhamana katika nafasi mbalimbali kuzitumia nafasi zao kinyume na viapo ikiwamo kuwa walevi na hata kupiga watu au kupigana wakiwa katika maeneo ya starehe. Mfano ni wiki iliyopita katika Wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani ambako Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alitangaza kuondolewa katika nafasi ya Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri (DED) hiyo kwa tuhuma za ulevi na kupigana na mwananchi katika baa moja.

Pia kumekuwa na tuhuma za mkuu wa wilaya mmoja za kumpiga na kumuumiza mwananchi aliyekuwa amekaa katika jukwaa akitazama mechi ya mpira wa soka, tukio ambalo limesambaa kwenye mitandao na vyombo vya habari.


Kama alivyosema Majaliwa kwa tukio la Kaimu DED, mambo hayo yanaharibu taswira ya uongozi na kuwaondolea sifa. Mambo hayo ni mifano ya watu waliopewa dhamana ya kuongoza watu na taasisi kufanya mambo ambayo yanashusha hadhi zao na ukiukwaji mkubwa wa maadili.

Wakati sasa umefika kwa uongozi wa juu katika serikali kusimamia misingi ya uwajibikaji na maadili kwa viongozi wa ngazi za chini na za kati kutokana na kuwapo kwa viashiria vya ukiukwaji wa maadili na misingi na taratibu za uongozi.

Kuna umuhimu kwa watu wanaoteuliwa katika nafasi za uongozi, wengi wao kwa sasa wakiwa vijana, wakafundwa kuhusu miiko ya uongozi kutokana na baadhi yao kudhani nafasi hizo ni sehemu ya kupata umaarufu, manufaa au fimbo ya kuwachapia wanyonge.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253 676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Hongera makonda kuwa marafiki wa 'madenti' wawapo barabarani

**MIAKA** ya nyuma ilikuwa si rahisi kuona kondakta wa daladala anawaita wanafunzi au maarufu kwa majina ambayo tumeyazoea 'madenti' wakiwataka wapande kwenye mabasi, tena kwa uswahiba kabisa.

Imekuwa kawaida, basi linapofika kituoni, utasikia tu "Kariakoo, sitaki kuona wa kusoma hapa!" Hizi ndizo ilikuwa kauli zao.

Hapo ikitokea bahati mbaya, akapanda huyo 'denti' atakoma na atajuta kwa nini alipanda. Ataanza kusakamwa na maneno.

"Sogea nyuma. Usikae hapo, sogea huku. Kama ukikaa kwenye siti utalipa nauli ya mtu mzima" na maneno mengi ya kukera, ili mradi tu mwanafunzi hadi afike nyumbani anakuwa hoi.

Kwanza kuchoka kwa masomo, inawezekana hata kashikashi za walimu shuleni, hekaheka za usafiri, lakini na unyanyasaji wa makonda wa daladala.

Haya yalikuwa ni maisha ya kila siku ya wanafunzi miaka ya nyuma.

Ilikuwa ni kawaida ya wanafunzi kuchelewa shuleni kutokana na kukataliwa vituoni. Ilikuwa si ajabu kwenye vitu mbalimbali vya mabasi kukuta umati wa wanafunzi waliokuwa wanasubiri usafiri wakutoka na kwenda shuleni, baada ya kukataliwa na makonda.

Nakumbuka kuna baadhi ya wanafunzi wawili wa darasa la kwanza wa jirani yangu, kwa wiki walikuwa wanahudhuria masomo mara mbili au tatu tu.

Ni kwa sababu walikuwa wakirejea nyumbani karibuni kila siku baada ya kukataliwa kupanda daladala. Wanafunzi wale inapofika saa nne wanarejea nyumbani na kusubiri tena bahati yao kesho.

Kwa siku tano za wiki wanazotakiwa kusoma, wanapata bahati ya kwenda shule mara mbili au tatu. Tena wakati mwingine kwa kuchelewa.

Sikwambii sasa kunyanyaswa humo ndani ya daladala. Tena kwa namna ya kushangaza, baadhi ya abiria wamekuwa wakifumbia macho manyanyaso hayo.

Walikuwa wanaona kama ni haki kwa 'denti' kukumbana na maneno makali ya makonda.

Kulikuwa na abiria wachache tu majasiri ndiyo waliokuwa wanaweza kusimama kuwatetea wanafunzi.

Kwa wale 'madenti' wakubwa darasa la saba na sekondari, ilikuwa ni vita na makonda wa daladala. Ilifika wakati mpaka wanakunjana na kupigana.

Katika hali iliyoonyesha maendeleo makubwa kwa sasa hali imebadilika, kuna maisha mapya. Makonda wengi wamebadilika. Inawezekana kabisa kwa sasa makonda wengi na madereva wa daladal ni kizazi ambacho kimeenda shule.

Zamani, kazi ya ukonda wa daladala ilichukuliwa kama ni ya watu ambao wamekosa kazi za kufanya. Ni watu ambao hawajaenda shule, lakini ukiwaangalia sasa baadhi yao ni watu wazima. Wengine ni vijana ambao unaona kabisa wamestaarabika.

Makonda wa sasa wamekuwa ni rafiki wa wanafunzi. Wanawaita wapande kwenye daladala zao. Hata kama wanakuwa zaidi ya 10, wataambiwa wapande wote, halafu makonda wakawachukulia kama wadogo zao.

Watawatania na kuwaweka kwenye siti ya nyuma kabisa, au ile iliyo katikati ya dereva na abiria kushoto. Pale, wanafunzi huwa wanajazana.

Mara nyingi baadhi ya 'madenti' hasa darasa la kwanza na la pili wanakuwa wameshamaliza nauli zao zote. Makonda wa sasa wanajua hilo. Watachukua nauli za wanafunzi ambao ni wakubwa kidogo, lakini wale wadogo akiona wanazunguka, wanajitafuta sana, wanajua tayari wameshakula pesa ya nauli kwa kununua 'ice cream', karanga au ubuyu, anamuacha tu.

Juzi nilimuona kondakta akishuka kwenye daladala lake lililojaa na watu walikuwa wanaligombea huku mvua kubwa ikinyesha. Akaenda kumnyakua mwanafunzi mdogo wa kike aliyekuwa kituoni na alikuwa ameloa.

Asingeweza kabisa kugombea basi, akamnyanyua na kwenda kumpitishia kwenye mlango wa dereva. Wengi wakashangaa na kupongeza.

Mara nyingi tumekuwa tukiwasema sana makonda wa daladala kutokana na baadhi ya tabia zao ambao zimekuwa kero kwa jamii. Lakini, wanapofanya vizuri tumeshindwa kuwapa haki yao.

Kwa hili wanastahili sifa. Wamebadilika kabisa! Siyo wale ambao tulikuwa tunawafahamu huko nyuma. Hawa ndiyo makonda wa kisasa. Hongereni sana. Endeleeni na moyo huohuo.

# LHRC yataka sheria kupinga ukatili

**Na Jenifer Gilla**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimeiomba serikali kutunga sheria mahususi ya kupinga ukatili wa kijinsia na wa majumbani.

Pia imeiomba serikali kurekebisha sheria zote kandamizi kwa wanawake zinazoendelea kusababisha changamoto katika ufikiwaji wa usawa wa kijinsia na ufurahiaji wa haki za wanawake ikiwamo sheria ya ndoa na mirathi.

Kadhalika, imetaka kutunga sheria au sera kuruhusu watoto wanaopata ujauzito kurudi shule kikamilifu, ili kukata gurudumu la umaskini litakaloendelea kuwaweka katika hatari ya kufanyiwa ukatili.

Hayo yamebainishwa katika tamko lililotolewa na kituo hicho jana ikiwa ni kuadhimisha siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia unaoendelea kushika kasi nchini hasa kwa makundi ya wanawake na watoto.

"Jeshi la Polisi liendelee kuboresha mifumo ya ukusanyaji taarifa kuhusu mauaji ya makusudi ya wanawake na kutengeneza miongozo inayozingatia hali halisi hasa katika ukusanyaji wa matukio ya mauaji ya wanawake kwa kuyatenganisha na mauaji ya kawaida," ilisema sehemu ya tamko hilo.

Vilevile kituo hicho kiliitaka jamii kuupaza sauti dhidi ya aina yoyote ya ubaguzi na ukatili na kuachana na mila potofu na zilizopitwa na wakati zinazowaweka wanawake, wasichana na watoto katika hatari ya kufanyiwa ukatili.

LHRC pia iliwataka wanawake kuendelea kuwa mashujaa dhidi ya ubaguzi na kushirikisha jamii kuondoa aina zozote za ukatili na kutoa taarifa pale wanapoona matendo hayo yanafanyika.

Tamko hilo pia limeeleza kuwa mwaka 2021 Tanzania imeshuhudia kuongezeka kwa vitendo vya ukatili wanawake na watoto wakiwa waathirika, ikirejelea Taarifa ya Haki za Binadamu ya mwaka 2021 kuwa kulikuwa na matukio 23,685 ya ukatili dhidi ya wanawake kwa mwezi Januari hadi Desemba kukiwa na ongezeko la matukio 2,859.

Taarifa ya Jeshi la Polisi ya mwaka 2022 iliripoti matukio 472, 544 kwa mwaka 2018, 487 kwa mwaka 2019, 531 kwa mwaka 2020 na 554 kwa mwaka 2021 ya mauaji ya wanawake kutokana ukatili wa wenza, uchawi na imani za kishirikina, mauaji yasiyo ya wenza mashambulio ya wanawake.

Tamko hilo limetaja mikoa inayoongoza kwa ukatili huo kuwa ni Arusha, Manyara, Lindi, Tanga na Temeke (mkoa wa kipolisi), sababu kuu ikiwa ni wivu, kulazimisha tendo la ngono, pombe na ulevi, matatizo ya akili, umaskini, ukosefu wa uwezeshaji uchumi kwa mwanamke, ushirikiano na mila na desturi zilizopitwa na wakati. Pia tamko limesema sheria kandamizi kama ile ya mirathi ya kimila, sheria ya ndoa na kutokuwapo kwa sheria maalumu ya ukatili wa kijinsia au ukatili wa majumbani kumeendelea kuleta changamoto katika kupambana na vita hiyo.

Nyingine kuwa ni kutotekelezwa kwa sheria na kanuni zilizoko kama ya kanuni za mahakama zinazotaka ukamilishwaji wa kesi zinazohusu wanawake kuisha ndani ya miezi sita na sheria ya mtoto.

Aidha, ametaja sababu nyingine kuwa ni kutokuwapo kwa uhuru wa kiuchumi wa wanawake, kukosa elimu ya teknolojia, kung'ang'ania kwenye ndoa au uhusiano usio salama kwa kuogopa jamii.

Aidha, LHRC imepongeza juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na serikali kukabiliana na vita hiyo ikiwamo kuridhia mikataba ya kimataifa ikiwamo wa kupinga aina yoyote ya ubaguzi dhidi ya wanawake na wa haki za wanawake Afrika au maarufu Maputo Protocol.

Dunia inaadhimisha siku 16 za ukatili wa kijinsia kuanzia Novemba 25 hadi Desemba 10, mwaka huu, ikiongozwa na ujumbe wa "Tuungane pamoja kuendeleza harakati za ukatili dhidi ya wanawake na wasichana.

Ujumbe wa Tanzania ni "Kila uhai una thamani. Komesha mauaji ya wanawake na ukatili dhidi ya wanawake na watoto".



Msafara ukiingia kwenye viwanja vya Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU), kwa ajili ya mahafali ya 16 ya chuo hicho, mkoani Dar es Salaam juzi. Wahitimu 943 walitunukiwa shahada za awali, uzamili na uzamivu. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# TANESCO yapokea mtambo wa MW 20

**Na Maulid Mmbaga**

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO), limepokea mtambo kutoka Marekani wenye uwezo wa kuzalisha megawati 20 za umeme ambao utafungwa katika kituo cha kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia cha Ubungo III.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na TANESCO jana, mtambo huo uliwasili nchini Desemba 3, mwaka huu, na kwamba utasaidia kukabiliana na upungufu wa umeme.

Pia taarifa hiyo ilisema shirika linaendelea vizuri na majaribio ya mitambo miwili katika kituo cha upanuzi cha Kinyerezi I ambacho kwa sasa kinaingiza megawati 65 katika gridi ya taifa.

"Tunategemea hadi kufikia mwishoni mwa Desemba, 2022 mitambo hii itakuwa ikizalisha megawati 90. Pia bado tunaendelea na matengenezo ya mitambo miwili ya Ubungo III. Baada ya kukamilika mwishoni mwa Desemba, itazalisha megawati 40," ilisema.

Iliongeza kuwa shirika linategemea mitambo mingine miwili itaanza kufanya kazi katika kituo cha upanuzi cha Kinyerezi I kuanzia Februari, 2023 ili kuingiza megawati 90 katika gridi ya taifa.

Aidha, taarifa hiyo ilisema ujenzi wa mradi wa bwawa la kufua umeme la Julius Nyerere (JNHPP) unaendelea kwa kasi na kwa sasa utekelezaji wake umefikia asilimia 77.

Ilisema ujenzi wa bwawa hilo utakapokamilika, litakuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 2,115 na kwamba zitasaidia nchi kuwa na nishati hiyo ya uhakika na ya kutosha kwa matumizi ya kawaida, viwanda na hata kuuza nchi za jirani.

"Hali ya ukame nchini bado ipo kwa kuwa mvua zinazoendelea kunyesha katika mikoa ya Iringa, Dodoma, Njombe, Morogoro, Tanga na Kilimanjaro ambako ndipo mabwawa yetu ya kufua umeme ya Kidatu, Kihasi, Mtera, Pangani, Hale na Nyumba ya Mungu yaliko hazijawa za kutosha kuongeza kiwango cha uzalishaji umeme.

"Iwapo mvua zitanyesha za kutosha na matengenezo yaliyobakia kukamilika kama yalivyopangwa, basi tunatarajia kiasi cha upungufu wa umeme kitaendelea kupungua. Tutaendelea kutoa taarifa ya hali ya umeme na ratiba ya upungufu wa umeme kadri inavyozidi kuimarika," ilisema.

## KABWELA






Baadhi ya wapambe wa wagombea wa ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, wakiwa na mabango yenye picha za kuwanadi wagombea wao katika Mkutano Mkuu wa 10 wa chama hicho, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Vigogo chali NEC CCM

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKATI Samia Suluhu Hassan, amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), baadhi ya vigogo wa zamani na wasasa wamepigwa mweleka katika kinyang'anyiro cha Ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya chama hicho.

Aidha, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi na Kanali mstaafu Abdulrahaman Kinana, wamechaguliwa kuwa Makamu Wenyeviti wa CCM Tanzania Bara na Tanzania Visiwani.

Katika matokeo hayo, Samia alipata kura 1,914 huku kura moja ikiwa ya hapana. Dk. Mwinyi alipata kura 1,912 kati ya 1915 zilizopigwa, huku tatu zikiwa za hapana na Kinana alipata kura 1,913 kati ya 1,915 huku mbili zikimkataa.

### VIGOGO CHALI

Katika uchaguzi huo, baadhi ya vigogo wakiwamo wajumbe wa Sekretarieti ya NEC na mawaziri, naibu mawaziri wa sasa na wa zamani wameangukia pua katika kinyang'anyiro hicho.

Wajumbe wa Sekretarieti ya NEC walioangushwa ni Dk. Moudline Castico (Katibu wa Oganaizesheni) na Kanali mstaafu Ngemera Lubinga (Katibu wa Siasa na Uhusiano wa Kimataifa) na Katibu Mkuu wa Umopja wa Wanawake Tanzania (UWT), Mwalimu Queen Mlozi. Mwanachama wa CCM maarufu mwingine aliyeangushwa ni Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma.

Mawaziri na naibu mawaziri wa zamani na wa sasa walioangushwa ni William Lukuvi, Balozi Amina Salum Ali, Japhet Hasunga, George Simbachawene, Balozi Ali Abeid Karume, Mudhihir Mudhihir, Stephen Masele, Daniel Nsanzugwanko, Deo Ndejembi na Geoffrey Mizengo Pinda, Jumanne Gagini na Ritha Mlaki.

Wengine maarufu walioangushwa ni Tarimba Abbas, Haji Manara, Francis Nanai, Ismail Aden Rage, Murtaza Mangungu, Jerry Silaa, Deo Mwanyika, Jackson Kangoye, Iddi Azan na Beno Malisa.

Katika kundi la wanawake Tanzania Bara, walioshindwa ni Assumpta Mshama, Zena Yusuph (Shilole), Teresia Mtewele, Asha Baraka, Angel Akilimali, Namelock Sokoine, Khadija Taya (Keisha), Sophia Simba, Amina Mollel, Shyrose Bhanji.

Wanaume katika kundi la Tanzania Bara, walioshindwa ni Hamis Mkotya, Hassan Bumbuli, Murtaza Mangungu, Haji Manara, Jackton Manyerere, Fredy Ngajilo (Vunja Bei), Fredy Mwakibete (Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi), Nyambari Nyangwine na Shaffi Dauda.

### WAIBUKA KIDEDEA

Wakati vigogo hao wakiangushwa, wajumbe wa Sekretarieti ya NEC ni Abdullah Sadala Mabodi (Naibu Katibu Mkuu Zanzibar), Shaka Hamdu Shaka ambaye ni Katibu wa Itikadi na Uenezi na Christina Mndeme (Naibu Katibu Mkuu Tanzania Bara, waliibuka kidedea katika uchaguzi huo.

Walioshinda katika kundi la Wanawake Zanzibar na kura kwenye mabanoi ni Dk. Saada Mkuya (653), Tabia Mwita (666), Najma Murtaza Giga (686), Leila Ngozi (702), Amina Hamis Omary (579) na Mvita Mustapha Ali (547).

### WANAUME ZANZIBAR

Katika kundi la Wanaume Zanzibar, walioshinda ni Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa (798), Issa Haji Ussi(704), Joseph Abdalla Meza (701), Shaka (698), Mohamed Said Mohamed (651), Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, Hamza Khamis Chilo (637).

Wengine ni Amin Salum Amour (610), Mohamed Habib Mohamed (583), Mbarouk Nassor Mbarouk (554), Abdulhafar Idrissa Juma (521), Nasir Ali Juma(419), Khamis Mbeto Khamis (416), Mbaraka Saidi Rashid (379), Abdullah Sadala Mabodi (363).

### KUNDI LA BARA WANAWAKE

Walioshinda wanawake ni Naibu Katibu Mkuu CCM Bara, Christina Mndeme (761), Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Dk. Angeline Mabula (770), Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara Dk. Ashatu Kijaji (764), Hellen Makungu Bogohe (755), aliyewahi kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Fenella Mukangara (747) na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Miko na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki (730).

### WANAUME BARA

Katika kundi la Wanaume Tanzania Bara, walioshinda ni Igaga Mahenda (845), Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Innocent Bashungwa (720), Stephen Wasira (680), Mbunge wa Geita Joseph Musukuma (587), aliyewahi kuwa Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Richard Kaselela (574), Wambura Mwita (545) na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (510).

Wengine ni Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye (508), Mbunge wa Kawe, Josephat Gwajima (497), Waziri wa Nishati, January Makamba (452), Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (450), aliyewahi kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha (435) na Mkuu wa zamani wa Wilaya ya Babati, Dk. Ibrahim Msengi (415).

Walioshinda wanawake Tanzania Bara ni Dk. Angelina Mabula, Dk. Ashatu Kikaji, Christine Mndeme, Hellen Bogohe, Dk. Fenela Mukangara na Angellah Kairuki.

# Taarifa za wafungwa, mahabusu kidijitali

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Magereza linatarajia kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa uchukuaji wa taarifa wafungwa na mahabusu ili kuimarisha utendaji na kuondoa malalamiko kwa wananchi.

Mkuu wa Jeshi la Magereza, Kamishna Jenerali Mzee Ramadhan Nyamka, alisema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo maofisa magereza, askari na watumishi raia kuhusu Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Alisema jeshi hilo litakuja na mfumo wa uchukuaji wa taarifa za wafungwa na mahabusu na hiyo ni kutaka kupunguza msongamano wa mahabusu ikiwamo kuepusha malalamiko.

"Tulijaribu kuwa na mfumo huu awali lakini haukuendelea kwa vile tulikuwa bado hatujajipanga vizuri lakini sasa mfumo huo utakapokamilika utasaidia sana kuboresha utendaji," alisema Nyamka.

Alisema katika mwaka wa fedha 2022/23, serikali imelitengea jeshi hilo Sh. bilioni tano kwa ajili ya kufunga vifaa vya upekuzi na kamera za ulinzi (CCTV).

Kamishna Jenerali Nyamka (pichani) alisema baada ya mfumo huo kufungwa, vilio vya wabunge vitapungua kutokana na kulalamikia mfumo huo uwapo.



"Mara nyingi vilio vya wabunge vilikuwa jeshi kuja na mfumo wa kisasa ili kuondokana na mfumo wa upekuzi tulio nao," alisema Nyamka.

Pia alisema jeshi hilo liko mstari wa mbele kuendana na kasi ya mabadiliko ya TEHAMA.

"Kuwapo na mafunzo ya kutosha kwa wataalamu wa TEHAMA nje ya idara ili kuwajengea uwezo zaidi kwenye maeneo muhimu kama 'cyber security' na 'digital forensic'," alisema.

Alisema kuwa kitengo cha TEHAMA makao makuu ya jeshi kimekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kinatoa huduma kwa vitengo vingine ili kufanikisha shughuli za kila siku kwa kuzingatia sheria ya nchi.

Pia alisema katika mwaka huu wa fedha, mfumo wa matumizi ya ofisi mtandao yataanza na kwamba mfumo huo utapunguza gharama za matumizi ya karatasi na kutoa huduma kwa haraka na ufanisi.

"Kila ofisa, askari anapatiwa kitambulisho cha kazi kulingana na cheo chake. Kila mtumishi kupatiwa barua pepe ya serikali na kuacha kutumia barua pepe binafsi na zoezi hilo limeanza kwa wanasheria wote wa Jeshi la Magereza na awamu itakayofuata ni watumishi wote wa jeshi hili," alisema.

Nyamka alisema pia jeshi hilo litakuwa na kanzi data ya pamoja iliyounganishwa na mfumo wa utumishi hilo litarahisisha kupata taarifa za watumishi kwa haraka na kwa usahihi.

## TIRA yaipongeza TTCL huduma bima simu mkononi

**Na Frank Monyo**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bima nchini Tanzania (TIRA), imeipongeza Kampuni Tanzu ya Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL Corporation) T-Pesa kwa kuanzisha huduma za bima ijulikanayo kama Bima ya T-Pesa kupitia mtandao wa simu za mkononi.

Pongezi hizo zimetolewa jana jijini Dar es Salaam na Kamishna wa TIRA, Dk. Baghayo Saqware, alipokuwa akizindua rasmi huduma ya Bima ya T-Pesa inayotolewa na Kampuni ya T-PESA kwa kushirikiana na kampuni za bima.

Alisema kwa huduma hiyo ya T-Pesa inakuwa ni moja ya watoa elimu ya bima nchini, kwani itakuwa na kazi ya kusimamia uhai, uhimilivu na uendelevu wa soko la bima, kwa lengo la kuchangia ukuaji wa sekta ya bima.

"Nawapongeza kwa kuwa sehemu ya watoa elimu ya bima hapa nchini, tuna kazi ya kusimamia uhai, uhimilivu na uendelevu wa soko la bima, ili kuwezesha kukua kwa sekta ya bima," alisema na kuongeza:

"Lazima kuwe na mikakati ya kusajili watoa huduma wa bima mbalimbali, ambao pia wanaweza kuwafikia wananchi wahitaji sehemu mbalimbali hapa nchini." Dk. Saqware alisema TIRA imevutiwa zaidi na huduma hizo za Bima ya T-Pesa kwani baadaye itawanufaisha pia wakulima, wafugaji pamoja na wavuvi licha ya kutoa huduma nyingine za bima kwa jamii. "Wananchi wanahitaji elimu ya bima vizuri, hivyo ni matarajio ya serikali T-Pesa pamoja na washirika wenu mtakwenda kutimiza azma yenu nzuri kwa kufuata weledi wenye kuzingatia sheria za bima za nchi," alisisitiza Saqware.

Aidha, kamishna huyo alisema serikali inataka huduma za bima ziwe sehemu ya utatuzi wa matatizo ya jamii, ikiwamo kuondoa umaskini na kuongeza utajiri kwa wananchi.

Mkurugenzi wa T-pesa, Lulu Mkudde, alisema T-Pesa kwa kuanzia itatoa huduma za bima ya magari, bima ya nyumba, bima za ajali.




Mwenyekiti wa Kampuni ya Letshego Holding, Philip Odera (kushoto), akikabidhi vifaa tiba mbalimbali vyenye thamani ya Sh. milioni 50 kwa Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume, kwa ajili ya wagonjwa watoto katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) juzi. Kulia ni Mkurugenzi wa MNH, Prof. Mohamed Janabi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kesi kina Mdee kuendelea Machi 6

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu, Masjala Kuu Dar es Salaam imeahirisha kesi kupinga kuvuliwa uanachama iliyofunguliwa na wabunge 19 wa Viti Maalum kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) hadi Machi 6, 2023 kwa sababu wakili wa chama hicho hakuwapo.

Kesi hiyo ilitakiwa kuendelea kusikilizwa jana mbele ya Jaji Cyprian Mkeha na Mbunge Jesca Kishoa (33) alitakiwa kuendelea kuhojiwa na jopo la mawakili kuhusiana na kiapo chake alichokiambatanisha kwenye kesi hiyo, lakini ilishindikana kuendelea.

Kesi hiyo namba 36 ya mwaka 2022, iliahirishwa hadi mwakani kwa sababu mmoja wa mawakili wa chama hicho, Peter Kibatala, yuko kwenye kesi za vikao maalum vya mahakama mkoani Mwanza.

Kibatala alitoa taarifa hiyo kwa mahakama na pande zote za kesi hiyo, wakakubaliana kesi hiyo iendelee kusikilizwa Machi 6, 2023.

Julai 29, mwaka huu, Wakili Kibatala aliiomba mahakama kuwahoji wabunge wanane kati ya 19 kutokana na viapo vyao walivyoviwasilisha mahakamani hapo ambavyo wameviambatanisha kwenye kesi hiyo.

Kibatala aliwataja wabunge hao kuwa ni Grace Tendega, Nusrat Hanje, Cecilia Pareso, Hawa Mwaifunga, Esther Matiko, Esther Bulaya, Jesca Kishoa na Halima Mdee na mahakama ilikubali ombi hilo.

Hadi sasa, jopo la mawakili wa CHADEMA tayari limeshawahoji Tendega, Hanje, Pareso na Mwaifunga na ambao bado hawajahojiwa kabisa ni Esther Matiko, Esther Bulaya na Halima Mdee.

Wakati wabunge hao wanahojiwa na Kibatala, walidai kuwa wao ni wanachama halali na wanakipenda chama hicho ndiyo maana walikisotea sana hadi kukaa mahabusu na pia walidai wao si machizi kuwa wajipeleke Dodoma kuapishwa bila kupitishwa na chama.

Mdee na wenzake walifungua shauri hilo Julai 22, 2022 wakiomba mahakama hiyo ipitie mchakato na uamuzi wa kuwafukuza uanachama na kisha itoe amri tatu.

Katika shauri hilo, wabunge hao wanaiomba mahakama itengue mchakato na uamuzi wa kuwavua uanachama na pia iwalazimishe CHADEMA kuwapa haki ya kuwasikiliza.

Pia wanaomba amri ya zuio dhidi ya Spika wa Bunge na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kutokuchukua hatua yoyote hadi malalamiko yao yatakapotolewa uamuzi.

Pamoja na mambo mengine, wabunge hao wanadai kuwa mchakato na uamuzi wa kuwafukuza uanachama haukuzingatia matakwa ya kisheria na misingi ya haki, wakidai kuwa hawakupewa haki ya kusikilizwa.

Katika kiapo, Mdee anadai kuwa Novemba 25, 2020 CHADEMA walimtumia barua ya maelezo ya makosa yake kupitia mtandao wa WhatsApp na kumtaka ahudhurie kikao cha Kamati Kuu kilichopangwa kufanyika Novemba 27, 2020, ikiwa ni taarifa ya siku mbili tu.

"Kutokana na hasira na vitisho vya usalama wake na kauli za Katibu Mkuu wa CHADEMA kwa umma kuwa ni wasaliti matokeo yake wanachama wa Chadema walianza kutoa vitisho kwa kiwango cha kushutumiwa na hata kuitwa Covid- 19," kilidai kiapo cha Mdee.

Mdee anadai kuwa kutokana na hayo, aliingiwa na hofu ya kushambuliwa na wanachama wa CHADEMA waliochochewa na kauli za viongozi akiwemo Katibu Mkuu, John Mnyika.

Mdee pia anadai kwamba mara tu baada ya kula kiapo, Novemba 24, 2020, Mnyika alimtaja yeye na wenzake 18 kama wasaliti.

# Waandishi wa habari wahakikishiwa usalama

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI imewahakikishia uhuru na usalama waandishi wa habari nchini wakati wa kutimiza majukumu yao, huku ikiwasisitiza kuandika habari bila hofu yoyote na kuibua vitu ambavyo haviko sawa katika jamii kwa ajili ya kuchukuliwa hatua.

Hayo yalisemwa jana mkoani Dar es Salaam na Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, wakati akifungua Mkutano Mkuu Maalumu wa Muungano wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC), uliowaleta pamoja viongozi wa klabu za waandishi wa habari nchini kujadili masuala mbalimbali ya tasnia hiyo.

Alisema serikali haipuuzi kazi nzuri zinazofanywa na waandishi wa habari, huku ikiwasisitiza kuandika na kuchapisha habari kwa kujiamini.

"Zingatieni kuandika habari zenye ukweli, zisizo na uchochezi, zisizo na nia ovu na zenye kujenga nchi yetu badala ya kuibomoa, watu wa kuitangaza vizuri Tanzania ni waandishi wa habari," alisema na kuongeza:

"Niwapongeze sana vyombo vya habari mmekuwa imara, hamjachukuliwa na upepo wa upotoshaji kwenye mitandao ya jamii, hii ndio taaluma, habari inayosambazwa iwe imeandaliwa kwa weledi, ikusanywe, ichakatwe na kutangazwa kitaalamu," alisisitiza Msigwa.

Alisema ufanisi wa waandishi wa habari utakuja pindi watakapofanya kazi zao kwa weledi, akieleza kuwa kazi nzuri ya weledi ndiyo itakifanya chombo cha habari kuwa salama na mbaya ndiyo itakayokiingiza chombo kwenye matatizo.

Aidha, aliwapongeza UTPC kwa kuhakikisha waandishi wa habari wanafanyakazi kwa weledi na kufuata maadili na uwajibikaji kwa wananchi na kutoa mchango mkubwa katika taifa lenye maendeleo makubwa.

Pia, alieleza kwamba anatambua katika tasnia ya habari kuna changamoto, ikiwemo ya sheria zinazohusu vyombo vya habari kwamba zinahitaji kurekebishwa.

"Niwahakikishie dhamira ya serikali inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ni kutengeneza mazingira wezeshi kwa vyombo vya habari kufanya kazi bila bugdha yoyote," alisema na kuongeza:

"Rais Samia ameshamuagiza Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye kukutana na wadau wa sekta ya habari na kujadili namna ya kuziboresha sheria ambazo sio rafiki kwa tasnia ya habari, ikiwemo sheria ya huduma ya habari namba 12 ya mwaka 2016," alibainisha Msigwa.

Kwa mujibu wa Msigwa, vikao kadhaa kati ya serikali na wadau vimeshafanyika, na kwamba majadiliano ngazi ya wadau yameshakamilika, akieleza kuwa wizara ya habari inajiandaa kuwasilisha bungeni mabadiliko ya sheria hiyo, ili wabunge wakiridhia waendelee na utekelezaji wake.

Vile vile, alihakikisha kwamba serikali itaendelea kufanya kazi kwa ukaribu na wadau wa habari kuhakikisha matatizo ya kitaaluma yanayowakabili yanatatuliwa.

Rais wa UTPC, Deogratius Msokolo, alisema umoja huo utaendelea kuwanoa waandishi wa habari katika kuwaongezea uelewa kitaaluma katika utekelezaji wa majukumu yao kwa kuzingatia weledi.

# Gwajima: Iwe aibu mwanamke asiposukuma ajenda ya ukatili

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Doroth Gwajima, amesema iwe ni aibu kwa mwanamke anayeshindwa kusukuma ajenda ya wanawake na kupinga ukatili wa kijinsia nchini.

Aidha, ametaka kila ajenda kwenye kila kikao kuanzia ngazi ya mtaa kuwa na masuala ya ukatili wa kijinsia ambayo yanajadiliwa na kuwekewa mikakati ya kukabili.

Akizungumza hivi karibuni wakati wa kongamano la wanawake na uongozi, katika maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia, lililoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP).

Alisema haitakuwa na maana kuwa na wanawake kwenye ngazi mbalimbali za uongozi halafu agenda zinazowahusu zinapokuja wasizungumze kueleza mambo yanayowahusu kwa uwazi na yapate nafasi.

"Ni lazima tufikie vipaumbele vyetu, lazima tuwe na wanawake wengi viongozi. Tutafakari vipaumbele vyetu kwa kadri ya mazingira yetu. Tabia ya jamii kufumbia macho ukatili baada ya kujazwa hofu haikubaliki," alisema na kuongeza:

"Alisema kesi nyingi zinamalizwa kifamilia wakati aliyetendewa ukatili ameshaathirika maisha yake yote, wazazi tuongee na watoto wetu bila hofu, kizazi cha sasa sio cha zamani," alisema Waziri Gwajima.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi, alisema ni muhimu viongozi wanawake kuendelea kuonyesha mfano katika vita dhidi ya ukatili wa kijinsia.

"Nafahamu hata ninyi kuna wakati mnakumbana na vitendo hivi ndio maana kiongozi mwanamke anafahamu ubaya wa ukatili wa kijinsia kwani wengi tumepitia kwa njia moja au nyingine," aliwaambia viongozi hao,

"Uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi hayajatuacha salama katika suala la ukatili wa jinsia, wanawake na wasichana wanapitia ukatili wakati wanahangaika kutafuta nishati ya kupikia yaani kuni," alisema na kuongeza:

"Wanawake wanabakwa na kupigwa huko msituni wakati wanasaka kuni, pia wanaporejea nyumbani hawako salama wanapata vipigo kwa wenzi wao huku wengine wakikaguliwa kama waligawa ngono wakiwa kwenye zoezi la kusaka kuni.

"Kwa nishati hii adhimu kusogea mbali kutokana na mabadiliko ya tabia nchi wanawake hutumia muda mwingi kutafuta kuni huku majukumu ya kutoa huduma za kifamilia na kijamii yakiwa bado yanawaelemea."

Liundi alisema ni muhimu kujadili na kuwekeza katika teknolojia na ubunifu, ili kupata nishati mbadala ya bei nafuu kuwanusuru wanawake na wasichana na ukatili wa jinsia.

"Maji ni changamoto ambayo inachangiwa na mabadiliko ya tabianchi. Wanawake wanatumia muda mrefu, wanapigwa, wanaombwa rushwa ya ngono, masaa mengi ya kutafuta maji yanawaongezea mzigo wa majukumu. Ni muhimu kutafuta ufumbuzi wa changamoto hizi ili kupunguza ukatili wa kijinsia," alisema.

Aidha, alisema maendeleo ya sayansi na teknolojia yamekuja na aina mpya za ukatili wa jinsia hususan kwenye mitandao ya kijamii na kwamba ni muhimu kuwa na hatua za haraka kwa kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo linalokuwa kwa kasi.

Mwenyekiti wa Bodi ya TGNP, Gema Akilimali, alisema ukatili ni janga la kitaifa hususani mataifa ya Kiafrika, na kwamba vifo vingi, ulemavu, udhalilishaji udunishaji wa utu wa wananawake, wasichana na watoto kutokana na vitendo vya ukatili wa kijinsia ukiwemo ubakaji na ulawiti.

"Theluthi ya wanawake wanakumbana na ukatili kutoka kwa wenzi au marafiki. Taarifa ya Kituo cha Haki za Binadamu mwaka 2021 inaonesha kuwa kila siku takriban wanawake 30 wanakabiliwa na ukatili wa kijinsia," alisema na kuongeza:

"Ukatili dhidi ya wanawake unaathari kubwa sana si tu kwa wanawake bali pia katika uchumi wa nchi na maendeleo na ustawi wa jamii kwa ujumla. Utafiti uliofanywa na UN Women 2013, upotevu wa uzalishaji unaosababishwa na ukatili wa kijinsia unakadiriwa kuwa kati ya asilimia 1.2 ya pato la taifa la Brazili na Tanzania na asilimia 2 kwa upande wa nchi ya Chile."

Akilimali alisema taarifa ya Maendeleo ya Binadamu Afrika (2016) inasema nchi za Afrika zinapoteza zaidi ya Dola za Marekani milioni 95 kwa mwaka kwa kutokuzingatia usawa wa kijinsia.

Mwenyekiti huyo aliwaomba wataalamu kuendelea kubuni nishati mbadala yenye nafuu kwa wananchi wa kipato cha chini, ili kupunguza matumizi ya kuni.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango (Sera), Lawrence Mafuru (kushoto), akimpongeza Mkurugenzi wa Fedha wa Benki ya Absa Tanzania, Obedi Laiser, wakati wa uzinduzi wa ripoti ya Absa ya Viashiria vya Masoko ya Fedha Afrika, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi wa Masoko ya Kifedha wa Absa, Esther Maruma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## RC Songwe aanza uchunguzi tukio DC kumpiga msichana

**Na Mwandishi Wetu**

OFISI ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe, imesema inafuatilia tuhuma zinazomkabili Mkuu wa wilaya hiyo, Simon Simalenga, za kudaiwa kumpiga makofi msichana Frolencia Chrispin (20), mkazi wa kijiji cha Mbangala na kumjeruhi jicho la kulia.

Frolencia aliliambia Nipashe Jumatatu kuwa, Mkuu wa wilaya hiyo alimpiga makofi siku ya Alhamisi baada ya kukaa pembezoni mwa ukuta wa jukwaa, Kata ya Mkwajuni, Makao Makuu ya wilaya ambako inadaiwa hairuhusiwi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano serikalini, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Baraka Mwashambwa, vyombo vya dola vinafuatilia jambo hilo.

"Ofisi ya Mkuu wa Mkoa imeona taarifa ambayo imesambaa kwenye mitandao ya kijamii kuhusu tukio la kupigwa kwa msichana anayeonekana kutoa maelezo kwenye mitandao ya kijamii kwamba kapigwa na kujeruhiwa na Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Songwe," ilisema taarifa hiyo.

Aidha, ilisema kutokana na video hiyo, ofisi hiyo inawataarifu wananchi kuwa vyombo vya dola vinafuatilia jambo hilo na kuwaomba wawe watulivu katika ufuatiliaji ukiendelea.

Kutokana na madai hayo juzi, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Doroth Gwajima, alisema tayari ameshatuma kikosi kazi cha ustawi wa jamii kulifuatilia sakata hilo na kubaini lina ukweli. Waziri Gwajima alisema ametuma kikosi kazi hicho kiende nyumbani kwa msichana huyo ili kumpa ushauri wakati shauri hilo likiendelea.

Frolencia aliliambia gazeti hili kuwa tukio lilitokea baada ya kutii wito wa Mkuu wa wilaya hiyo ambaye aliwakuta wamekaa kwenye jukwaa akiangalia mpira na alipomsogelea alipigwa makofi na kumuumiza jicho la kulia.

# Mwanamume asimulia kunyimwa unyumba miaka 9

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MWANAMUME (jina lake limehifadhiwa), mkazi wa Kitongoji cha Mahameni wilayani Shinyanga, amedai kunyimwa unyumba na mke wake miaka tisa licha ya kuishi nyumba moja.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Masengwa Wilaya ya Shinyanga, Zacharia Ntemi, alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na mwandishi wa Nipashe aliyetembelea kijijini humo.

Alisema mwanamume huyo baada ya kupata elimu ya ukatili wa kijinsia mwaka jana, ndipo alipopaza sauti na kumuweleza namna anavyotendewa ukatili na mke wake kwa kunyimwa unyumba.

Alisema baada ya kuelezwa tatizo hilo, alifika kwenye kaya hiyo zaidi ya mara tatu kuzungumza na mke wa mwananchi huyo na kufanikiwa kuutatua mgogoro huo.

Alisema wanandoa hao walikuwa na ugomvi mkubwa na kusababisha mkewe kuanza kujenga nyumba nyingine pembeni ili watengane.

"Chanzo za mgogoro huu hadi kufikia hatua ya mwanamume kunyimwa unyumba miaka tisa, ni kugoma kwenda kulima ukweni, lakini tunashukuru tatizo limekwisha na watu hawa wamezaa mtoto mwingine baada ya kuwasuluhisha na wanaishi pamoja hakuna tena ugomvi na wanajumla ya watoto watano," alisema Ntemi.

Aliwapongeza wanaume ambao wanapaza sauti wanapofanyiwa ukatili vitendo vya ukatili wa kijinsia, kuliko kukaa kimya huku wakiendelea kuumia, na mwisho wa siku wanajichukuliwa sheria mkononi na kutekeleza mauaji kwa wake zao.

Mwanamume huyo alithibitisha kunyimwa unyumba na mkewe kwa miaka tisa, huku akibainisha kuwa hawezi kuzungumzia namna alivyo kuwa akikidhi matamanio yake.

Alisema licha ya kusuluhishwa, mwanamke huyo ameanza kumsumbua tena kwa kumnyima unyumba.

Aidha, aliwaomba wanaharakati kuendelea kumsaidia ili kuokoa ndoa yake huku akieleza kuwa hajui kinachomsumbua mkewe kwa kuwa wameishi pamoja wakiwa na mtoto mdogo, lakini ana shangaa kumnyima unyumba na kumpa kwa kulazimisha.

Mtendaji wa Kata ya Masengwa Shinyanga, Hussen Majaliwa, alisema kesi za ukatili ofisini kwake ni za watoto pamoja na wanawake, lakini wanaume huwa wagumu kupaza sauti.

Alisema mwaka huu alipokea kesi tatu za wanawake wakipigwa na walisuluhisha wahusika waendelea kuishi pamoja.



## Aliyeachishwa kazi kwa cheti darasa la 7 afunguka

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

ALIYEKUWA Muuguzi Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Esther Laiser, aliyeachishwa kazi kutoka na kuajiriwa kwa cheti cha darasa la saba, amefunguka na kutoa ya moyoni namna ndoto yake ya kuanzisha kituo cha wajawazito wenye vidokezo vya hatari 'Faraja Matenity and Nursing Waiting Home' ilivyokatishwa baada ya kuachishwa kazi Aprili, 2017.

Akizungumza na Nipashe jana, alisema malengo yake yalikuwa kuanzisha kituo hicho ili kuwasaidia wajawazito na watoto kwa kuwa wakati akihudumu katika nafasi hiyo, alishuhudia wanawake wakipoteza maisha kwa kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya. Alisema kabla ya kuwa muuguzi wa wilaya hiyo, kwa kipindi cha miaka mitatu aliyohudumu, aliwahi kuwa Mratibu wa Afya ya Mama na Mtoto wilayani humo na mtumishi katika kituo cha afya cha Orkesument, lakini baada ya kujiendeleza kielimu alipandishwa vyeo kushika nafasi hizo za juu.

"Mimi niliajiriwa kwa cheti cha darasa la saba na kupata Stashahada ya Uuguzi (Diploma), mwaka 2006-2008 na baadaye Shahada ya kwanza mwaka 2009-2012 kwa cheti cha sekondari na malengo yangu yalikuwa kuanzisha kituo hicho ili kuwasaidia wajawazito na watoto kutokana na wimbi la vifo vya wajawazito na watoto na sasa hivi nina umri wa miaka 60," alisema. Alisema awali mwaka 1982 alikuwa na wazo la kuanzisha kituo cha kulelea watoto yatima, kwa kuwa siku moja akiwa kazini alipokea vifo vitatu vya wanawake katika wilaya yake na kulazimika kutoa elimu ya kugundua vidokezo vya hatari vya uzazi wakati wa ujauzito wakiwa kwenye uchungu na kujifungua na baada ya kujifungua.

Alimpongeza na kumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuagiza waliofukuzwa kazini kutokana na tuhuma za kutumia vyeti feki kulipwa mafao yao kwa kuwa wanamchango wao katika ujenzi wa taifa.

"Ninamshukuru sana Rais Samia kwa moyo wa huruma kwetu tuliokuwa na vyeti feki vya sekondari ila vya taaluma ni vya halisi kulingana na vyuo nilivyosomea.

Ilikuwa ni huzuni kubwa kwetu, na wengi wetu wamepoteza maisha kwa kupoteza matumaini ya matarajio yao ya baadaye, ni ukweli usiopingika kuwa tulichangia mchango mkubwa wa maendeleo chanya ya taifa letu pamoja na elimu yetu ndogo ya darasa la saba tuliweza kufanya vizuri," alisema.

"Baada ya masomo furaha yangu ilikamilika kwa kuwa nilijua ninaweza kusimamia kwa ushirikiano wa watumishi wa afya na viongozi katika jamii kutimiza ndoto yangu, ghafla nilijikuta natoka kazini kwa cheti feki cha kidato cha nne iliniuma sana ila sijakata tamaa ijapokuwa nguvu ya kutimiza mlengo ya kuanzisha kituo imepungua," alisema.

Aidha, alisema ana nafasi ya kuendeleza na kukamilisha malengo yake ya ujenzi wa kituo hicho, kwa kuwa sasa hivi anajishughulisha na kazi za mamalishe na amekuwa akipata wateja wengi kutokana na kutambua mchango wake katika jamii wakati akiwa muuguzi. "Ili niungane na wataalamu wenzangu kupunguza vifo vya mama na watoto vitokanavyo na uzazi atakayeguswa kwa moyo wa hiari kunichangia japo nondo moja, mifuko ya saruji na bati nitashukuru sana kwa kuwa hadi sasa hivi nina waya wa uzio rola 10, nondo nane, mchanga lori tano, matofali 3000 na fedha taslimu Sh. 800,000.

# H'shauri yaagiza waliopewa zabuni miradi kuongeza kasi

**Na Allan Isack,** ARUMERU

HALMASHAURI ya Arusha wilayani Arumeru imeagiza mafundi wote waliopewa zabuni ya miradi mbalimbali inayoendelea kutekelezwa kuongeza kasi ya ujenzi ili ikamilike kwa wakati kulingana na mikataba inavyoelekeza.

Agizo hilo, lilitolewa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi, wakati akikagua miradi maendeleo katika sekta ya elimu na afya inayotekelezwa katika halmashauri hiyo.

"Mafundi mliopewa zabuni ya ujenzi wa miradi ongezeni kasi ya kufanya kazi ili ikamilike kwa wakati kulingana na namna mikataba yenu inavyoelekeza," alisema mkurugenzi huyo.

Aidha, aliwataka kutambua miradi yote ya serikali inafanywa kwa muda maalumu wa ujenzi kutokana na malengo yaliyopangiliwa na kwamba kuna umuhimu wa kuikamilisha kwa wakati sahihi. "Serikali imewaamini na kuwapa dhamana ya kufanya kazi hizi, wako walioomba wakakosa, tumieni fursa hii mliyopewa kufanya kazi yenye ubora, pamoja na kukamilisha kwa wakati uliopangwa kwenye mikataba yenu, kinyume cha hapo mtapoteza sifa na kuvunjiwa mikataba yenu," aliongeza Msumi.

Pia amezitaka kamati za usimamizi wa miradi hiyo, ngazi ya jamii kuwabana makandarasi hao na kuhakikisha mafundi wanakuwa eneo la kazi wakati wote.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi wa Zahanati ya Mirongoine, Ibrahimu Lemeirudi, alisema atahakikisha anawabana mafundi waliowapa kazi ili wafuate ratiba yao waliyoiwasilisha kwenye mkataba kwa kufanya hivyo ujenzi utakamilika kwa wakati.Aliishukuru serikali kwa kuwapatia Sh. milioni 50 za kukamilisha ujenzi wa zahanati yao na kuwa walitumia mafundi jamii 'Force Akaunti' katika ujenzi kama ilivyokuwa utaratibu wa kiserikali, pia wametoa fursa kwa wananchi kusimamia miradi inayotekelezwa katika maeneo yao.

Alisema utaratibu huo, unawapa nafasi wananchi kuilinda miradi hiyo, kwa kuwa wanafahamu hatua zote za utekelezaji na kuzuia mianya ya ubadhirifu au upotevu wa fedha na mali ya umma. "Serikali kuzitumia kamati za wananchi, inasaidia kuwapo kwa usimamizi wa karibu, tunafahamu hatua zote za mradi, kuanzia mikataba, ununuzi, mapokezi ya vifaa na utunzaji, matumizi ya fedha zote za ujenzi hadi kulipia huduma kwa usimamizi na wataalamu wa halmashauri, lakini wananchi tunatambua mradi huu ni mali yetu," alisema Mwenyekiti wa kamati hiyo.

Mkurugenzi huyo aliambatana na Timu ya Menejimenti (CMT), kukagua miradi yenye thamani ya Sh. milioni 470, inayoendelea katika kata za Laroi, Oljoro, Bwawani, Nduruma na Mlangarini.



Ofisa wa Jeshi la Zimamoto na Ukoaji Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Walles Kiondo (kushoto), akishirikiana na wenzake kufanya usafi wa mazingira katika ofisi za halmashauri ya wilaya hiyo na stendi kuu ya mabasi jana, yakiwa maandalizi kuelekea kilele cha sherehe za miaka 61 ya Uhuru wa Tanzania Bara. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Kanisa Efatha latoa msaada wodi kinamama

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KANISA la Efatha Tanzania, Mkoa wa Arusha, limetoa misaada mbalimbali katika wodi ya kinamama na watoto katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa huo ya Mount Meru.

Waumini wa kanisa hilo pia walichangia damu salama katika benki ya damu salama hospitalini hapo.


Uchangiaji damu na ugawaji wa misaada ulifanyika jana katika wodi ya mama na mtoto. Katibu wa Kanisa hilo, Mkoa wa Arusha, Edward William, alisema wameamua kutoa misaada hiyo kwa lengo la kushirikiana na serikali kwenye uboreshaji wa sekta ya afya nchini.

"Jukumu letu kusaidia jamii kupitia idara maalumu tumeamua kushirikiana na serikali kuhakikisha ustawi wa jamii unaboreka kimwili.

"Kanisa mbali na kujenga ustawi wa kiroho kwa jamii inayotuzunguka, lakini tuna jukumu madhubuti la kuhakikisha tunashirikiana na serikali kujenga ustawi wa kimwili na baada ya hapa tutatembelea na kutoa misaada mingine Magereza," alisema. Aidha, aliomba makanisa na wadau wengine kusaidia serikali katika nyanja mbalimbali ikiwamo sekta ya afya, elimu na maji.

Muuguzi katika hospitali hiyo, Abdul Salum, alilishukuru kanisa hilo kwa kusaidia kuchangia benki ya damu hospitalini hapo kutokana na uhitaji mkubwa wa wagonjwa wanaowapokea.

"Tunashukuru kwa msaada wenu na tunaamini damu hizi mmechangia zitawasaidia wagonjwa wengi hasa wanawake ambao wakati wa kujifungua mara nyingi wanapoteza damu," alisema. Alisema katika hospitali hiyo kuna tatizo la upungufu wa damu kutokana na kuhudumia wagonjwa wengi.





## Wananchi Negero walilia huduma majisafi

**Na Hamida Kamchalla,** KILINDI

BAADHI ya wananchi wa Kata ya Negero, wilayani Kilindi, mkoani Tanga, wametoa kilio kwa serikali na wadau mbalimbali kuwasaidia kupata majisafi na salama ambayo imekosekana kwa muda mrefu.

Diwani wa kata hiyo, Ahamad Madodi, akizungumza kwa niaba ya wananchi wa kata hiyo, alisema kuna vijiji vinne ambavyo vina shule za msingi na sekondari na havina kabisa huduma hiyo, jambo linalosababisha wanafunzi kufuata maji kwa kutembea umbali mrefu.

Alisema hayo jana wakati wa makabidhiano ya kisima cha maji kilichofadhiliwa na taasisi isiyo ya kiserikali ya Hamdan Group, wilayani humo.

"Shida ya maji kwenye shule za kata yangu ni kubwa kwa mfano Shule ya Sekondari ya Negero, kijiji hiki cha Negero kina shule tano na wanafunzi wote wanakwenda kuchota kwenye sekondari hiyo na kuna shida kubwa sana na watoto wanatumia muda mwingi kwenda kutafuta maji kwenye visima.

"Katika Kijiji cha Kimamba, wanafunzi wanafanya vizuri, lakini wana shida ya maji, katika Kijiji cha Kwalugulu hali iko hivyo kwa kuwa mto umepita maeneo ya mbali, naomba mtuangalie na wananchi wangu mtusaidie kama walivyonisaidia watu wa Hamdani," alisema Madodi.

Wanafunzi wa Shule ya Msingi Lukole, walisema wanatembea umbali mrefu kufuata maji na wakati mwingine husababisha kukosa vipindi darasani, huku maji wanayokwenda kuchota sio safi na salama.

"Tunashukuru kwa kutuletea maji hapa shuleni, kwa kuwa tulipata na usumbufu mkubwa na tulitumia maji ambayo si safi na salama, lakini mradi huu sasa utasaidia tuwe tunatumia maji mazuri yanayofaa kwa matumizi ya binadamu," alisema Zuhura Shabani.

Viongozi wa Hamdan Group, waliofadhili kisima hicho, waliwataka wanafunzi na wananchi kuhakikisha wanatunza miundombinu ya kisima hicho ili waweze kuendelea kupata huduma ya maji kwa kipindi kirefu.

"Wananchi zaidi ya 4,000 katika eneo hili, watakwenda kunufaika na mradi huu, ambao utakuwa unasimamiwa na uongozi wao wenyewe, ninaomba hakikisheni mradi mnautunza.

"Wito wangu kwa wananchi, kwa kuwa ndio wahusika wakubwa pindi viongozi wa taasisi hizi watakapokuja kukagua mradi waukute bado uko katika mazingira mazuri na salama," alisema Habibu Mbota, kiongozi wa Hamdan Group.




Mkuu wa Wilaya Rombo, mkoani Kilimanjaro, Hamisi Maiga, akizungumza katika uzinduzi wa wiki ya msaada wa kisheria, iliyoandaliwa na shirika lisilo la kiserikali la Action for Justice in Society (AJISO), katika Tarafa ya Usseri, wilayani humo jana. **PICHA: JAMES LANKA**

## Bil. 271/- kupandisha elimu jumuishi nchini

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

SHILINGI bilioni 271 zilizotokana na ufadhili wa Mfuko wa Serikali ya Uingereza ukihusisha mradi wa ujenzi wa shule bora umelenga kuiunga mkono serikali kupandisha kiwango cha elimu jumuishi nchini.

Mradi huo pia, umelenga kuweka mazingira salama ya kujifunzia kwa wanafunzi wa kike na wa kiume kuanzia shule za awali, msingi na sekondari nchini.

Mratibu wa mradi wa shule bora, Mkoa wa Tanga, Thomas Aikaruwa, aliyasema hayo jana wakati wa mafunzo ya siku moja ya mradi huo kwa waandishi wa habari.

Alisema mradi utahakikisha kuwa elimu jumuishi inaboreshwa na itatolewa kwa watoto wote.

"Kwa ushirikiano wa serikali yetu, mradi huu utafanya maboresho yatakayowezesha kila mtoto kupata msingi mzuri katika elimu ya awali, ili kutoa fursa na mchango katika ukuaji wa nchi na maendeleo kwa ujumla wake," alisema. Aidha, alisema watafanya kazi katika mikoa tisa ukiwamo wa Dodoma, Katavi, Kigoma, Mara, Pwani, Rukwa, Simiyu, Singida na Tanga na makao makuu yatakuwa Dodoma.

"Mradi unalenga katika maeneo manne ambayo ni kujifunza kwa watoto wote shuleni, kujifunza na ufadhili huu, ni kwa hisani ya Mfuko wa Serikali ya Uingereza na utasaidia kuimarisha kazi ya ufundishaji.

"Utajenga mfumo imara, utaunga mkono juhudi za serikali katika kuimarisha na kupata thamani ya fedha katika utoaji wa elimu katika ngazi zote kuanzia chini hadi taifa," alisema.

Kipaumbele cha mradi huo ni wanafunzi wenye mahitaji maalumu na wanaotoka katika mazingira magumu ili kuwawezesha kuwa shuleni na kujifunza katika mazingira bora na salama hadi kufikia elimu ya sekondari.

"Pamoja na kuwashirikisha wazazi na jumuiya kuboresha usalama wa shule na kuondoa migogoro, tutahakikisha walimu wanazungumzia mambo ya jinsia na upatikanaji wa mahitaji ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

"Pia kutayarisha mazingira salama na kuwaunga mkono wasichana kushiriki na kujadili mambo yanayowahusu, na kuwasaidia kipindi wakiwa kwenye hedhi," alisema.

Mwenyekiti Msaidizi wa Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Tanga, Burhani Yakubu, alishukuru kwa waandaaji wa mafunzo hayo ambayo yataleta tija kwa waandishi katika kutekeleza majukumu yao kwa umma.

"Tatizo ni kwamba wananchi wengi wanaona shule haziwahusu ni ya mwalimu na mwenyekiti wa kijiji na hii inatokana na kukosekana kwa uwazi na ushirikishwaji, unaweza kukuta hata hizo fedha zinazoletwa kutoka serikalini hawapati taarifa na ndio maana wanaona hakuna umuhimu wa kuchangia hata chakula shuleni," alisema.

Mafunzo hayo yalitolewa kwa waandishi wa habari 30 na maofisa habari wa halmashauri za wilaya tisa na ofisa habari wa mkoa huo.

## Waajiri watakiwa kuajiri wataalamu kuepuka lawama

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, amewaagiza waajiri wote nchini, kuajiri wataalamu wa ununuzi na ugavi wenye sifa ili kuepukana na mzigo wa lawama kwa baadhi yao miradi inapokwama.

Alisema hayo jana katika kongamano la 13 la wataalamu wa ununuzi na ugavi lililofanyika jijini hapo.

Alisema ili kuepukana na jambo hilo, ni vyema waajiri wakahakikisha wanaweka watu wenye sifa za kusimamia idara za ununuzi na ugavi.

"Panapotokea mwajiriwa kakosa sifa wasisite kuwapeleka shule ili kuwawezesha kujiendeleza na sisi tutajitahidi kuzifanyia kazi lengo likiwa ni kupata watu wenye sifa katika sekta hii," alisema Ndejembi.

Aliitaka bodi ya wataalamu wa ununuzi na ugavi kuendelea kuchukua hatua kwa kuzingatia sheria, utaratibu na kanuni zilizoko kwa wataalamu watakaokiuka miiko ya taaluma hiyo ili kuhakikisha wataalamu hao, wanafanya kazi kwa weledi na ujuzi, kwa kuwa wana mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi.

"Ili kuleta tija kwenye utekelezaji wa miradi serikali, lazima ijielekeze kufanya ununuzi wa kimkakati kwa kuzingatia ukubwa wa ununuzi na uwiano wa bidhaa na huduma zinazotumika serikalini, ni imani yangu kwenu kupitia mada na majadiliano mbalimbali yatakayowasilishwa kuhusu ununuzi wa kimkakati zitawajengea uwezo na ufanisi katika katika kutekeleza miradi," alisema.

Alisema serikali ina matumaini makubwa na wataalamu wao kufikia malengo ya mipango ya maendeleo ya taifa ya miaka mitano na anategemea maazimio ya kongamano hilo yatapelekea kupunguza matatizo yanayotokea katika ununuzi na ugavi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB), Godfrey Mbanyi, alisema mwaka 2022 wamesajili wataalamu 1995 na kuongeza idadi ya 15,309.

"Bodi iko katika hatua za awali za kuchukua hatua za kinidhamu na imekusudia kuwaita wataalamu 63, ili waweze kutoa maelezo na hatua mbalimbali zichukuliwe, lakini tumetoa karipio kwa wataalamu 78, ambao wamebainika kufanya kazi chini ya weledi na maelekezo ya kitaaluma," alisema Mbanyi.

Alisema lengo la kongamano hilo ni kuwaleta na kuwakutanisha pamoja wataalamu hao ili kujadili fursa na matatizo yaliyoko, kwa ajili ya kupeleka taaluma hiyo katika kiwango kinachohitajika.

Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Jacob Kibona, alisema bodi yake imepewa jukumu la kisheria la kusimamia wataalamu wa ununuzi na ugavi, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha Tanzania inakuwa na wataalamu wa kutosha wenye sifa stahiki na kufuatilia utendaji wao.

Kaulimbiu ya kongamano hilo ni "Fursa na changamoto katika kutekeleza ukuaji endelevu wa uchumi na maendeleo ya jamii".

ama
ALHAMISI DESEMBA 8, 2022
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 16
**UNFPA na Ireland zaungana mradi kutete a afya, uzazi, ngono**



Ukurasa 17
Madaktari, wauguzi wasimulia shida yao hospitalini kuwahudumia viziwi



Ukurasa 18
**Unazijua faida za afya, mazoezi ya kutembea kwa kurudi nyuma?**

AFYA

# Ofisa Mtendaji alia na ugeni UKIMWI, 'dadapoa' wavamizi, agawa kondomu

**Na Sabato Kasika**

KATA ya Mipeko iko wilayani Mkuranga mkoani Pwani, ikibeba jumla ya vijiji 125 na vitongoji 477, miaka 10 iliyopita, iliripotiwa kuwa na jumla ya wakazi 10,890.

katika makazi hayo, Ofisa Mtendaji wa kata hiyo, Gamalu Sogosogo, anafafanua ni kata inayopakana na eneo la Mbande mkoani Dar es Salaam, wakiwa na mwingiliano mkubwa.

Anasema mwingiliano huo unachagizwa na watu kutoka maeneo mbalimbali wanaofanya biashara ya ngono na kusababisha kuwapo maambukizi ya Virusi vya Ukimwi.

Sosogo anaeleza kuwa, endeo la Mipeko limechangamka kutokana na kuwapo shughuli za kiuchumi kama viwanda vya kuzalisha bidhaa mbalimbali, kitendo hicho kinachangia hata wafanyabiashara wa ngono kuwa wengi.



Mwezeshaji wa Kitaifa wa Masuala ya Afya ya Akili na Msaada wa Kisaikolojia na Kijamii kutoka TAMISEMI, Leokadia Mbawala, akizungumza katika Siku ya Taifa ya Ukimwi, wilayani Mkuranga. Kushoto ni Mkurugenzi wa Shirika la Himiza, Prisca Ngweshemi, Mtendaji wa Kata ya Mipeko, Gamalu Sogosogo na Mwenyekiti wa Kijiji cha Mipeko, Adinan Amanda. **PICHA: SABATO KASIKA**

Akizungumza katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani, Desemba Mosi, yaliyofanyika Mipeko na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali, anaanikia uhalisia kwa kauli:

"Januari hadi Oktoba mwaka huu, watu 2,165 walipimwa VVU kwa hiari, wanaume wakiwa 680 na wanawake 1,485, waliobainika kuwa na maambukizi ni 51, wanaume ni 14, wanawake 37," anasema Gamalu.

Anafafanua kwamba, wengine 59 wanatumia dawa za kufubaza VVU ambao wamekuwa wakipata dawa katika zahanati ya Mwanambaya na kwamba wanaume ni tisa na wanawake 50.

Ofisa Mtendaji huyo anataja sababu nyingine zinazochangia kata hiyo kuwa na maambukizi kuwa ni jamii kutozingatia elimu kujikinga na ugonjwa huo, tabia hatarishi majumbani ikiwamo ukatili wa ngono, ulevi kupindukia, ngono zembe, ngoma za usiku na matumizi ya dawa za kulevya.

"Kwa ujumla hizo ndizo sababu kuu zinazochangia kata yetu kuwa na maambukizi, lakini niwashukuru wanawake kwa mwitikio wao wa kujitokeza kupima VVU," anasema.

Anasema anaendelea kushirikiana na viongozi wenzake wakiwamo wa idara ya afya kuhamasisha watu kuwa na mwamko wa kupima, ili wajihakikishie usalama wa afya zao.

**VITA VILIVYO**

Sogosogo anasema kuanzia mwaka 2020 hadi sasa, wamegawa bure jumla ya kondomu za kiume maboksi 5,900, katika vijiji vitatu vinavyounda kata hiyo vya Mwanadilatu, Mwanambaya na Mipeko.

Aidha, anasema kata hiyo imekuwa ikishirikiana na wadau mbalimbali kuhamasisha watu kupima afya zao, pia kutoa elimu kuhusu maambukizi ya VVU na UKIMWI, lengo ni kuhakikisha jamii inakuwa salama.

Ofisa huyo wa serikali, anaeleza kuwa elimu imekuwa ikitolewa kwa njia ya mikutano na maeneo mbalimbali, inasaidia watu kuwa makini na kuachana na biashara ya ngono inayoshamiri katika kata hiyo.

Aidha, anasema matarajio yao ni kuunda na kuhuhisha kamati ya UKIMWI, zisaidie vita hivyo, ili kila mmoja atimize wajibu wakati wa kupiga vita.

**BWANA SAIKOLOJIA**

Mgeni rasmi katika maadhimisho hayo, Mwezeshaji wa Kitaifa wa Afya ya Akili, Msaada wa Kisaikolojia na Kijamii kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI, Leokadia Mbawala, anasema serikali inafanya jitihada kuhakikisha biashara ya ngono inatokomezwa, hivyo anaiomba jamii iiunge mkono.

"Ikibidi, kila mmoja arudi katika imani yake ya dini kumwomba Mungu, pia kubadili tabia ili kukabiliana na ugonjwa huu hatari," anasema Leokadia, anayewataka wanaotumia dawa kufubaza VVU wasikatishe dozi, kwa kuwa ni hatua hasi kwa usalama wa maisha yao.

"Pamoja na hayo, jamii isiwanyanyapae wenye ugonjwa huo, kwani wengine wamekuwa wakiacha dozi kutokana na kunyanyapaliwa majumbani na mitaani," anasema.

Rai yake ni jamii ikiungana katika vita dhidi UKIMWI, hakuna atakayemnyanyapaa na maambukizi yanaweza kwisha, kwa kuwa kila mmoja atakuwa anajua wajibu wake kiafya.

**NGO YANENA**

Mkurugenzi wa shirika lisilo la kiserikali la Himiza Development Organization, Prisca Ngweshemi, anasema wazazi na walezi wanawajibika kuhakikisha watoto wanakuwa salama dhidi ya UKIMWI.

"Wazazi wawe tayari kuzungumza na watoto wao kuhusu ugonjwa huo na kuwahamasisha kupima afya zao, huu si wakati wa kuendelea kuficha ukweli, wafundisheni waelewe madhara ya ugonjwa huu," anasema Prisca.

Mkurugenzi huyo alifafanua kuwa vijana waliofikisha umri wa miaka 18 wanaweza kupima kwa hiari yao na kwamba walio chini ya umri huo wanaweza kupima kwa ridhaa ya wazazi au walezi wao.

"Hivyo, si vibaya mkakaa nao na kuwashauri kupima, kwani siku watoto wadogo ndio wanaofanyiwa ukatili wa kingono, mkiwaruhusu wapime mtaweza kujua afya zao na kuwasaidia zaidi," anasema.

Anafafanua kuwa ukatili wa kingono unafanyika majumbani, shuleni na mitaani, huku akiongeza kuwa mtoto anaweza kujikuta ana UKIMWI bila mzazi kujua na kujikuta akipoteza maisha.

AFYA

# Mganga Mkuu: Uviko-19 ulitutoa jasho hivi, tukapambana namna hii

**Na Elizabeth Zaya**

MKOA wa Dar es Salaam na sisi tulitikisika kidogo baada ya kuripotiwa kwa ugonjwa wa Uviko-19," ni tamko la kwanza la Mganga Mkuu Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume, akizungumza na Nipashe kuhusu ugonjwa huo. Anaendelea:

"Huu ni mkoa mkubwa wa kibiashara na una idadi kubwa ya watu, kwa hiyo mwanzoni kabisa katika wimbi la kwanza, hofu ya ugonjwa ilikuwa kubwa mno na tulipata idadi kubwa ya wagonjwa katika vituo vyetu tulivyokuwa tumetenga."

Anasema mgonjwa wa kwanza mkoani aligundulika na kuthibitika Machi 2020 na baada ya hapo waliendelea kupata wengine katika wimbi hilo la kwanza.

Dk. Mfaume anaeleza kwamba, mikasa mingi katika wimbi la kwanza, la pili na tatu, athari zake za awali ni ya kisaikolijia iliyotokana na hofu.

Anasema baadhi ya wagonjwa wenye ratiba za kliniki wakiwamo kinamama, watoto na wenye magonjwa yasiyo ya kuambukizwa, waliacha kwenda kwenye huduma hiyo, hususani katika vituo vilivyopokea wagonjwa hao wa Uviko-19.

"Katika mifumo yetu ya utoaji wa huduma, kuna huduma ambazo ni endelevu na watu wanatakiwa waje kupata huduma hizo, mfano kinamama walitakiwa kuendelea kuja kliniki na kuna ratiba katika mahudhurio yao.

"Watoto walitakiwa wapelekwe kwenye vituo kwa ajili ya chanjo, kuna watu wanaoishi na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU), walitakiwa kufika kwenye vituo kupata huduma hiyo, kwa hiyo wakati huo watu walipata hofu ya kwenda kwenye vituo. Walijua kabisa kwamba huduma ya Uviko-19 inapatikana kwenye vituo vyao ambavyo hufanyia kliniki.

"Kwa hiyo, kulikuwa na kuathirika kidogo kwa upokeaji wa makundi kama hayo kwenda kwenye vituo kwa zile ratiba ambazo sehemu kubwa ni za kinga au tiba. Kwa hiyo, unapopata hiyo shida tegemea kwamba kidogo kutakuwa na mwingiliano wa mwendelezo sahihi wa matibabu," anaeleza.

Mganga Mkuu pia anasema, katika wimbi la kwanza na pili, kwa siku walikuwa wagonjwa wa Uviko-19 hadi 30 na changamoto nyingine anaitaja, kuwapo na bidhaa za kiafya walizotegemea kutoka nje ya nchi.

"Pamoja na kwamba Dar es Salaam tuna viwanda vya uzalishaji wa bidhaa za afya, lakini zipo bidhaa ambazo bado huwa tunategemea kuzipokea kutoka nje ikiwamo China na maeneo mengine ambayo yameathirika na Uviko-19. Bidhaa zilikuwapo, lakini kulikuwa na upungufu.

"Sasa unapokuwa na upungufu kidogo wakati ule ambao idadi ya wagonjwa ilikuwa kubwa, kidogo iliathiri utoaji wa huduma ambao ni bora kulingana na viwango vinavyohitajika," anasema Dk. Mfaume.

Pia anataja shida ya kuwapo vituo vingi vilivyokosa mapato, kutokana na idadi ya wagonjwa kupungua, hususani wasiougua Uviko-19.

"Sasa unapokuta wateja unaowahudumia, namba (idadi) inapungua kidogo hata mapato ya kwenye vituo vyetu vya kutoa huduma inashuka kidogo. Kwa hiyo tuliona vituo vingi mapato yale ya uchangiaji, yakiwa yameshuka kidogo wakati ule wa ujio wa Uviko-19 hasa wimbi la kwanza na la pili," anasema Dk. Mfaume.

Anaendelea: "Lakini tunashukuru Mungu kwamba hatukupata athari kama ambavyo tulikuwa tukisikia kwa nchi za wenzetu. Hali ya hofu ilianza kupungua baada ya serikali kuendelea kuwatoa hofu wananchi na kuwaambia kwamba haitawafungia ndani bali wataendelea na shughuli zao."

> Sasa unapokuwa na upungufu kidogo wakati ule ambao idadi ya wagonjwa ilikuwa kubwa, kidogo iliathiri utoaji wa huduma ambao ni bora kulingana na viwango vinavyohitajika.

#### UJIO WA CHANJO

Dk. Mfaume anasema, ujio wa chanjo ukawa ndio mwarobaini, akinena :"Umetoa ahueni kubwa sana kwa wananchi wenyewe, kwa familia zao, kwa serikali na kwa vituo vya kutoa huduma vya umma na sekta binafsi, hapa ndio tulipumua.

"Ukienda katika hospitali zetu (za serikali) baada ya watu kuchanja, idadi ya watu ilipungua, ulikuwa hukuti idadi kubwa ya waliolazwa kama ilivyokuwa awali iliporipotiwa ugonjwa katika wodi zetu na hata ukikuta ni mmoja au wawili ambao nao ni kwa sababu hawajachanja.

"Hatusemi Uviko umeisha kwa asilimia 100, lakini hata mtu akiugua unakuta ni mafua ya siku moja au mbili na hayamlazi."

#### MAGUMU YA CHANJO

Dk. Mfaume anaeleza kuwa, mwanzoni wakati Rais Samia Suluhu Hassan, amezindua chanjo, idadi ya waliojitokeza kwa siku hizo za kwanza ilikuwa kubwa, lakini baada ya wiki kadhaa, idadi ilipungua kiwango cha kuwapa hofu.

Anasema mwanzoni walianza watu 7,000 kwa siku na baada ya hapo idadi ilishuka mpaka kati ya 400 na 200, hata wakabuni namna ya kuwashirikisha wenyeviti wa mitaa, wajumbe na wahudumu wa afya ngazi ya jamii, kupita majumbani kuhamasisha hadi vijiweni, watu wakachanje.

"Baada ya kushirikisha wenyeviti wa mitaa yote pamoja na hao wahudumu wa afya ngazi ya jamii, idadi ikaanza kuongezeka tena mpaka watu 30,000 kwa siku. Tulipita nyumba kwa nyumba hadi kwenye vijiwe vya bodaboda tukawachanja hukohuko. Na ndiyo hiyo ilitupatia matokeo mazuri ya kufikia malengo yetu ya chanjo kwa mkoa wa Dar es Salaam," anasema Dk. Mfaume.

#### BAADA KUCHANJA

Anasema, baada ya chanjo idadi ya wanaolazwa kwa ugonjwa huo, ikaanza kupungua kila siku, akitamka mafanikio kwa kauli: "Baada ya watu kuchanja, unaweza kukuta waliolazwa hakuna au ni mmoja.

"Kwa hiyo, kwa sasa ukienda wodi hazina wagonjwa wa Uviko-19. Ila tunaendelea kusisitiza kwamba watu waendelee kuchanja kwa sababu hatusemi ugonjwa umeisha maana tunaendelea kuona hata kwenye nchi za wenzetu huko.

"Hiyo ndiyo nguvu ya afya ya kinga au chanjo ilivyoleta ahueni, kwanza kwa kupunguza na kuzuia virusi vya ugonjwa huo, lakini hata ukipata shuhuda sasa hivi tunaziona hazikupeleki katika kulazwa."

#### WALIOCHANJA DAR

Anasema lengo kwa mkoa ni kuchanja watu milioni 3.8, lakini mpaka sasa wamefanikiwa kufikia watu milioni 3.2 na mtazamo ulioko ni hadi kufika mwisho wa mwezi huu, lengo la asilimia 100 litakuwa limefikiwa.

"Sayansi inatuambia kwamba, asilimia kubwa wakichanja, wanawasaidia na wengine ambao hawajachanja, japo tunataka wote wachanje," anasema Dk. Mfaume, hivyo wanaendelea kuhamasisha umma wote uchanje, katika kazi anayosema haitakoma hata lengo likifikiwa, bali ni endelevu uwafikie wageni na wanaozaliwa.

"Kwa hiyo tuseme hatua ambayo imeleta matokeo makubwa ni hii ya chanjo ya UVIKO, tumetoka mbali tumepitia milima na mabonde kwenye Uviko 19, kulikuwa na changamoto nyingi lakini hatimaye tumekuwa imara, japokuwa tunaendelea kuchanja na kuchukua tahadhari nyinginezo."

Anasema mkoani Dar es Salaam, wamekuwa na vituo 321 vya kutoa huduma ya Uviko 19, vikijumuisha binafsi na vya serikali. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Wizara ya Afya Desemba 5, mwaka huu kuhusu mwenendo wa Uviko-19 kuanzia Oktoba 29 hadi Desemba 2, mwaka huu jumla ya visa maambukizi 442, yamethibitika na hakukuwapo na mgonjwa aliyelazwa au kuripotiwa kufariki.

***• Fuatilia mazungumzo zaidi ya Nipashe, na Mganga Mkuu wa Mkoa Dar es Salaam, kuhusu Uviko 19 Dar es Salaam, Alhamisi wiki ijayo.***



Mganga Mkuu Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume. **PICHA: ELIZABETH ZAYA**

AFYA

KUTOKA CHUO KIKUU MUHIMBILI...

# Fahamu kuongezeka magonjwa duniani, kila mmoja ni mhusika

**Na Waandishi Maalum**



Watu wakiwa katika huduma za kliniki, ambako pia kunapatikana elimu ya afya. **PICHA ZOTE: MAKTABA**

TANGU mwaka 1990, kumekuwapo na ongezeko kubwa la magonjwa duniani kote hasa ya kuambukizwa kukishuhudiwa katika nchi zinazoendelea, ikiwamo Tanzania.

Baadhi ya magonjwa hayo ya kuambukiza ni kipindupindu, kuhara, magonjwa ya tumbo, malaria, kifua kikuu, virusi vya ukimwi na upungufu wa kinga mwilini (UKIMWI).

Pia dunia sasa inashuhudia kuongezeka magonjwa yasioyambukizwa ikiwa ni pamoja na moyo, shinikizo la damu, kisukari na kansa. Kama ilivyo kwenye nchi nyingine zinazoendelea, Watanzania wameshuhudia kuongezeka vifo vitokanavyo na magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza.

Kwa mfano, baada ya kuripotiwa kwa ugonjwa hatari wa UVIKO-19 Desemba 2019 nchini China, ugonjwa huo uliingia nchini Tanzania mnamo Machi 2020 na kuchangia vifo zaidi ya 800.

Kisha Julai mwaka huu, ulitokea ugonjwa wa homa ya Mngunda (Leptospirosis/Field fever) katika maeneo ya kusini mwa nchi, hususani mkoani Lindi katika wilaya ya Ruangwa.

### MADHARA YAKOJE?

Yote kwa jumla haya yamekuwa yakileta madhara makubwa kwenye nguvukazi ya taifa. Mfano hai, ni kuongezeka matukio ya vifo vya ghafla, pia watu kugundulika na magonjwa wakiwa wamechelewa.

Wananchi wengi wamekuwa wakipoteza rasilimali na maisha kutokana na kuumizwa na magonjwa hayo. Kwa mfano, kutokana na janga la UVIKO-19 lililotikisa dunia nzima kwa zaidi ya miaka mitatu sasa, Tanzania wananchi wamepoteza ndugu na rasilimali nyingi, ikiwamo fedha katika kupambana na tatizo hilo. Magonjwa yasiyoyakuambikizwa yamekuwa yakigharimu maisha ya watu wengi duniani na nchini wanategemewa katika ujenzi wa taifa.

Hadi sasa, kuna magonjwa haya yameshawaathiri wengi na kurudisha nyuma maendeleo katika nyanja zote za maisha yaani kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kisiasa.

Ni wazi kwamba magonjwa mengi yanayotusumbua yanatokana na tabia zetu za kila siku na namna tunavyojiendesha. Kwa mfano; kutokuzingatia usafi wa mazingira na vyakula, kutokuzingatia mlo kamili, kukosa kufanya mazoezi ya mwili kwa ukawaida, kunywa pombe kupita kiasi, upotovu wa maadili kingono na kadhalika.



Shughuli za kampeni ya afya wilayani Kishapu, Shinyanga, ambayo ni sehemu ya elimu ya afya.

Hivyo, inatajwa ni muhimu kwa kila mwananchi kuhakikisha anafanya tathmini na ufuatiliaji wa afya yake binafsi na kuchukua hatua za awali mara tu anapoona kasoro yoyote katika afya yake.

Baadhi ya hatua zinazotakiwa kuchukuliwa ni pamoja na kwenda katika kituo cha tiba na kupata huduma stahiki.

Kwanini? Ni muhimu kupata matibabu ya tatizo husika, kabla halijawa kubwa zaidi au kufikia hatua ya kushindwa kutibika.

Pia watu wanatakiwa kujitahidi kufuata ushauri unaotolewa na watoa huduma za afya, ikiwa ni pamoja na kupunguza ulaji vyakula vyenye kiwango kikubwa cha sukari na mafuta, hasa yale yenye lehemu (cholesterol) nyingi, kama ilivyo kupunguza matumizi ya vilevi hasa vikali, na kufanya mazoezi ya mwili.

Pia kila mwananchi anapaswa ajitahidi kustawisha mazoea bora yanayochangia kulinda afya, kama vile kunawa mikono, kunywa maji na kutumia chakula safi na salama, kupumzika vya kutosha, kuzingatia mlo kamili ili kuupa mwili uwezo kupambana na magonjwa mbalimbali.

Hayo yote yanaelekezwa, bila ya kuacha mazoezi ya mwili, pamoja na kuendelea kuzingatia masharti na maelekezo ya wataalamu, hasa kwa walio katika matibabu ya muda mrefu, ikiwa ni pamoja na kutumia dawa kwa wakati na kwa usahihi.

### FAIDA ZA HATUA?

Kama kila mmoja atafanya tathmini na ufuatiliaji wa karibu wa afya yake, basi kuna matumaini ya kupata faida; kuanzia kwa mtu binafsi, jamii na taifa. Faida ya kwanza ni kutambua hali halisi ya maendeleo ya afya yake.

> **Hadi sasa, kuna magonjwa haya yameshawaathiri wengi na kurudisha nyuma maendeleo katika nyanja zote za maisha yaani kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kisiasa.**

Pili ni kugundua mapema kasoro yoyote ya kiafya hata kama ni dogo na hivyo kupata ushauri/ufumbuzi wa mapema. Mambo hayo mawili yatasaidia wataalamu kufuatilia na kutambua chanzo cha ugonjwa husika na kuweza kuchukua hatua stahiki kwa wakati unaofaa.

Sasa unafahamika umuhimu wa kufanya tathmini na ufuatiliaji wa karibu wa afya zetu kila mara. Huo ndio wakati mwafaka wa kila mmoja kutimiza jukumu hilo kikamilifu na kuchukua hatua stahiki na zinazofaa.

Wito uliopo sasa kila mwananchi aanze kufanya tathmini na kufuatilia kwa karibu afya yake ya sasa, huku akilinganisha na aliyokuwa nayo awali, ili kutambua mapema mabadiliko yoyote ya kiafya katika mwili na hata akachukua hatua mapema inapobidi.

Hiyo ni pamoja na kutembelea vituo vya huduma za afya mapema, ili kupata msaada sahihi. Kama kila moja katika jamii atafanya hivyo, basi inawaasaidia wataalamu wa afya katika kutambua mapema vyanzo vya magonjwa na kutoa tiba sahihi, kulingana na matatizo yaliyoko. Hilo likizoelewa, huenda kukapatikana suluhisho la muda mrefu, hasa katika kuhakikisha afya ya kila mtu aendelee kuwa katika hali njema, muda wote kuwa na jamii yenye afya njema na imara.

***• Waandishi wa makala hii; Pankras Luoga (0757 645746), ni Mhadhiri Msaidizi wa Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathimini ya Miradi ya Afya na Judith Costantine (0782 1158020) Mhadhiri Msaidizi Famasia, katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS).***

AFYA

## SIKU 16 KUPINGA UKATILI JINSIA NCHINI

# UNFPA na Ireland zaungana mradi kutetea afya, uzazi, ngono salama




Balozi wa Ireland, Mery O'Neill (kushoto), akiwa na mwakilishi wa UNFPA nchini, Mark Bryan Scheiner, baada ya kutia saini makubaliano ya kutolewa fedha, Dola za Marekani milioni 1.4 zitakazotumika katika miradi miwili. **PICHA: YASMINE PROTACE.**

**Na Yasmine Protace**

KATIKA kuelekea Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) na Ubalozi wa Ireland nchini, wametia saini makubaliano ya miradi miwili yenye thamani ya dola za Marekani milioni 1.4, inayohusu jinsia, ulemavu, hali ya kijamii na uchumi.

Kwa mujibu wa makubaliano hayo, mtazamo mkuu ni kuchambua takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 na kuisaidia jamii mkoani Kigoma.

Mwakilishi wa UNFPA nchini, Mark Bryan Schreiner, ameyasema hayo wakati wa kuadhimisha Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia zilizofanyika jijini Dar es Salaam.

Inaelezwa, miradi hiyo ya miaka miwili, inatarajiwa kutekelezwa kuanzia mwaka ujao hadi 2024, ubalozi wa Ireland ukitoa ruzuku ya Dola za Marekani 200,000 inayolenga kuimarisha uwezo wa kitaifa wa kufanya uchambuzi wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022.

"Mradi unalenga kusaidia matumizi ya takwimu za idadi ya watu kwa ajili ya kupanga ushahidi, kuimarisha uwezo wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu kuchambua zaidi takwimu za Sensa ya mwaka 2022 kuhusu masuala ya jinsia, ulemavu na hali ya kijamii na kiuchumi," anasema.

Mwakilishi huyo wa UNFPA, anaongeza kuwa, mradi mwingine wa mwaka mmoja utakaotekelezwa kuanzia mwaka huu hadi ujao, wenye thamani ya dola milioni 1.2 (Sh.) unalenga kusaidia wakazi wa wilaya tano za mkoa wa Kigoma.

> "Hii imeunda seti nono ya data ambayo itawezesha serikali na washirika wake kupanga na kutekeleza sera katika miaka ijayo ambazo zinakidhi mahitaji ya idadi ya watu inayoendelea na inayoongezeka.

Mark anaeleza kuwa, dira ya mradi ni kuwawezesha wasichana, vijana na wanawake katika afya na haki za ngono na uzazi, akisena: " Mradi huo utaongeza uwezo wa kitaifa na kujenga uungwaji mkono katika juhudi zinazofanywa na watendaji wa ndani kwa manufaa ya watu nchini."

Pia anaeleza kuwa, serikali pia itashiriki katika utekelezaji wa miradi hiyo miwili, itakayojumuisha wadau mbalimbali wa maendeleo.

**BALOZI IRELAND**

Balozi wa Ireland nchini Tanzania, Mery O'Neill, anaipongeza serikali nchini kupata mwitikio kwa wastani asilimia 99.9 katika kipindi cha kuhesabu kura.

Pia anaipongeza UNFPA, huku akiwataka wadau wengine wa maendeleo kuwa sehemu ya juhudi za kiserikali katika kukuza usawa wa kijinsia, afya, uzazi na haki nchini.

Kwa muda mrefu, UNFPA na ubalozi wa Ireland zimekuwa zikishirikiana, ikirejewa kuanzia mwaka 2018 hadi sasa, mradi wa mkoani Kigoma unaozingatia afya na haki za jinsia na uzazi, umeshafikia zaidi ya vijana 24,000 na wajawazito 82,000 katika wilaya za mkoani humo.

Anasisitiza dhamira yao ya pamoja ni kushughulikia usawa wa kijinsia nchini Tanzania, kufanya kazi na serikali pia na washirika wa ndani ya nchi.

Mery anaeleza kuwa Ireland na UNFPA wana historia ya kufanya kazi pamoja duniani kote, katika kukuza usawa wa kijinsia, kusaidia afya na haki za ngono na uzazi na kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia.

"Hapa Tanzania, Ireland inafanya kazi katika ngazi ya kitaifa na katika mikoa muhimu ya Tanga, Dodoma, Kigoma na Zanzibar," anafafanua, akiwa na ziada kwamba mjini Kigoma, Ireland imesaidia mashirika ya Umoja wa Mataifa, ikiwamo UNFPA, yanayofanya kazi chini ya mpango wa pamoja wa Kigoma tangu mwaka 2018.

Anaeleza, lengo kuu mjini Kigoma ni kuendeleza upatikanaji haki na afya ya uzazi na jinsia, pia kupunguza vifo vya uzazi, huku wakikabiliana na unyanyasaji wa kijinsia, kupitia fursa kamili za kijamii.

"Safari ya kuelekea usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake inaweza kuwa ndefu na wakati fulani, ambayo tunaweza kuthamini mafanikio na nyingine, ambayo tunapambana na vikwazo na kurudi nyuma," anasema.

"Ubalozi wa Ireland na UNFPA tumefanya kazi pamoja na kusaidiana katika safari, hasa katika kutekeleza programu ya 'ujana wangu, nguvu yangu' katika kipindi cha miaka minne iliyopita," anafafanua.

Balozi Mary anaahidi kwamba, wataendeleza kazi zao chini ya Mpango wa Pamoja wa Kigoma, kwa kuzingatia kuwawezesha vijana na hasa wasichana katika mpango huo. Ireland imeahidi kutoa Paundi milioni 1.2 mwaka huu na mchango wao tangu mwaka 2018, inafika Paundi milioni 5.7.

Anasema safari hii, wameongeza kipengele kipya cha kazi ya ushirikiano wao na UNFPA, akikitangaza kwa jina 'Takwimu Bora kwa Maendeleo Endelevu' ni mradi wa miaka miwili unaoimarisha uwezo wa Tanzania kuchambuaa Sensa ya Watu na Makazi ya 2022.

Katika hilo Balozi Mary anaipongeza serikali nchini kufanikisha kufanyika Sensa ya Watu na Mkazi ya mwaka huu kwa ufanisi kwa asilimia 99.9 katika kipindi cha kuhesabu.

"Hii imeunda seti nono ya data ambayo itawezesha serikali na washirika wake kupanga na kutekeleza sera katika miaka ijayo ya idadi ya watu inayoendelea na inayoongezeka," anatamka na kuongeza:

"Ireland ina furaha kutangaza kutoa Pauni milioni mbili kwa UNFPA, ambazo zitasaidia mashirika ya takwimu nchini Tanzania, hasa Ofisi ya Taifa ya Takwimu kufanya uchambuzi zaidi wa takwimu za mwaka 2022 za idadi ya watu na makazi, ikiwa ni pamoja na suala la ulemavu wa usawa wa kijinsia, kijamii na kiuchumi."

Balozi anaeleza kwamba mtazamo mkuu ulioko ni kwamba, hakuna mtu anayepaswa kuachwa nyuma katika kupata huduma bora, ili kuboresha maisha yake ikionyesha mada ya kampeni ya siku 16 ya mwaka huu ya kila jambo muhimu katika maisha.

Anasema, mchanganuo wa sensa utaiwezesha serikali kuelewa mahitaji mahususi ya wanawake, wanaume wasichana, wavulana na watu wote binafsi na makundi yenye mahitaji maalum wakiwamo watu wenye ulemavu.

Anasema matokeo ya uchambuzi yatawezesha matumizi bora ya ahadi za kitaifa kuhusu Tanzania kimataifa na kikanda pamoja na sera na programu zake za kitaifa kama vile

Mpango wa kitaifa wa utekelezaji wa ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

AFYA

# Madaktari, wauguzi wasimulia shida yao hospitalini kuwahudumia viziwi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

VIZIWI na wenye usikivu hafifu, ni sehemu ya makundi ya watu wenye ulemavu wanaohitaji huduma maalumu, hususani hospitalini, mahakamani, vituo vya mabasi na shuleni, ili waweze kupata huduma kama yalivyo makundi mengine na kuondoa dhana ya unyanyapaa.

Matatizo aliyo nayo kiziwi, humkwaza katika mawasiliano ndani ya mazingira anayoishi, hivyo inamwathiri kwa njia nyingi ikiwamo nyanja za elimu, uhusiano na maendeleo ya kijamii, hata akashindwa kupata huduma stahiki au kwa ufasaha, pale anapofika katika sehemu za mahitaji; vituo vya afya au mahakamani.

Kwa kuwa matatizo ya viziwi zaudi ya kimawasiliano na hayaonekani kwa macho, kuna hali inayojitokeza ya kusahaulika katika utoaji huduma na wanapofika hospitalini kupata huduma, wanahudumiwa na wauguzi wasiojua namna sahihi ya kuwasiliana nao.

Ni hali imekuwa ikisababisha shida kwao katika kupata huduma tofauti zikiwamo za kimatiabu, na kuliibua kundi la watoa huduma kupaza sauti na kuyataka mafunzo ya lugha za alama, ili kupata ujuzi wa namna ya kuwahudumia.



Mwalimu wa lugha ya alama kutoka TAMAVITA, Carlos Mgulukwenda, akitoa elimu ya lugha ya alama kwa wauguzi wa Hospitali ya Manispaa ya Kahama na wanafunzi 50 wa chuo. **PICHA: SHABAN NJIA**

### SAUTI ZA WAUGUZI

Muuguzi wa Hospitali ya Manispaa ya Kahama, Joyce Michael, anasema, amekuwa akikutana na wagonjwa wa aina hiyo, lakini anapata wakati mgumu wa kuwahudumia, pale anapozungumza nao huku akiwafuatilia mdomo kuangalia namna anavyotamka na ugonjwa anaoumwa.

Anasema, kuna wakati wanalazimika wanawatumia ndugu na jamaa zao katika kutafsiri kile mgonjwa anakihitaji na wanafanya hivyo kwa sababu, wao wanaishi nao na wanajua namna ya kuzungumza.

Muuguzi, Omary Juma, anasema wanatumia uzoefu kuwasiliana na baadhi ya wasiosikia wakitumia njia ya kuangalia na ishara kuanzia kinywa na nyinginezo, hata hivyo bado inakuwa ni vigumu kuelewa kwa haraka anaumwa ugonjwa gani.

Naye Mwanaidi Ali, mwanachuo wa mwaka wa tatu ngazi ya stashahada katika Chuo cha Uuguzi Kahama, anasema wanapata shida kuwahudumia wagonjwa wa aina hiyo ya usikivu pale wanapokuwa katika mafunzo ya vitendo hospitalini na kusababisha kukosa alama katika masomo yao.

Aidha, anasema, hata pale wanapolazimika kuwashirikisha wauguzi na madaktari ambao ni wazoefu wa kukukutana nao, pia wanashindwa kuwasaidia kwa kutokujua namna ya kuzungumza nao, hivyo anashauri ili kuondoa tatizo hilo, ni vyema serikali ikaanzisha somo hilo vyuoni, hususani kwa wauguzi na madaktari.

> Sisi kama wataalamu wa lugha za alama wengi wetu tupo mitaani tunasubiri mpaka tupate ajira za muda mfupi na hasa zinahusu watu wenye usikivu hafifu.

### NDUGU ZAO

Charles Edward, mkazi wa Nyasubi, anasema kwenye familia yao kuna mtu mwenye ulemavu huo, awali hawakufahamu namna ya kuzungumza naye, lakini kadri siku zilizovyozidi kwenda walifahamu na sasa wanaelewa vyema kumhudumia, hata pale anapoumwa wanafahamu.

Anasema, pale anapoumwa huwa wanaongozana naye katika kituo cha afya au hospitali, kwa ajili ya kutoa tafsiri ya kile anachoumwa kwa daktari anayemhudumia, ili kujua anasumbuliwa na tatizo gani na laiti kungekuwa na madaktari wanaojua namna ya kuzungumza nao, wangeelezana kwa undani zaidi.

Sakina Abdallah wa Segese anasema, kitendo cha kuwapeleka mahakamani au vituo vya afya kupata huduma, inawafanya kupoteza muda zaidi wa kufanya kazi na kujiongezea kipato, hivyo ni vyema serikali ikaajiri watoa huduma wenye kujua lugha ya alama katika hospitali, mahakamani na Mamlaka ya Kodi Tanzania (TRA) kwa ajili yao.

"Tukipata wataalamu wanaojua lugha za alama katika ofisi za serikali, basi watu wetu watapata huduma ipasavyo nasi tunapata muda wa kufanyakazi, ili kujiongezea kipato tofauti na sasa tumebaki kuwa watafsiri wa lugha baina ya mgonjwa na mtoa huduma," anasema Abdallah.

### MGANGA MFAWIDHI

Dk. Deo Nyaga, ni Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Manispaa Shinyanga, anakiri kukutana na wagonjwa wa namna hiyo na kuwapatia matibabu na kulingana na uzoefu alionao na asilimia kubwa anawatibu kwa stadi za namna ya kumtibu mtoto mchanga asiyeweza kuzungumza.

Anasema, viziwi wengine wanalazimika kuanza kuonyesha maungo yao yanayouma, mfano kichwa au miguu na wenye ndugu zao wanakuja nao hospitalini wakisaidia kufafanua kile mgonjwa anakieleza, hata ikaeleweka ipasavyo.

Nyaga anasema, wanawaopokea wagojwa wengi na hata anaiomba serikali kuanzisha mtaala mpya wa lugha ya alama kuanzia shule za msingi hadi sekondari, kama lilivyo somo la kiingereza, ili kuwapata wauguzi wenye sifa hizo.

"Wenye matatizo ya macho wako hatarini kupata tatizo la kutokusikia, kwa sababu wengi ninaokutana nao kwenye kitengo cha macho, napowauliza juu ya kutokusikia wanadai wanasikia kwa mbali, hivyo tunahitaji wauguzi na madaktari wenye ujuzi huu," anaongeza Nyaga.

### MTAALAMU LUGHA

Hosea Joseph, mtaalamu wa lugha ya alama, anasema ili kuwasaidia zaidi viziwi na watu wenye usikivu hafifu, ni bora serikali ikaajiri wataalamu wa lugha hiyo katika sehemu mbalimbali.

"Sisi kama wataalamu wa lugha za alama wengi wetu tupo mitaani tunasubiri mpaka tupate ajira za muda mfupi na hasa zinahusu watu wenye usikivu hafifu," anasema Joseph.

Anasema, kama wataalamu wa lugha hii watakuwa wengi basi elimu hiyo itaweza kutolewa katika makundi mbalimbali yanayotoa huduma na taasisi kama vile Mahakama, TRA na benki ambazo ndio zinatoa huduma kwa makundi mengi yatatoa huduma ipasavyo.

### TAASISI VIZIWI

Kwa kuona ukubwa wa tatizo hilo, Taasisi ya Viziwi Tanzania (TAMAVITA) imeingilia kati na kuchukua jukumu la kuanza kutoa elimu ya lugha za alama kwa wauguzi, wanachuo wa afya na matabibu ili kuwajengea uwezo wa kuzungumza na kundi hilo na kupata huduma vizuri.

Kelvin Nyema ni Mtendaji Mkuu wa TAMAVIT anayesema, wameanza kutoa mafunzo kwa wauguzi na matabibu kwa lengo la kuwajengea ufahamu wa mawasiliano ya lugha za alama, ili kuwa na uelewa pale wanapopata wagonjwa wa aina hiyo.

Anasema, wamejikita pia katika wanachuo wa uuguzi ngazi ya stashahada ambao ndio wanaoenda kuingia kwenye mfumo wa ajira baada ya kuhitimu, kwani wengi wao hawafahamu namna ya kuzungumza na kundi hilo likiwamo madaktari hospitalini.

Anadai kuwa, wauguzi na madaktari katika hospitali na vituo vya afya wamekuwa na tatizo la kutoelewana, hata kushindwa kutoa huduma kwa usahihi na hata kinyume na tatizo la mgonjwa.

### DAS KAHAMA

Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama, Timothy Ndanya, akifungua mafunzo ya wauguzi 50 wa Hospitali ya Manispa Kahama, anakiri kundi hilo kuwa na changamoto ya huduma na kuna wakati wanakwama, kwa sababu ya shida mawasiliano.

Anasema, serikali kwa kushirikiana na wadau wa afya imeendelea kutatua changamoto zinazoikabili sekta ya afya.

Hivi karibu Taasisi ya Viziwi Tanzania (TAMAVITA) ilitoa mafunzo ya lugha ya alama kwa wauguzi wa Hospitali ya Manispaa ya Kahama, wanachuo cha Chuo cha Uuguzi Kahama na Ofisa Matabibu wa Manispaa ya Sumbawanga mkoani Rukwa, kuwajengea uelewa wa namna ya kuzungumza na kundi hilo.

AFYA

# Unazijua faida za afya, mazoezi ya kutembea kwa kurudi nyuma?

**Na Mwandishi Wetu**

MOJAWAPO ya faida zinazoonekana za kutembea kwenda nyuma, ni uimara ulioboreshwa na usawa. Kutembea huko huwa hakulazimishi uhitaji wa vifaa maalum au uanachama wa sehemu za mazoezi, maarufu 'gym'.

Kwa wengi, kutembea ni jambo la kawaida tu. Hakuhitaji juhudi za makusudi kwa hivyo wengi hawakumbuki faida iliyo nayo kwa afya zetu.

Inazama kwamba, ikiwa mtu ataacha kutembea kawaida tu ya kutoa changamoto kwa akili na mwili akitembea kurudi nyuma, faida yake inaangukia katika manufaa ya mageuzi binafsi ya kiafya.

Shughuli za kimwili zinatajwa sio ngumu, bali iwe kawaida kwa kutembea kila siku, kunaweza kutoa manufaa mengi ya kiafya na yanaweza kuhesabiwa, kulingana na mapendekezo ya Shirika la Afya Duniani (FAO), kwamba ya kutosha ya viungo kila wiki.

Hata hivyo, kutembea ni jambo gumu zaidi kuliko wengi wetu wanavyofikiri. Kusimama wima kunahitaji uratibu kati ya mifumo ya kuona, hisia zinazohusiana na harakati ni kama vile kugeuka au kusonga haraka na mifumo ya kustahimili (ufahamu wa mahali ambapo miili yetu iko angani).

Mtu anapotembea kwenda nyuma, akili zake huchukua muda mrefu kushughulikia mahitaji ya ziada ya kuratibu mifumo hii. Hata hivyo, kiwango hicho cha juu cha changamoto huleta faida kubwa za kiafya.

Faida mojawapo ya kutembea kwenda nyuma, ni uthabiti na usawa ulioboreshwa. Mazoezi yanaweza kusaidia kuboresha mwendo wa kawaida, yaani kwenda mbele na katika kuboresha usawa, husaidia watu wazima wenye afya nzuri, pia hata walio na ulemavu wa mifupa na maungo.

Wakati wa kutembea kwenda nyuma, huchukuliwa hatua fupi na za mara kila mara, inayoboresha uvumilivu wa misuli chini ya mguu na kupunguza mzigo kwenye viungo. Mbinu hizo zimetumika hata kutambua na kutibu usawa na kasi ya kutembea kwa wagonjwa wenye matatizo ya neva au baada ya kuugua kiharusi cha muda mrefu.

Kuongeza kasi na kutembea juu au chini kwenye mteremko, kunatajwa kusaidia kubadilisha aina mbalimbali za mwendo wa viungo na misuli yao, huku wanapunguza maumivu, ikiwamo ya kisigino.

Mabadiliko ya namna ya kukaa yanayosababishwa na kutembea kwenda nyuma, nayo yanatajwa kusababisha matumizi zaidi ya misuli inayounga uti wa mgongo.



Watu wakishuka Mlima Kilimanjaro, ni sehemu ya mazoezi ya kinyume. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Kuongeza mzigo wa jumla huongeza matumizi ya misuli ya goti inayopanuka huku ukiweka mahitaji mazito kwenye moyo na mapafu kwa muda mfupi.**



Mazoezi ya kutembea kinyume.

Hizo zinaonyesha kwamba, kutembea kwenda nyuma kunaweza kuwa zoezi la manufaa kwa watu wenye maumivu ya muda mrefu ya sehemu ya chini ya mgongo.

Mbinu hiyo imetumika hata kutambua na kutibu usawa na kasi ya kutembea kwa wagonjwa wenye matatizo ya mishipa ya mwili, au baada ya kupata kiharusi cha muda mrefu.

### MABADILIKO YANAYOTUMIKA

Manufaa ya kubadilisha maelekezo, si ya matibabu pekee watafiti wanagundua manufaa mengine. Ingawa kutembea kawaida kunaweza kusaidia kudumisha uzito sahihi, kutembea kwa kurudi nyuma kunatajwa kuwa na ufanisi zaidi.

Utafiti mmoja unaonyesha, kupunguzwa mafuta ya mwili kwa wanawake waliomaliza mafunzo ya kukimbia kwa wiki sita au kufanya mazoezi ya kutembea kwa kurudi nyuma.

Mtu anapojiamini kwa kutembea kurudi nyuma, kusonga mbele na kukimbia, kwa namna hiyo kunaweza kuongeza mahitaji hata zaidi.

Ingawa mara nyingi husomwa kama zana ya urekebishaji, kukimbia kurudi nyuma huongeza uimara wa misuli ambayo ni muhimu kwa kunyoosha goti, sio tu kwamba hutafsiri kwa kuzuia majeraha, pia kwa uwezo wa kutoa nguvu na utendaji.

Kukimbia kwa kurudi nyuma kwa kasi, hupunguzwa nishati inayotumiwa wakati wa kusonga mbele. Maboresho hayo yana manufaa hata kwa wakimbiaji wenye uzoefu, ambao tayari wana mbinu ya kukimbia kwa ufanisi zaidi.

Ikiwa kutembea kurudi nyuma inakuwa rahisi sana na mapungufu ya nafasi yanaonekana kufanya mazoezi ya kukimbia huku, njia nyingine ya kuongeza ugumu ni kuanza kuburuta uzani.

Kuongeza mzigo wa jumla huongeza matumizi ya misuli ya goti inayopanuka huku ukiweka mahitaji mazito kwenye moyo na mapafu kwa muda mfupi.

Utembeaji kinyume na uzani, kunatajwa kunaweza kuboresha nyakati za kawaida za kukimbia kwa wanariadha wachanga.

Kutembea kwa gari la kuteleza na kukirudisha nyuma kuna hatari ndogo ya kuumia, kwani matokeo yanayoyowezekana ikiwa tumechoka kupita kiasi ni kwamba hakitasonga.

Lakini kwa uzani mwepesi, aina hiyo ya mazoezi inaweza kutoa kiwango cha kutosha cha upinzani ili kuchochea uboreshaji mkubwa katika nguvu za mwisho zile kidogo.

Kwa uzani wa kuburuta chini kama ya uzito wa kawaida, kwa nafasi sahihi ya kukimbia, zinaweza kupatikana kati ya wanariadha wachanga.

### NAMNA YA MAZOEZI

Ni safari ya kutembea kurudi nyuma, si ngumu, lakini haimaanishi kuwa ni rahisi. Hivyo, mtu anaongozaje, ni utaratibu wake wa mazoezi?

Mtu anaporudi kinyume, kuna uwezekano mkubwa wa kukutana na vizuizi, pia hatari anazoweza kugonga au kuanguka nayo.

Kwa hivyo, kwa ajili ya usalama, ni bora mtu akaanza na ndani ya nyumba, ambako anajua hutagongana na kitu au mtu au afanye mazoezi hayo katika sehemu iliyo wazi na tambarare.

Kisha anatakiwa kugeuza mwili wake na kutazama juu ya bega lake, kichwa na kifua kinaelekea juu akinyoosha kidole chake kikubwa nyuma kwa kila hatua, anausonga mguu wake kutoka kwenye vidole hadi kisigino.

Mara tu anapokuwa na ujasiri zaidi, anaweza kuharakisha, kuhakikisha kuwa unatumia reli za mwongozo inapohitajika. Ikiwa unatumia uzito, anaanza na uzito wa chini.

Si lazima mtu akafanya safari nyingi, bali ni muhimu kutembea, badala ya kufanya safari ndefu kwa umbali usiozidi mita 20 wakati anaanza.

***• Kwa mujibu wa taarifa kimataifa.***

AFYA

# Ulivyo ukubwa wa tatizo la kuoza meno hadi kwenye shida ujauzito

Na Mary Geofrey



Mgonjwa wa meno kuoza.

TAKWIMU zinaonyesha kuwa magonjwa ya kinywa na meno yameendelea kuwatesa Watanzania wengi. Asilimia 76.5 ya watu wazima wameoza meno yao, huku asilimia 31.1 ni ya watoto walioza meno.

Mkurugenzi Msaidizi, Huduma za Kinywa na Meno, Wizara ya Afya, Dk. Baraka Nzobo, anasema asilimia 62.8 ya watu wazima wana magonjwa ya fizi kama vile kutoa damu, harufu mbaya na asilimia 57.4 ya watoto wana magonjwa ya fizi.

Anasema magonjwa hayo mawili ni ya kinywa na meno yanayoongoza kusumbua watu wengi nchini na duniani kwa ujumla.

Hapo anataja jumla ya watu bilioni 3.5 duniani wanasumbuliwa na magonjwa ya kinywa na meno na kati yao, watu wazima bilioni mbili na watoto milioni 520 wana tatizo la kuoza meno yao duniani.

Dk. Nzobo anasema, kila mwaka Tanzania imekuwa ikihudumia idadi kubwa ya wagonjwa wenye matatizo ya kuoza meno na takwimu zilizoko Wizara ya Afya kutoka vituo vya matibabu, ambavyo ni hospitali, kliniki na vituo vya afya vya umma na binafsi).

Anasema takwimu hizo zinaonyesha ongezeko la Watanzania wenye matatizo ya kuoza meno na magonjwa ya fizi kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2017 hadi 2021: mwaka 2017 (kulikuwa na wagonjwa 766,604 walioza meno), mwaka 2018 (kulikuwa na wagonjwa 811,865 walioza meno), mwaka 2019 (kulikuwa na wagonjwa 860,714 walioza meno), mwaka 2020 (kulikuwa na wagonjwa 858,452), mwaka 2021 (kulikuwa na wagonjwa 839,324).

"Hali hii inaonyesha kuwa tatizo la kuooza meno ni kubwa nchini kwani idadi hiyo ni ya wagonjwa wapya walioamua kwenda kupata huduma. Lakini bado idadi kubwa ya wananchi wanaishi na meno yaliooza bila kwenda kupata matibabu hospitali," anasema.

Anaeleza kwa kipindi hicho cha mwaka 2017 hadi 2021 idadi ya wagonjwa wenye magonjwa ya fizi walikwenda kutibiwa hospitalini walikuwa wengi zaidi.

Dk. Nzobo anaeleza kuwa, mwaka 2017 (wagonjwa 79,753), mwaka 2018 (wagonjwa 92,680), mwaka 2019 (wagonjwa 108,686), mwaka 2020 (wagonjwa 108,764) na mwaka 2021 (wagonjwa 116, 543).

"Hao ni baadhi tu ya watu waliojitokeza kwenda kutibiwa magonjwa ya fizi kwenye vituo vya kutolea matibabu. Bado idadi kubwa ya wananchi wanatembea wakiwa na magonjwa ya fizi bila kutibiwa," anasisitiza.

> Hivyo tunashauri tuzingatie sana usafi wa vinywa vyetu kwa kupiga mswaki angalau mara mbili kwa siku, asubuhi na usiku kabla ya kwenda kulala kwa kutumia dawa ya meno yenye madini ya floridi.



Fizi inayotoa damu: **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Anasema magonjwa hayo ya kuoza meno na magonjwa ya fizi yanasababisha Watanzania wengi kushindwa kufurahia maisha yao ya kila siku.

Anasema katika utafiti wa Kitaifa wa Magonjwa ya Kinywa na Meno (National Oral Health Survey, 2020) uliofanyika mwaka 2020, ulionyesha kuwa; asilimia 33.3 ya watu wazima hushindwa kula, asilimia 21.9 hushindwa kupata usingizi usiku, asilimia 19.7.

Anasema pia hushindwa kusafisha meno yao na asilimia 14 hushindwa kuongea vizuri wanapokuwa wameshambuliwa na magonjwa hayo. Kwa upande wa watoto; asilimia 19.7 hushindwa kula, asilimia 13.1 hushindwa kabisa kusafisha meno yao na asilimia 7.9 hushindwa kulala usiku.

### KUATHIRI MIMBA

Magonjwa ya fizi yamekuwa na athari kubwa kwa kinamama wajawazito kwa sababu, vimelea wa wadudu aina ya bakteria na sumu zao wanauwezo wa kusafiri kwenye damu kutoka mdomoni na kupenya kwenye mfuko wa mimba kwa mama mjazito.

Dk. Nzobo anasema bakteria hao na sumu zao husababisha mfumo wa mimba kushindwa kuruhusu ukuaji mzuri wa mtoto aliyepo tumboni hivyo kusababisha mama mjamzito kujifungua mtoto mwenye uzito mdogo.

Anasema, vilele magonjwa ya fizi husababisha mimba kuharibika, kifafa cha mimba na pia mama mjamzito kujifungua mtoto njiti.

Mtaalamu huyo anasema, magonjwa ya fizi yasipotibiwa kwa wakati pia husababisha harufu mbaya mdomoni, meno kulegea na kung'oka, fizi kutoa damu na kutengeneza utando mgumu uitwao ugaga kati ya jino na jino au jino na fizi.

Anafafanua zaidi kuwa, mama mjamzito ambaye ana meno yaliyooza ana uwezo mkubwa wa kujifungua mtoto ambaye baada ya kuanza kuota meno, yana uwezo mkubwa wa kuanza kuoza au kutoboka.

Anasema jino liliooza lisipotibiwa kwa wakati, nje ya kuleta maumivu makali kwa mgonjwa; jino lililooza huweza kuleta jipu la jino ambalo humsababishia mgonjwa kuvimba shavu na maumivu makali.

Anafafanua kuwa, usaha wa jipu la jino huweza kukimbilia kwenye mapafu na pia huweza kupanda kwenye fuvu la kichwa, pia usaha wa jipu la jino huweza kusababisha kifo kama mgonjwa atachelewa kupata matibabu sahihi toka kwa daktari wa kinywa na meno.

"Hivyo tunashauri tuzingatie sana usafi wa vinywa vyetu kwa kupiga mswaki angalau mara mbili kwa siku, asubuhi na usiku kabla ya kwenda kulala kwa kutumia dawa ya meno yenye madini ya floridi," anaeleza.

Dk. Nzobo anawashauri wananchi wahudhurie kwenye vituo vya kutolea huduma ili kutibiwa magonjwa ya fizi na pia kutibiwa meno yao yaliyooza na siyo kukimbilia kuyang'oa.

Anasema, serikali kupitia Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais (TAMISEMI), inaendelea kuboresha huduma za kinywa na meno, kwa kuajiri ya madaktari wa kinywa na meno, kuboresha kliniki za kinywa na meno na kununua dawa na vifaa tiba vya kinywa na meno katika ngazi zote za kutolea huduma kuanzia vituo vya afya, hospitali za halmashauri, hospitali za rufani za mikoa, rufani za kanda na Hospitali ya Taifa Muhimbili.

AFYA

# Vijue vyanzo vya magonjwa meno

Na Mwandishi Wetu

MATATIZO ya meno ni shida au magonjwa yanayotokea baada ya bakteria na wadudu kuwapo mdomoni. Hiyo imamfanya mtu kuwa na maumivu makali kwenye meno na mpaka kutoa damu au harufu mbaya na kuathiri meno.

Watu wengi wana tatizo la meno ila wanatofautiana ukubwa.



Mgonjwa wa meno akitibiwa. **PICHA: MTANDAO**

### AINA ZA MAGONJWA

• Meno kutoboka; ni tatizo linalotokea kwa kuwapo bakteria kwenye meno na kuharibu meno. Bakteria hao wanatokana na kuwapo mabaki ya vyakula hasa vya sukari nyingi. Mabaki yasipoondolewa, bakteria huzalisha tindikali ambayo huharibu meno na kutengeneza vitobo.

• Meno kuvunjika, ni tatizo huwatokea watu wakionekana na baadhi na vipande kutoonekana, jino laweza kuwa nusu au robo tatu. Mara nyingi hilo sio tatizo la kuathiri fizi, ila linamnyima mtu uhuru. Pia ulimi ukigusa unahisi kama ni kitu chenye ncha.

• Meno kusagika au kupungua kimo;- tatizo hutokea mtu akiwa amelala, hata mchana akiwa na mawazo, hasira au hisia ambapo meno hugusana na kusagana. Meno huweza kupungua kimo na kwisha taratibu na kupungua kimo husababisha maumivu ya meno na kubadilika rangi.

• Tatizo la fizi; katika fizi kuna kuwa na maumivu, kama vidonda au kutokwa damu, kuwa na usaa au uchafu. Mara nyingi hutokana na bakteria wanaokuwa kwenye mabaki ya chakula. Mtu mwenye hilo tatizo hutoa harufu mbaya.

• Meno kuharibika, fizi kuachia na kulegea; ni pale meno yanapoonekana sio ya kawaida; yaani yanakuwa yamebadilika rangi, fizi kupungua, fizi kutoka damu na meno kulegea. Tatizo laweza kuwa kubwa na kutotibika.

• Meno kufa ganzi na kushindwa kuhisi; huwakuta wengi katika mazingira ya baridi sana au joto sana, pia wakila baadhi ya vyakula vyenye uchachu, hata sukari. Ni dalili za kuharibika jino ndani au nje

• Harufu mbaya na kupumua vibaya - Hili tatizo hutokea kwa mtu kutoa harufu mbaya mdomoni ambayo huwakela watu wengi, hii hutokea pale anavyokuwa na mabaki ya vyakula kwenye mdomo, kutofanyia usafi meno na mdomo pia, kuwa na tatizo la meno au mdomo.

• Utando mdomoni - Hili ni tatizo ambalo mdomoni huwa na weupeweupe usioeleweka kama ute, mara nyingi huwatokea watu wasio na kinga imara hasa wenye matatizo ya kiafya kama kisukari, UKIMWI, Kansa (Saratani), Asthma. Hii hali huondolewa na dawa.

• Meno kuwa na rangi ya njano, kaki au kahawia - Hili tatizo limeonekana kuchukua baadhi ya maeneo, ambapo idadi kubwa ya watu wameonekana wakiwa na meno yenye rangi inayoendana. Hii ni kwasababu ya vyakula na maji ya kunywa yanayopatikana maeneo hayo kuwa na uwingi wa aina fulani ya madini hasa Fluoride.

### CHANZO CHAKE

Chanzo cha magonjwa ya meno kwa asilimia kubwa ni mitindo ya maisha;

• Kutokusafisha mdomo pamoja na meno

• Ulaji holela wa vyakula vyenye mafuta mengi na sukari nyingi

• Kutokupata tiba ya kisukari na ugonjwa wa moyo

• Kuvuta sigala

• Kuwa na magonjwa yanayopunguza kinga ikiwamo na UKIMWI

• Kubadilika kwa baadhi ya homoni

• Umri

• Utumiaji wa dawa zenye kemikali nyingi huharibu mfumo wa vimiminika vinavyofanya mmeng'enyo

• Historia magonjwa yanayoambatana na meno katika familia

• Mazingira

### DALILI ZA MWENYE TATIZO

Mara nyingi dalili hujionyesha wazi, wengi;

• Meno kuuma wakati wa kula au muda wa baridi au joto

• Kutokwa na damu kwenye fizi

• Meno kuanza kulegea na kuachana na fizi

• Kutoa harufu mbaya mdomoni, hii huonesha kuna tatizo

• Meno kubadilika rangi mfano nyeusi, njano, kahawia na rangi zingine zisizo za kawaida

• Fizi huwa nyekundu kama damu ikiwezekana kuna vidonda

• Mdomo kuwa mkavu

• Meno kufa ganzi

• Meno kuchomoka au kutikisika

### KUEPUKA MAGONJWA

• Ondoa mabaki ya chakula kwa kusukutua mdomoni na maji baada ya kutoka kula pia kunywa maji mengi dakika 30 baada ya kutoka kula

• Safisha meno yako hata mara mbili kwa siku

• Punguza mawazo

• Usivute sigara

• Punguza au acha kunywa pombe

• Kula vizuri vyakula bora hasa asilia na sio vyakula vyenye kemikali, vyakula vyenye mafuta mengi na sukari nyingi

***• Kwa mujibu wa ripoti za mtandao,***

Dondoo: Kulia


1. Kinga
5. mji wake mkuu ni Nairobi
6. Rais mweusi Marekani
8. matokeo mabaya
9. mwanamke mzee sana
11. topiki
13. wingi wa neno kosa
15. jambo ambalo ni wajibu kwa mtu kulitekeleza
16. sali
17. baa

Chini:

1. gimba lenye nuru angani
2. mwanadamu wa kwanza
3. tuliza macho mahali pamoja
4. Neema
5. mfuasi wa chama cha siasa
7. Mimea
10. fahamu jambo
11. tafsiri ya kitu
12. fikira inayoeleza jambo fulani
13. Jimbo
14. kaba

## CHEMSHABONGO NA -00 28 00-


Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com




Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

MKATE
ACHAMA
MKATO
OMBEA
TANGO
ADHABU
MWANZO
AZANIA
MATAA
KWANZA
WAKATI
KIAMA
TABAKA

UTU
AGO
KAA
WAA
KAZI




Majibu toleo lililopita





# Watoto wenye ulemavu walilia upendo

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WATOTO wenye ulemavu Mkoa wa Mbeya, wameiomba jamii kuwapa upendo na ukaribu bila kujali hali walizonazo ili kufurahia maisha kama watoto wengine wasiokuwa na ulemavu.

Wakizungumza na Nipashe kuhusu siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia, walisema watoto wenye ulemavu wana uwezo wa kuleta maendeleo katika familia na jamii ikiwa hawatatengwa na kunyanyapaliwa.

Froida Chaula, mwenye ulemavu wa viungo alisema licha ya changamoto hiyo anajitengenezea kipato chake kwa kujishughulisha za ushonaji vikapu, culture na kutengeneza rozari.

Aisha Yohana, alisema licha ya ulemavu wa kutokuona wazazi wake hawakumtenga walimpeleka shule na kumtimizia mahitaji yake na hivi sasa anajishughulisha na kibiashara.

Alisema mtu yeyote anaweza kuwa na ulemavu wakati wowote na kwamba jamii inapaswa kutambua haki za watu hao.

Ofisa Maendeleo ya Jamii kutoka Kituo cha Shirika la Watumishi wa upendo, Nyumba ya Mtakatifu Guanella, Iwindi, Mbalizi wilayani Mbeya, Jane Sanga, alisema watoto wenye ulemavu wana uwezo wa kufanya shughuli za uzalishaji na kujipatia kipato ikiwa wataendelezwa vipaji vyao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika lisilokuwa la kiserikali la Sauti ya Mama Afrika (SAMAFO), Tabitha Bugali, aliwashauri wazazi na walezi kuwa karibu na watoto ili kutokomeza unyanyapaa na ukatili kwa watoto.

Mwenyekiti wa Kituo cha Taarifa na Maarifa Kata ya Nsalala, Felister Kaisi, alisema wazazi wanaowakatia tamaa watoto wao wana ulemavu zaidi na kutakiwa kuachana na dhana potofu.

# Shughuli za binadamu zakausha vyanzo vya maji

**Na Grace Mwakalinga,**

MBEYA

ASILIMIA 90 ya Hifadhi ya Msitu wa Mlima Mbeya imeharibiwa kwa shughuli za kibinadamu ikiwamo kilimo, uchomaji mkaa na uingizaji wa mifugo na kusababisha kukauka kwa baadhi ya vyanzo vya maji vinavyohudumia wakazi wa Jiji la Mbeya na vitongoji vyake.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, historia ya mlima huo inaonesha ilikuwa na vyanzo vya maji zaidi ya 49, lakini kwa sasa vimebaki visivyozidi 20.

Kutokana na uharibifu wa mazingira katika safu za Mlima Mbeya, Dk. Chuachua ameelekeza wanyama wote wanaoingizwa na kuchungwa ndani ya hifadhi wakamatwe na kupigwa mnada ili kukomesha tabia ya wafugaji wanaokwenda kulisha mifugo yao ndani ya hifadhi hiyo.

"Nataka wananchi wote wanaoendesha shughuli za kilimo, ufugaji na uchomaji mkaa ndani ya hifadhi ya msitu wa Mlima Mbeya waondoke mara moja, watakaokamatwa wakifanya shughuli hizo wachukuliwe hatua kali za kisheria," alisema Dk. Chuachua.

Hata hivyo, Ofisa Uhusiano wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya, Mbeya-UWSSA, Aminael Julius, alisema athari ya kukauka kwa vyanzo vya maji.

"Kukauka kwa vyanzo vya maji kumesababisha wananchi wa Jiji la Mbeya kupata mgawo wa maji kwa sababu uzalishaji umepungua kutoka lita 10,000 kwa siku mpaka lita 4000," alisema Aminael.

Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi wa Misitu nchini TFS, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Cosmas Ndakidemi, alisema wameanza kusimamia sheria za uhifadhi wa msitu huo.

Alisema Hifadhi ya msitu wa safu za Mlima Mbeya, inasimamiwa na Wakala wa Huduma za Hifadhi ya Misitu nchini (TFS), ambao wanaeleza hatua wanazochukua kunusuru msitu huo.

Pia wameanza kusimamia upandaji miti katika msitu huo ili kurejesha uoto wa asili uliohar-ibiwa kutokana na shughuli za kibinadamu.

Wananchi wanaoishi kuzunguka Msitu wa Hifadhi ya Mlima Mbeya walisema uharibifu wa msitu huo unasababishwa na wenzao wenye tamaa ya kupata fedha za haraka kwa kuingia ndani na kuchoma mkaa bila kibali.

Raphael Mwakalenga, alisema shughuli za kilimo ndani ya hifadhi zinafanywa na watu wanaotoka mjini hususani katika Jiji la Mbeya kwenda kutafuta ardhi



Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, akipanda mti katika Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) Kampasi ya Mbeya juzi, ikiwa ni hatua za kuunga mkono jitihada za serikali kutunza mazingira, kabla ya mahafali ya tisa ya chuo hicho. Kulia ni Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Emmanuel Mjema. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Tani 30 mbolea zaingia Mbeya kutoka Kenya

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

TAYARI tani 30 za mbolea ya kupandia na kukuzia zimeingizwa kutoka nchini Kenya kupitia Kampuni ya Mbolea ya SBL ambayo imeanza kutolewa kwa wakulima wa mkoa huo katika msimu huu wa kilimo.

SBL imeingia ubia na Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC), kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na uhakika wa masoko nchini Kenya.

Akizungumzia hatua hiyo, Kaimu Meneja wa TFC, Kanjela Mroba, alisema kuwa tayari tani 30 zimegawiwa kwa wakulima na kwamba matarajio ni kuagiza tani 3,000 kulingana na mahitaji ya wakulima kwa sasa.

"Tulipokea tani 30 za majaribio ambayo itatolewa bure kwa baadhi ya wakulima na tayari tumefanya utafiti ni mbolea inayofanya vizuri katika uzalishaji hususan kwa zao la mahindi," alisema Mroba.

Mkurugenzi wa kampuni ya SBL, Joe Kariuki, alisema ujio wa mbolea ni fursa kwa wakulima kwa kuwa ina uwezo wa kuzalisha mazao ikiwa ni pamoja na kurejesha ubora wa udongo ulio athirika kwa matumizi yasiyo sahihi.

Alisema pia watatoa elimu kwa wakulima huku TFC ikiwa inasimamia usambazaji na masoko na kwa nchi ya Kenya watatumia mfumo wa kubadilishana mbolea na mazao kwa asilimia 100.

"Mbolea hii inafanya vizuri sana katika uzalishaji na tayari tuna vituo 150 nchini ambavyo vinasambaza itauzwa kwa gharama nafuu ili mkulima aweze kumudu," alisema Mroba.

Mkulima wa Kijiji cha Iwindi wilayani Mbeya, Fredy Aloyce, alisema ujio wa kampuni za mbolea utasaidia wakulima kurejesha matumaini na kuzalisha mazao ya kimkakati.

"Tunaomba serikali kupitia Wizara ya Kilimo iongeze ushindani wa kampuni za pembejeo za kilimo pamoja na kudhibiti mfumuko wa bei kwa mawakala ambao wamekuwa mwiba kwa wakulima na kukatisha tamaa katika uzalishaji.





# CWHRDS ilivyochangia uongozi, uzazi salama wanawake

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MTANDAO wa Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu (CWHRDS), umechangia kwa zaidi ya asilimia 90 uongozi kwa wanawake, kumiliki mali na kujifungua kwenye mazingira salama.

Mratibu wa wa kitaifa wa CWHRDS, Hilda Dau, alibainisha hayo juzi jijini hapo wakati wa maadhimisho ya siku ya kimataifa ya wanawake watetezi wa haki za binadamu.

"Tumechangia kwa asilimia 99 kuwapo wanawake sehemu za uongozi, kumiliki mali na hata kujifungua kwenye mazingira salama," alisema.

Alisema mpaka sasa wamewafikia wanawake watetezi 120 ambao wamejengewa uwezo kuhusu haki za binadamu.

"Tumetoa misaada ya kisheria na ya kibinadamu kwa wale waliokutana na madhira hasa wakati wa kutetea haki za wanawake na makundi maalum," alisema.

Pia wanawake watetezi walikuwa mstari wa mbele, lakini mazingira ya kufanyia kazi bado yana upungufu.

Naye mwakilishi kutoka Wizara ya Katiba na Sheria, Dk. Anne Malipula, alisema wanawake watetezi wa haki za binadamu wana nafasi kubwa kukuza na kulinda haki za binadamu.

"Serikali inatambua mchango wenu wa kuboresha maisha ya wanawake wa Tanzania, mnaisaidia sana serikali kufuatilia haki za wanawake na wasichana.

Mwakilishi kutoka Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Lissa Kagaruki, alisema wanawake watetezi wanapitia vikwazo vingi.

"Kabla ya mwaka 2019 watetezi wanawake walikuwa waoga sana lakini kupitia mitandao wamekuwa na ujasiri.

"Tunahitaji sheria inayosimamia inayomtaja mtetezi wa haki za binadamu ni nani," alisema.

Mkurugezi kutoka Idara ya Sheria Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Nagu Assey, alisema kila mmoja ana wajibu wa kuhakikisha watetezi hawanyanyaswi, hawatishwi.

# Rasimu mitaala, mapitio sera elimu vyakamilika

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema rasimu za mitaala na mapitio ya sera ya elimu ya mwaka 2014, zimekamilika zinasubiri kuingia kwenye mchakato wa ndani wa serikali huku maoni ya wadau kuhusu ufundi stadi yakizingatiwa.

Prof. Mkenda aliyasema hayo juzi jijini hapo kwenye mkutano wa mwaka wa tathmini ya maendeleo ya sekta ya elimu uliojumuisha wadau wa elimu ikiwamo washirika wa maendeleo.

Alisema katika mkutano huo ameeleza mageuzi yanayofanywa na serikali kwenye sekta ya elimu katika mapitio ya mitaala na sera ili kuhakikisha masuala mbalimbali yanajumuishwa ikiwamo elimu ya ufundi stadi.

"Kama mnavyojua maelekezo tuliyopewa ni kuhakikisha elimu yetu kwa kiasi fulani lazima iongeze ufundi stadi kwenye elimu, sasa ni kwa namna gani imeongezwa itakuja kutangazwa baadaye baada ya mchakato wa ndani wa rasimu hizi kukamilika, tutahitaji kuongeza nguvu kwenye elimu ili kutoa elimu hiyo," alisema.

Alisema wadau wa maendeleo wanapojipanga kusaidia sekta ya elimu waanze kupata mwelekeo wa mageuzi yanayotaka kufanywa na serikali.

Awali, Katibu Mkuu wa wizara hiyo akifungua mkutano huo, Dk. Francis Michael, alitaja mafanikio yaliyopatikana kwenye sekta ya elimu kuwa ni ukarabati na ujenzi wa miundombinu ikiwamo madarasa, mabweni, maabara na matundu ya vyoo kwa shule za msingi na sekondari.

"Ukarabati wa miundombinu ya Taasisi za Elimu ikiwamo vyuo vikuu, kuajiri walimu 11,547, kutoa mafunzo kwa walimu 402 wanaotoa mafunzo kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum, kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania imeandaa miongozo ya utoaji wa elimu kwa kutumia TEHAMA kwa elimu ya awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu," alisema.

Pia alisema kukamilisha mpango wa maendeleo wa sekta ya elimu 2021/22 hadi 2025/26 na kutoa wito kwa washiriki kutumia vipaumbele vilivyoainishwa katika mpango huo.

"Hatutarajii kuona utekelezaji wa vipaumbele ambavyo siyo sehemu ya mpango wetu wa sekta," alisema.

Naye Faith Shayo, kutoka Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Elimu na Mwenyekiti wa wadau wa maendeleo ya elimu, alisema mkutano huo umekuja wakati muafaka ambao dunia inalenga mabadiliko na mageuzi katika masuala ya elimu.

"Tumekuja kuendelea kutoa msaada kwa serikali ya Tanzania, katika masuala ya mageuzi au kuangalia masuala ya mitaala ya elimu na sera ya elimu, wadau tupo pamoja na serikali kwa ajili ya kutoa ushirikiano ili kuleta mabadiliko kwenye sekta ya elimu Tanzania," alisema.




Mkazi wa Dar es Salaam, Hamidu Mikongo, akiwa na bango ambalo alidai kuwa anamfanyia kampeni mgombea wa nafasi ya Uenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa wajumbe kwenye Mkutano Mkuu wa 10 wa chama hicho, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wasiolipa pango ardhi kupelekwa mahakamani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imesema itawapeleka mahakamani na kubatilisha umiliki wananchi ambao hawatalipa malimbikizo ya kodi ya pango la ardhi baada ya kuisha kwa msamaha wa riba uliotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Julai mwaka huu, Rais Samia alitoa msamaha wa riba kwa kipindi cha miezi sita ambacho ukomo wake ni Desemba 31, mwaka huu.

Mkuu wa kitengo cha kodi wa wizara hiyo, Denis Masami, aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari. Alisema hatua zingine zitakazochukuliwa kunadi mali ili kufidia kodi husika na kubatilisha miliki ili zirudi kwa Rais wapewe watu wengine wenye uwezo wa kuzilipia na kuziendeleza. "Wizara kupitia waziri mwenye dhamana alitangaza msamaha wa malimbikizo ya kodi ya pango la ardhi uliotolewa na Rais Samia kwa wananchi wote waliokuwa na madeni ya malimbikizo ya kodi ya pango la ardhi walipe deni la msingi ili wasamehewe riba na msamaha huu ulianza Julai hadi Desemba," alisema.

Alisema kwa muda wa miezi mitano wananchi takribani 10,000 wamejitokeza na kunufaika na msamaha huo kwa kulipa deni la msingi.

"Takwimu zinaonesha kwa kipindi cha miezi mitano kiwango cha makusanyo pia kimeongezeka tulikuwa tunakusanya wastani wa Shilingi bilioni nane hadi 10 kwa mwezi, lakini kwa sasa wanakusanya Sh. bilioni 15 kila mwezi hivyo kuna ongezeko la theluthi nzima ya makusanyo kupitia msamaha huu," alisema.

Alisema wapo wamiliki milioni mbili wa vipande vya ardhi ambao wapo kwenye mifumo ya wizara na mwamko wa ulipaji malimbikizo hayo umeongezeka kutoka asilimia 40 hadi 60 ya ulipaji. Alitoa wito kwa wananchi muda uliowekwa na kutangazwa na serikali nafuu ya msamaha iliyotolewa na Rais Samia sasa inakaribia kwisha watumie fursa hiyo kulipa.

Alifafanua kuwa mwenye sifa ya kupata msamaha huo ni kila mmiliki wa kipande cha ardhi ambaye kimepimwa au kutambuliwa na kipo kwenye mifumo ya ukadiriaji. "Unaweza ukawa na ofa, leseni ya makazi, hati, au upo hatua za umilikishaji, lakini tayari umeshatambuliwa na upo kwenye mifumo yetu unatozwa kodi ya pango la ardhi," alisema.

Kuhusu waliochukuliwa hatua mpaka sasa alisema zipo takwimu za mashauri 3,400 yaliyoendeshwa mahakamani wengi wao asilimia 90 walilipa, zilizobaki wamefika katika hatua za ubatilisho.

"Huko nyuma kwa miaka miwili iliyopita zipo miliki nyingi ambazo tumebatilisha hasa za mashamba makubwa ambazo tumezirudisha katika serikali, tunawagawia wananchi na tunauza kwa wamiliki wapya watakaoviendeleza," alisisitiza.

Naye Mratibu wa Kodi Mkoa wa Dodoma, Letare Shoo, alisema kodi ya pango la ardhi huwa inatozwa kila mwaka kuanzia Julai hadi Desemba bila adhabu na ifikapo Januari hutozwa kwa ambao hawakufanya hivyo.

Alisema kwa Mkoa wa Dodoma wapo wananchi 150,000 ambao hawajalipa kodi muda mrefu huku 450 walijaza fomu ya msamaha na kulipa kodi ya msingi.





Katibu Mtendaji wa Baraza la Usafirishaji nchini (TSC), Sallu Johnson (wa tatu kushoto), akishuhudia baadhi ya teknolojia zilizoonyeshwa na wanafunzi wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), katika tamasha la kwanza la taaluma liitwalo Career Fair, Dar es Salaam mapema wiki hii, lililokuwa na lengo la kuwajengea uwezo wanafunzi katika kukabiliana na hali ya soko la ajira nchini kwa kukutana na waajiri. (Wa pili kushoto) ni Mkuu wa chuo hicho, Prof. Zacharia Mganilwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kiwango mavuno mazao ya baharini chaongezeka

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar, imesema kiwango cha mazao ya baharini yanayovunwa nchini kimeongezeka tangu serikali ilipotangaza sera ya uchumi wa buluu miaka miwili iliyopita.

Akizungumzia mafanikio yaliyopatikana tangu Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi, alipotangaza sera hiyo, Katibu Mkuu Wizara ya Uchumi wa Buluu Dk. Aboud Suleiman Jumbe, amesema hiyo ni dalili njema kwa Zanzibar katika kustawisha maisha ya watu wake na kuongeza pato la serikali.

Kuhusu sekta ya uvuvi, Dk. Jumbe alisema, tani 47,110 za samaki zilivuliwa mwaka 2021 kulinganisha na 38,107 mwaka 2020, likiwa ongezeko la asilimia 19.1. Alisema mchango wa sekta ya uvuvi katika pato la taifa umeongezeka kutoka Sh. bilioni 206.4 (4.5%) mwaka 2020 kufikia bilioni 236.8 mwaka 2021 sawa na asilimia 5.1.

Alisema hali hiyo inaonesha uwezekano mkubwa kwa Zanzibar kufikisha tani 65,000 za samaki mwishoni mwa mwaka 2023, ikizingatiwa serikali imeimarisha sekta ya uvuvi kwa kugawa vifaa vingi vya kisasa ili kuinua pato la wananchi na taifa. Ili kuongeza uvunaji samaki, alisema agizo la ilani ya uchaguzi ya CCM 2020/2025, imeelekeza kununuliwa kwa boti 300 zenye urefu wa mita saba kila moja na boti 277 (mita nane).BKwa upande wa kilimo cha mwani, Katibu Mkuu huyo alisema kiwango cha uzalishaji kimekuwa kikiongezeka kutoka tani 14,000 kwa mwaka, ikitarajiwa hadi mwisho wa 2023, tani 21,000 zitavunwa.

Jumbe alisema hatua kubwa imefikiwa upande wa ufugaji kaa ambapo mwelekeo kwa sasa ni kuvuna tani 200 kila mwaka.

Katika ufugaji majongoo bahari, alisema kuwa Zanzibar ilivuna na kusafirisha nje ya nchi tani 30 mnamo mwaka 2019 kabla kuibuka janga la UVIKO-19, na mwelekeo mpya ni kufikisha zaidi ya tani 50 kiwango ambacho husafirishwa na nchi ya Madagascar ambayo ndio msafirishaji mkubwa duniani wa mazao hayo kwa sasa.

Alisema katika kuongeza uzalishaji wa mazao ya baharini, serikali kupitia Ilani ya CCM imeagiza wakulima wa mwani wapewe boti 500 za urefu wa mita tano kila moja.

Aliongeza kuwa, ilani hiyo pia imeagiza kuanzishwa mashamba 60 ya kufugia kaa na 40 ya kufugia samaki, mashine moja ya chakula cha samaki na mashine 500 za boti za mwani (urefu mita 9.9).

Alisema agizo jingine ni kutoa mafunzo kwa wajasiriamali wa sekta ya uvuvi na ufugaji wa mazao ya baharini ili waweze kuendesha miradi yenye tija na ufanisi. Kwa upande wa kilimo cha mwani, alisema kiwango cha uzalishaji kimekuwa kikiongezeka kutoka tani 14,000 kwa mwaka, ikitarajiwa hadi mwisho wa 2023, tani 21,000 zitavunwa.

Alisema hatua kubwa imefikiwa upande wa ufugaji kaa na mwelekeo kwa sasa ni kuvuna tani 200 kila mwaka.

Katika ufugaji majongoo bahari, alisema Zanzibar ilivuna na kusafirisha nje ya nchi tani 30 mwaka 2019 kabla kuibuka janga la UVIKO-19, na mwelekeo mpya ni kufikisha zaidi ya tani 50 kiwango ambacho husafirishwa na nchi ya Madagascar ambayo ni msafirishaji mkubwa duniani wa mazao hayo kwa sasa.

Alisema katika kuongeza uzalishaji wa mazao ya baharini, serikali imewapa wakulima wa mwani Unguja na Pemba boti 500 za urefu wa mita tano kila moja.BPia katika maeneo mbalimbali visiwani humo, kumeanzishwa mashamba ya kufugia kaa 60 na 40 ya kufugia samaki, huku serikali ikitoa mashine moja ya chakula cha samaki na mashine 500 za boti za mwani (urefu mita 9.9).

Alisema ili kuongeza uzalishaji samaki na mazao ya baharini kwa wajasiriamali, boti 1,077 (577 za uvuvi, 500 za mwani) na mashine zimenunuliwa.

Jumbe alisema mashamba 100 ya matango bahari na mashamba 60 ya kaa tope kupitia mradi wa UVIKO-19 ujenzi umefanyika katika kuinua wazalishaji wa mazao ya baharini.

Pamoja na miradi mingine inayogusa uchumi wa buluu, katika sekta ya uvuvi, serikali imetenga Sh. bilioni 30 kwa ajili ya ujenzi wa bandari mbili za uvuvi 2022/2023.BBandari mkoa itajengwa Kizimkazi Mkoa wa Kusini Unguja na Shumbamjini, Kaskazini Pemba.

## Jumbe: Miaka 2 ya Rais Mwinyi yaleta mafanikio

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Dk. Aboud Suleiman Jumbe, amesema katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa Dk. Mwinyi, wizara hiyo imepeta mafanikio makubwa ya kiutendaji na kukuza mapato kwa wananchi.

Alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari, ofisini kwake Maisara Mjini Unguja.

Alisema kabla ya kuundwa kwa wizara hiyo leseni ya uvuvi wa bahari kuu Tanzania zilikuwa mbili na sasa leseni hizo zimefikia 32 jambo la kujivunia kwa upande wa kiutendaji.

Alisema wizara hiyo imejipanga kuhakikisha malengo waliyojiwekea yanakamilika kwa wakati na mapaka sasa serikali imetenga Sh. milioni 600 kuwajeengea uwezo wa kitaaluma wananchi na wafugaji wa mazao ya bahari.

Alisema mafanikio makubwa yamepatikana kupitia fedha za ahuweni ya UVIKO- 19 ya Sh. bilioni 36 .5 kwa kuwasaidia wananchi mbalimbali hasa wafugaji wa mazao ya bahari.

Alisema katika kuwajali wavuvi hasa wadogo, Serikali ya Zanzibar imetoa boti 1077 kwa upande wa wavuvi wagodo wapatao 577 na kwa upande wa wanawake wakulima wa mwani boti 500. Alisema hivi sasa wananchi wengi wamekuwa na mwamko wa kulima mwani, ufugaji wa samaki na matango bahari na wakulima wote hao wizara imekuwa ikishirikiana nao vyema kuwapa taaluma ya ufugaji huo.

# BAKITA, BAKIZA zatakiwa kuchangamkia fursa Burundi

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Kiswahili la Taifa (BAKITA) pamoja na Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA) yametakiwa kuchangamkia fursa za kufundisha lugha ya Kiswahili nchini Burundi ambayo tayari imeanza mchakato wa kufundishwa kwa lugha hiyo katika ngazi ya shule za msingi, sekondari hadi vyuo vikuu.

Balozi wa Tanzania nchini Burundi, Dk. Jilly Maleko, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuwa hiyo ni nafasi nyingine kwa mabaraza yaliyopewa jukumu la kukuza na kuendeleza Kiswahili nchini kuitumia kutokana na uwezo wa Tanzania katika kuzungumza lugha hiyo kwa ufasaha mkubwa na kufundisha.

Alisema Burundi rasmi imeanza kufundisha lugha ya Kiswahili katika ngazi za shule ikiwa ni hatua ya kutekeleza maagizo ya viongozi wa nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ya kutumika lugha ya Kiswahili katika vyombo vya kutunga sheria ikiwamo mabunge na ngazi nyigine.

"Wenzetu Burundi rasmi wamejipanga kuanza kukitumia Kiswahili kwa ajili ya kufundishia katika shule za msingi na sekondari pamoja na mabunge yake ambapo hiyo ni fursa nyingine muhimu kwa wataalamu wetu katika mabaraza kuzungumza lugha hiyo BAKITA pamoja na BAKIZA kutoa wataalamu wa kufanya kazi hiyo," alisema.

Dk. Maleko alisema yapo matumaini makubwa kwa nchi ya Burundi kufanya vizuri kukifundisha na kuisambaza lugha ya Kiswahili kwa sababu katika nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki nchi hiyo wananchi wake wengi wanazungumza lugha hiyo vizuri.

Alisema alipoteuliwa kuwa balozi wa Tanzania nchini Burundi mwaka 2020 wakati alipowasilisha hati zake mbele ya Rais wa Burundi, hayati Pierre Nkurunziza, mazungumzo yao yalitawaliwa kwa lugha ya Kiswahili.


"Niliwasilisha hati zangu za ubalozi mbele ya Rais hayati Nkurunziza ambapo tulipoanza kuzungumza aliniambia tuzungumze Kiswahili yeye alikuwa akizungumza kwa ufasaha mkubwa," alisema.

Dk. Maleko aliwataka wafanyabiashara kutoka Tanzania kuchangamkia fursa za biashara kwa kupeleka vyakula vya aina mbalimbali katika nchi hiyo yenye idadi ya watu milioni 12.

Alisema nchi hiyo inayo mahitaji makubwa ya chakula kutokana na udogo wake na vyakula vya nafaka aina ya mchele, maharagwe vinahitajika kwa kiwango kikubwa.

Aidha, alipongeza juhudi zinazochukuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan za kasi ya ujenzi wa reli ya SGR ambayo inakwenda moja kwa moja hadi Burundi kutoka Kigoma na kufungua zaidi fursa za uwekezaji na kibiashara.

"Nataka niwaambie wafanyabiashara kutoka Tanzania tuchangamkie fursa za kibiashara ziliopo katika nchi ya Burundi ambazo ni nyingi na matarajio yatakuwa makubwa mara baada ya kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa reli ya SGR," alisema.





Baadhi ya wafanyabiashara wadogo maarufu machinga, wakiendelea kuuza bidhaa zao eneo la Makoroboi katikati ya Jiji la Mwanza jana. Mwishoni mwa mwaka jana, serikali iliwaondoa kwenye eneo hilo na kuwapanga katika masoko rasmi, lakini kwa sasa wameanza kurejea tena. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# Wachukua hatua kukabiliana uharibifu mazingira

**Na Vitus Audax,** SENGEREMA

WILAYA ya Sengerema mkoani Mwanza, imeanza kuchukua hatua za kukabiliana na uharibifu wa mazingira na ukame uliokithiri kwa kupanda miti zaidi ya milioni 1.5 kuelekea mwaka 2023 ili kupambana na athari za kimazingira.

Katika hatua za awali wilaya hiyo kwa kushirikiana na Wakala wa Huduma za Misitu Nchini (TFS), wilayani Sengerema juzi, walipanda miti 1,800 katika Chuo cha Ufundi Stadi (VETA), huku jamii ikitakiwa kutunza mazingira na kulinda uoto wa asili.

Akifungua kampeni hiyo endelevu Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Senyi Ngaga, aliwaagiza TFS wilayani humo kuotesha miche ya matunda pamoja na maua na kuigawa bure kwa wananchi ili waipande katika makazi yao.

Ngaga alisema wameanza kazi hiyo baada ya Makamu wa Rais, Dk. Philipo Mpango, kuagiza mikoa yote ili kuweka mazingira ya nchi kuwa ya kijani.

"Tumefungua zoezi hili rasmi sasa hii ni kufuatia agizo la viongozi wetu wa juu na sisi Wilaya ya Sengerema tunatarajia kupanda miti zaidi ya milioni 1.5 kuelekea mwaka 2023, niwatake TFS kuendelea kuotesha miche ya kutosha ili kufanikisha kazi hii na kuiweka Sengerema yetu kuwa ya kijani," alisema Ngaga.

Meneja Uhifadhi wa TFS, Wilaya ya Sengerema, James Aloyce, alisema hali ya uoto na uhifadhi wa misitu katika halmashauri hiyo hairidhishi na kuwataka wananchi kushiriki katika upandaji miti ili kurejesha mazingira vizuri.

Alisema TFS wamejipanga kuhakikisha wanarejesha hali ya ukijani wilayani humo hususani katika Halmashauri ya Sengerema pamoja na kukumbwa na ukame.

"Niwaombe wananchi hususani wafugaji katika wilaya hii kuchunga sana mifugo yao na kuhakikisha haiharibu miche hiyo iliyoanza kupandwa, vilevile niwatake mwananchi mmoja mmoja au vikundi kufika katika kitalu chetu kuchukua miche tuliyonayo na kwenda kupanda katika maeneo yao lengo ni kurejesha Sengerema ya kijani," alisema Aloyce. Mkuu wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA), wilayani Sengerema mkoani Mwanza, Yela Malando, aliahidi kuitunza miche hiyo 1,800 iliyopandwa katika eneo la chuo hicho.

Aliwaomba watu binafsi na vikundi mbalimbali kuweka mkazo ili kuhakikisha wanafikisha huduma ya misitu katika maeneo mbalimbali hususan yenye uhitaji.

# Ukosefu chakula shuleni kikwazo cha ufaulu

**Na Neema Sawaka,** SHINYANGA

UKOSEFU wa chakula shuleni pamoja na umbali mrefu wa zaidi ya kilomita nane hadi 19 kwenda na kurudi shuleni ni moja ya chanzo cha utoro wa wanafunzi kuhudhuria masomo yao na kusababisha matokeo mabaya ya ufaulu.

Ofisa Elimu Kata ya Didia, Justus Bilago, aliyasema hayo juzi Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga alipozungumza na Nipashe.

Mahojiano hayo ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa sauti za kaya na vyombo vya habari katika kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto unaotekelezwa na klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Shinyanga (SPC), kupitia Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT), Halmashauri ya Shinyanga Vijijini.

Bilago alisema kata hiyo ina jumla ya wanafunzi 4,158 na kati ya hao wasichana 2,137 ambao wameathiriwa na utoro zaidi kuliko wavulana.

Alisema wasichana wanafanyiwa ukatili wa kijinsia kwa kurubuniwa kwa zawadi ndogo na wanaume ambao huwashawishi kujiingiza kwenye vitendo vya ngono wakiwa katika umri mdogo.

Bilago alisema tatizo lililoko kwa wazazi ni kudhani kuwa chakula kinachochangwa shuleni kwa ajili ya wanafunzi hutumika pia kuwanufaisha walimu.

Alisema suala hilo halina ukweli na kuwataka wazazi kuwa na mwitikio wa kuwachangia watoto wao chakula cha mchana kwa kuwa kukaa zaidi ya saa nane bila kupata chakula kunaathiri uwezo wa kufikiri kwa wanafunzi hao.

"Kuna uhusiano mkubwa kati ya kula chakula na kufaulu vizuri kitaaluma kwa kuwa ili mtu aweze kuelewa anachofundishwa ni lazima awe ameshiba," alisema.

Mmoja wa wanafunzi wa Shule ya Msingi Didia, Lucy Deus, alisema anapopata chakula cha mchana anakuwa na uwezo na nguvu ya kumsikiliza mwalimu anachokifundisha na kumwelewa.

Mwanafunzi, Rehema Mayenga, alisema alipokuwa anasoma masomo ya awali ya chekechea alikuwa anakunywa uji na alikuwa vizuri tofauti na sasa anapotembea umbali mrefu na kushinda na njaa tangu anapoingia darasani mpaka anapotoka jioni.

Mtendaji wa Kata ya Didia, Jackson Maganga, alisema wanajitahidi kuhamasisha wazazi wachangie chakula hicho kama njia pekee itakayowaepusha wanafunzi dhidi ya ukatili wa kijinsia.

# Wanawake wafundwa kupaza sauti ukatili kijinsia

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WANAWAKE nchini wametakiwa kupaza sauti kupinga vitendo vya ukandamizaji na manyanyaso ili kupata suluhisho litakaloleta amani na maendeleo katika jamii.

Wanawake wengi nchini wanavumilia maumivu wanapofanyiwa vitendo vya unyanyasaji ndani na nje ya familia zao na hivyo kuvipa nafasi kuendelea kushamiri katika jamii.

Akizungumza na gazeti hili, Ofisa wa idara ya wasichana na wanawake wadogo kutoka shirika lisilo la kiserikali la Amani Girls Home, Eminaely Tibesigwa juzi, alisema ili kudhibiti vitendo hivyo umefika wakati wa wanawake kupaza sauti.

Alisema ukatili unapofanyika hauna madhara kwa mtu mmoja pekee bali ni familia na jamii nzima inayodhurika na kusababisha kupotea amani katika familia pamoja na kurudisha nyuma maendeleo.

"Unaponyamaza manyanyaso na ukandamizaji utaendelea hivyo njia ya pekee ni kusimamia na kutoa sauti hiyo itatengeneza suluhisho na kuondoa vitendo hivyo, sisi tunatoa elimu ya kupinga ukatili, tunatoa elimu kwa wasichana na wanawake," alieleza.

Alisema kutokana na hali ilivyo kwa sasa ulimwengu utegemee kuzalisha kizazi ambacho kitashindwa kujitegemea na kufikia malengo kwa sababu ya ukatili uliopo ndani ya familia.

Alieleza hali hiyo ikiendelea jamii itatengeneza kizazi chenye ukatili na mtoto anapokuwa mdogo akiona vitendo hivyo na yeye atavifanya akiwa mkubwa.

"Kinamama wengi wanapopitia changamoto za kunyimwa haki na kufanyiwa mambo mbalimbali ikiwamo ukatili wanaogopa kueleza, kisa wanaogopa kuchekwa ama kuona kuwa wanajidhalilisha," alisema.

# Poland kuweka mfumo ulinzi wa angani Patriot

**WARSAW, Poland**

POLAND inajiandaa kuuweka mfumo wa ulinzi wa angani uliotengenezwa Ujerumani unaojulikana kama Patriot kwenye ardhi yake.

Hatua hiyo inatokana na Ujerumani kukataa kuuweka mtambo huo nchini Ukraine.

Waziri wa Ulinzi wa Poland, Mariusz Blascczak, alisema uamuzi huo umefikiwa baada ya kuzungumza na Wizara ya Ulinzi ya Ujerumani.

Aliesema kuiweka mifumo hiyo ya Patriot kwenye upande wa magharibi mwa Ukraine kutaimarisha usalama wa Wapoland na Waukraine.

Kwa hiyo wameanza mipango ya kuiweka mifumo hiyo ya makombora nchini Poland na kuiunganisha na mifumo ya kamandi ya nchi hiyo.

Ujerumani mwezi uliopita iliipa Poland mfumo wa Patriot ili kuisaidia kuilinda anga yake baada ya kombora kuanguka na kuwaua watu wawili nchini humo.

Waziri wa Ulinzi wa Poland baadaye aliitaka Ujerumani kupeleka mifumo hiyo nchini Ukraine hatua ambayo ilipingwa.

***DW***



Wafanyakazi wakisafisha dampo la taka eneo la Lujan, ambalo ni eneo kubwa la kutupia taka nchini Argentina. Serikali inaligeuza kuwa kituo cha mazingira na kukomesha uchafuzi wa mazingira. **PICHA: AFP**

# Washukiwa 25 wakamatwa Ujerumani

**BERLIN, Ujerumani**

JESHI la Polisi nchini Ujerumani wamefanya msako mkali nchini kote na kuwakamata watu 25 washukiwa wa siasa kali za mrengo wa kulia wanaodaiwa kupanga njama ya kuipindua serikali kwa kutumia silaha.

Waendesha mashtaka wa serikali walisema karibu maofisa 3,000 walifanya misako hiyo ya kile kinachofahamika kama vuguvugu la Reich Citizens. Baadhi ya wanachama wa kundi hilo wanapinga katiba ya Ujerumani iliyoandikwa baada ya vita kuu ya dunia na wametoa mwito wa kuangushwa kwa serikali.

Waendesha mashtaka walisema raia 22 wa Ujerumani wamekamatwa kwa kushukiwa kuwa wanachama wa kundi hilo la kigaidi.

Watu wengine watatu, akiwamo raia wa Urusi, wanatuhumiwa kuliunga mkono kundi hilo.

Jarida la kila wiki la Der Spiegel liliripoti kuwa maeneo yaliyofanyiwa msako yanajumuisha kambi ya kitengo maalum cha vikosi vya Ujerumani KSK katika mji wa kusini magharibi wa Calw.

KSK katika siku za nyuma ilituhumiwa kwa madai kuwa baadhi ya wanajeshi wake wanajihusisha na siasa kali za mrengo wa kulia.

***DW***

## Rais Xi kuanza ziara ya siku tatu Saudi Arabia

**RIADH, Saudi Arabia**

Katika ziara hiyo iliyoanza jana, Rais Xi wa China anapanga kukutana na viongozi wa nchi hiyo ya Ghuba na wa ulimwengu wa kiarabu.

Ziara hiyo inayoanza inatarajiwa kujumuisha mikutano kuanzia inayoanzia leo kwa kukutana na Mfalme Salman, Mrithi wa Kiti cha Ufalme Mohammed, pamoja na mkutano wa kilele na viongozi wa Ghuba na Uarabuni. Ziara ya Xi inajiri karibu miezi mitano baada ya Rais wa Marekani, Joe Biden kuitembelea nchi hiyo na kuwaambia viongozi wa Kiarabu kuwa Marekani haitaondoka na kuwacha ombwe la kujazwa na China, Urusi au Iran.

Nchi za Ghuba zimeimarisha mahusiano yao ya kiuchumi, kisiasa na usalama na China kwa miaka mingi.

China ni mshirika muhimu wa kibiashara wa Saudi Arabia na mteja wake mkubwa wa mafuta ghafi.

***DW***

## M23 wakubali kuondoka

**GOMA, DRC**

MAKABILIANO ya silaha yalizuka mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo juzi kati ya wanajeshi wa serikali na kundi la M23.

Hata hivyo, waasi hao walisema wako tayari kujiondoa katika maeneo wanayoyadhibiti.

Askari wa DRC walilikabili kundi hilo nje ya mji wa Bwiza, karibu kilomita 40 kaskazini mwa Goma ambao ni mji mkuu wa mkoa wa Goma.

Duru zinasema makabiliano hayo yalisababisha wakazi wa eneo hilo kukimbia na shughuli katika mji jirani wa Kitchanga kusitishwa.

Machafuko hayo yanajiri wiki moja baada ya shambulizi lililodaiwa kufanywa na M23 mashariki mwa mkoa wa Kivu Kaskazini kuwaua watu 300, karibu wote wakiwa ni raia.

Waasi hao wametoa taarifa wakisema wako tayari kujiondoa, ikiwa ni sharti muhimu lililowekwa na Angola kwenye mazungumzo ya amani mwezi uliopita pamoja na nchi jirani Rwanda litatekelezwa.

***DW***

# Kiongozi wa zamani Iran aunga mkono maandamano

**TEH RAN, Iran**

RAIS wa zamani wa Iran ametoa maoni yake akiwasifu waandamanaji wanaoipinga serikali na kuwataka wenye mamlaka kuzingatia matakwa yao kabla hawajachelewa.

Mohammad Khatami, mwenye umri wa miaka 79, alisema katika kauli zake za nadra kwamba kauli mbiu nzuri ya mwanamke, maisha, uhuru inaonyesha jamii ya Iran inaelekea kwenye mustakabali bora.

Pia alikosoa kukamatwa kwa wanafunzi katika msako wa vikosi vya usalama.

Maoni hayo yalikuja katika taarifa ya kuadhimisha Siku ya Wanafunzi iliyofanyika jana.

Wanafunzi wamekuwa mstari wa mbele katika machafuko yaliyoanza katikati ya mwezi wa Septemba kufuatia kifo cha Mahsa Amini, mwanamke mwenye umri wa miaka 22 ambaye alizuiliwa na polisi wa maadili kwa madai ya kukiuka sheria ya vazi la hijabu.

Maandamano hayo yanayoongozwa na wanawake yameenea katika miji zaidi ya 150 na vyuo vikuu 140 katika majimbo yote 31 ya nchi hiyo na yanaonekana kuwa moja ya changamoto kubwa zaidi kwa Jamhuri ya Kiislamu tangu mapinduzi ya 1979.

Uongozi wa Iran, akiwamo Rais mwenye misimamo mikali Ebrahim Raisi, umezitaja kuwa ni machafuko yanayochochewa na maadui wa kigeni wa nchi hiyo na kuviamuru vikosi vya usalama kukabiliana nao kwa uthabiti.

Kufikia sasa, waandamanaji wasiopungua 473 wameuawa na 18,215 wamezuiliwa, wakiwamo wanafunzi 586, kulingana na Shirika la Habari la Wanaharakati wa Haki za Kibinadamu (HRANA)

***BBC.***

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**MAGRETH C. NDEMBUKE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2178-0043** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **GOLDEN RIDGE SECONDARY SCHOOL** mwaka 2018. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DSM/PHQ/RB/472004/2022**

## KUPOTEA KWA VYETI



**JAPHET JOHN MASASI** anatangaza kupotea kwa vyeti vya taaluma: cheti cha chuo chenye usajili namba **299/DPS/T/2014** kilichotolewa na RUAHA **CATHOLIC UNIVERSITY** mwaka 2017 na TRANSCRIPT yenye usajili namba 299/DPS/T/2014 iliyotolewa na **RUAHA CATHOLIC UNIVERSITY** mwaka 2017. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/KIM/RB/470649/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JAPHET JOHN MASASI** anatangaza kupotea kwa **ENROLLMENT CERTIFICATE** yenye namba **0401816** iliyotolewa na **PHARMACY COUNCIL mwaka 2018.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA: DAR/KIM/RB/470649/2022**

## KUPOTEA KWA VYETI



**JAPHET JOHN MASASI** anatangaza kupotea kwa vyeti vya taaluma : cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0427-0200** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MAKAMBAKO SECONDARY SCHOOL** mwaka 2011 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0757-0530 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KYELA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2014. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/KIM/RB/470649/2022**

---

**FORM NO. 58**
**IN THE COURT OF DISTRIC T DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 134 OF 2022**

**In Matter of the Estate of the Late FAUSTIN WILLIAM MASHAURI**

**By 1. SOPHIA FAUSTIN MASHAURI**
**2. ..................................**

All Persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or latter of administration) is made to the above - named petitioner.
Objection to the grand should be field on or before the **28TH** day of **December / 2022.**
Dated at **Morogoro**, this **1st** day of **DECEMBER 2022**

RESIDENT MAGISTRATE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya BUKOBA**

**Kituo cha KARABAGAINE Mkoa wa KAGERA**

**Shauri la Madai No. 17/2021**

**Jina la mdai CHARLES BONIPHACE**

**Jina la Mdaiwa MUGISHA LEONARD**

**KUITWA SHAURINI KWA MDENI MHUKUMIWA**

**Kwa: MUGISHA LEONARD**

KWAMBA Mdai ameleta maombi mbele ya Mahakama hii kwa ajili ya utekelezaji wa hukumu ya shauri tajwa hapo juu. Unatakiwa kufika mbele ya Mahakama hii tarehe 20 Mwezi Desemba Mwaka 2022 ili kueleza kwa nini hukumu isitekelezwe dhidi yako. Kama hautahudhuria siku hiyo mahamaka inaweza kusikiliza maombi haya bila wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 30 Mwezi Novemba Mwaka 2022.

........................
**HAKIMU MFAWIDHI**
**MAHAKAMA YA MWANZO KARABAGAINE**
**BUKOBA**

---

## TANGAZO LA NOTISI - WADAIWA SUGU

**TUJIJENGE TANZANIA FINANCIAL SERVICE LIMITED,** Inatangaza notisi ya siku Sitini (60) Kuanzia tarehe ya Tangazo hili. Hatua zaidi za Kisheria zitachukuliwa kwa wadaiwa watakaoshindwa kulipa madeni yao ndani ya muda ulioainishwa( siku sitini).Ikiwa ni pamoja na kuwaruhusu madalali kuuza mali zao ambazo zimetumika kama dhamana za mikopo yao.

Wadiwa Sugu ni: -

1. Marco Esrom Mrikaria/Waven Esrom Mrikaria -Mwanza
2. Upendo Emmanuel Sarakikya - Mwanza
3. Mohamed Rashird Fokolo - Mwanza
4. Mashaka Juma Maige - Mwanza
5. Prisca Revocatus Mgeta - Mwanza
6. Hawa Hussein Kichwabuta - Mwanza
7. Simon Mpandula Ngalaba - Mwanza
8. Sadiki Kalokola Joseph - Mwanza
9. Khadija Beaty Mtengule - Mwanza

**Mawasiliano piga: +255 222774742-3/0677001063**
**Au Email: tujijengetanzania@tujijenge.or.tz**

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGFO YA TEMEKE**

**(TEMEKE KITUO CHA JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**

**MIRATHI NA 253 YA MWAKA 2022**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**HUMPHREY ELILEKIA MROSO**
**GETRUDE HUMPHREY MROSO............................MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(KANUNI YA 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 8 mwezi wa machi, 2023 saa 6:00 mchana siku ambayo shauri hili limepangwa kusikilizwa mbele ya Mhe. Jaji Asina Omari.
Imesainiwa Dar es salaam, leo tarehe 5 mwezi wa Disemba, 2022.

**NAIBU MSAJILI**

---

**FORM 58**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**

**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 1130 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late DENIS AMON JOHN**

**and**

**In the Matter of Application for Letters of Administration by DAVID DENIS AMON**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the **23RD day of DECEMBER, 2022**

Dated at DAR ES SALAAM this **06 day of DECEMBER, 2022.**

Senior Resident Magistrate

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**

**MAOMBI NAMBA 159 YA 2019**

**DENIS MATHEW MSANZYA..............MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**ELLY NASIFU CHUMA ................MJIBU MAOMBI**

**WITO WA KUITWA SHAURINI KWA**

**ELLY NASIFU CHUMA** Popote ulipo unaarifiwa ufike katika baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Morogoro tarehe 19/12/2022 mbele ya Mwenyekiti M.Khasim wewe mwenyewe binafsi au utume mwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutelewa uamuzi
Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 01 mwezi Desemba 2022.

M. KHASIM
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MOROGORO.

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO 131 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late:THOBIAS MICHORO MAKARANGA**

**BY 1.TABU MBOYI MASAIGANA**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 15TH DECEMBER.........2022

Dated at MOROGO this 29ST day of NOVEMBER.........2022

RESIDENT MAGISTRATE

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO....18....OF 2022**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE ABRAHAM SHEMNGA SHECHAMBO**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETER OF ADMINISTRATION**

**BY PAULO ABRAHAM SHECHAMBO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

ALL PERSON claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be field on or before the 05 day of JANUARY 2023

Dated at Korogwe this 06 day of DECEMBER 2022

DISTRICT COURT
KOROGWE

---

## TANGAZO LA NOTISI - WADAIWA SUGU

**TUJIJENGE TANZANIA FINANCIAL SERVICE LIMITED,** Inatangaza notisi ya siku Kumi na nne (14) Kuanzia tarehe ya Tangazo hili. Hatua zaidi za Kisheria zitachukuliwa kwa wadaiwa watakaoshindwa kulipa madeni yao ndani ya muda ulioainishwa( siku kumi na nne).Ikiwa ni pamoja na kuwaruhusu madalali kuuza mali zao ambazo zimetumika kama dhamana za mikopo yao.

**Wadiwa Sugu ni: -**

1. Respiscus Makoye Mayala - Mwanza
2. Penina Methusela Mgema - Mwanza
3. Marietha Mchele - Mwanza
4. Rosemary Ignatio Kailembo - Mwanza
5. Jackline Salehe Ramadhani - Mwanza
6. Rehema Jacob Kigwila - Mwanza
7. Leticiacrala Saimon Nyembe - Mwanza
8. Farida Majani Lweyemamu - Mwanza
9. Joseph James Bubele - Mwanza
10. Thomas Murimi Waise - Mwanza
11. Salmah Ismaily Mkama - Mwanza


**Mawasiliano piga: +255 222774742-3/0677001063**
**Au Email: tujijengetanzania@tujijenge.or.tz**

---

**OFISI ZA MATANGAZO,**
**MIKOCHENI**
**INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0782253676**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa**
**Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# DIMPOZ

## NIMEIBIWA MILIONI 30/-

MSANII wa Bongo Fleva, Ommy Dimpoz, amesema kuna watu wamempora mamilioni ya fedha bila kujali yupo katika kipindi cha maombolezo.

Dimpoz alitangaza kufiwa na mpenzi wake, mrembo, Maya Mia, ambaye aliwahi kuchumbiwa na mwigizaji maarufu, Idris Sultan.


Alisema baada ya kuibiwa, aliamua kutochukua hatua zozote za kisheria na kumwachia Mungu kwa sababu kipindi hiki hana nguvu ya kuanza kufuata taratibu za kuwashtaki waliomwibia.

"Yaani hata sijapoa na msiba, juzi nimeibiwa Dola 13,000, karibu milioni 30 za Kitanzania, lakini nimeamua kumshtakia Allah," aliandika Ommy kwenye Instagram yake.

Tangu alipotangaza kufiwa na mpenzi wake wa muda mrefu, amekuwa akipakua picha na video walivyokuwa wakila bata na mpenzi wake sehemu mbalimbali zenye hadhi ya nyota tano.

Taarifa ambazo sio rasmi zilidai Mia alijipiga risasi na kufariki dunia na Ommy ndiye alikuwa mtu wa kwanza kutoa taarifa hiyo.

## KANYE AMPA NENO MAMA WATOTO WAKE



RAP Kanye West kupitia mahojiano yake mapya na Infowars aliyoyafanya wiki iliyopita, amwomba mama wa watoto wake, Kim Kardashian, kumrudia Mungu.

Kanye amemtahadharisha Kim, kampuni anazofanya nazo kazi hazimpendi na asiruhusu shetani amtumie.

Pia, Kanye amemtaka Kim kufunga ndoa na mpenzi wake wa sasa, Tom Brady ambaye ni mcheza mpira wa Baseball nchini Marekani na atumie umaarufu na ushawishi alionao kuziunganisha familia pamoja.

Itakumbukwa, Kanye ametoa maneno hayo kwa Kim ikiwa ni siku chache tangu kukamilika kwa mchakato wao wa talaka na kuachana rasmi.

## BEN POL AMSHANGAA JUX



NYOTA wa Bongo Fleva, Ben Pol ametoa povu kuhusu kitendo cha msanii mwenzie, Jux kuchapisha mabango mtandaoni kuwa atahudhuria uzinduzi wa albamu yake ya 'King of Hearts'.

Jana, Jux alitarajiwa kuzindua albamu yake huku wasanii kadhaa wakubwa wakitajwa kuhudhuria.

Tofauti na wasanii wengine, Ben Pol alionesha kutofikia makubaliano ya kuhudhuria onyesho hilo.

"Una namba yangu umeshindwa kunipigia au kunitumia ujumbe? Au watu wako kuwasiliana na watu wangu? Tunakuja kuona kwenye mitandao nitakuwapo kwenye show yako.

"Wewe ulikasirika kwa Harmonize kukuweka kwenye matangazo ya 'event' yake bila kukutaarifu au kukualika ukafanya hadi interviews, lakini wewe unafanya kitu kile kile.

"Napenda sapoti lakini hii ni staili gani kaka," aliandika Ben Pol kwenye ukurasa wake wa mtandao wake wa Instagram.

# CHANZO MKWASA KUONDOKA RUVU SHOOTING CHAJULIKANA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya Ruvu Shooting kumtangaza, Mbwana Makata ndiye mrithi wa Charles Mkwasa, ambaye aliamua kujiuzulu, kocha huyo mkongwe amesema amechukua uamuzi 'mzito' kwa ajili ya kulinda heshima yake na si kusubiri kutimuliwa, imefahamika.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Mkwasa, alisema haiwezekani awe anafundisha timu ambayo haipati matokeo na kwa sababu yeye ni mtu anayejiheshimu, aliamua kuchukua uamuzi huo wa kupisha klabu itafute kocha mpya atakayesaidia kuipa matokeo mazuri.

Mkwasa alisema ameona akae pembeni huenda mafundisho yake hayapokelewi vyema na wachezaji na yeye anatamani kuona hali hiyo inaondoka.

"Huu ni uamuzi wangu, na hii si mara ya kwanza, zamani nilikuwa nacheza kwenye Timu ya Taifa (Taifa Stars), ilifika miaka mitatu timu haipati ushindi, nikaona kwa nini niendelee kuwa 'kepteni' timu haifanyi vizuri, nikajiuzulu, hata kuna wakati nilipokuwa kocha wa timu ya wanawake (Twiga Stars) niliwahi kujiuzulu," alisema Mkwasa.

Kocha huyo alisema Ruvu Shooting ilikuwa inacheza vizuri, lakini tatizo ni kupata ushindi, kitu ambacho kwa kiasi kikubwa ndicho kilichomfanya kukaa pembeni.

"Tukicheza utaona tunacheza vizuri, lakini hakuna timu inayopata pointi au ubingwa kwa kucheza vizuri, ni kushinda tu, wachezaji wanakosa penalti, mara wanajifunga wenyewe, ila nashukuru nimeondoka Ruvu Shooting nikiwa nimejenga mahusiano, nashukuru sana," alisema Mkwasa.

Nyota huyo wa zamani wa Yanga ameondoka Ruvu Shooting akiiacha ikiwa katika nafasi ya 15, ikimaliza mechi zake za mzunguko wa kwanza ikiwa na pointi 11 baada ya kupoteza michezo 10, ikishinda mechi tatu na kupata sare mbili.



Mshambuliaji wa Simba Queens, Asha Djafari (kushoto), akijipanga kuwatoka mabeki wa JKT Queens katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mo Arena ulioko Bunju, Dar es Salaam juzi. Simba Queens ilifungwa mabao 2-1. **PICHA: SIMBA SC**

# Mastraika Simba Queens tatizo

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukula, amesema amekerwa na ubutu wa safu ya ushambuliaji ya timu yake pamoja na kukosa umakini wa kutumia nafasi za kufunga wanazopata.

Kauli ya kocha hiyo imetolewa baada ya timu yake kuanza msimu mpya vibaya kwa kukubali kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa JKT Queens katika mechi ya ufunguzi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mo Arena, Dar es Salaam juzi.

Lukula alisema pia hajafurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wake ambao hivi karibuni walikuwa katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa wanawake.

"Nina kazi ya kufanya hasa katika safu ya ushambuliaji ambayo haikuwa makini, tumetengeneza nafasi nyingi na tumepata penalti tumeshindwa kutumia, hatuna cha kufanya kama tumekosa.

Nimesikitishwa sana na mtazamo wa wachezaji kwa sababu tungepata angalau pointi, sina maneno mazuri kwa wachezaji wavivu, nitaenda kubadili mitazamo yao, wasipokubali nitabaki na wachezaji wachache," alisema Lukula.

Naye Kocha Mkuu wa JKT Queens, Haule Grayson, alisema amewapongeza wachezaji wake kufuata yale aliyotoa katika uwanja wa mazoezi na kuyahamishia kwenye mechi na hatimaye wameondoka na pointi tatu.

Haule alisema mchezo huo ulikuwa mgumu na aliingia uwanjani kwa kuwaheshimu Simba ambayo 'aliipeleleza' ilipokuwa ikishiriki mashindano ya kimataifa.

## Meza kuchaguana Januari mwakani

**Na Shufaa Lyimo**

UCHAGUZI Mkuu wa Chama cha Mpira wa Meza Tanzania (TTTA), umepangwa kufanyika ifikapo Januari 7, mwakani jijini Dar es Salaam.

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano cha Baraza la Michezo Tanzania (BMT), Najaha Bakari, alisema fomu kwa ajili ya wadau wanaotaka kuwania nafasi za uongozi zimeanza kutolewa jijini na mchakato huo utamalizika Januari 3, mwakani.

Najaha alitaja nafasi ambazo zitawaniwa katika uchaguzi huo ni ya Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu Mkuu, Mweka Hazina, Mweka Hazina Msaidizi, wajumbe wa Kamati ya Utendaji na Mwenyekiti wa Kamati za Kudumu za chama hicho.

"Waombaji wanatakiwa kuwa na umri wa kuanzia miaka 30, awe amewahi kuwa mchezaji wa mchezo huo kwa muda usiopungua miaka minne, vile vile mgombea anatakiwa awe na elimu isiyopungua kidato cha nne," alisema ofisa huyo.

Aliongeza usaili kwa wagombea ambao watakuwa wamerudisha fomu utafanyika ifikapo Januari 6, mwakani.

## Netiboli Daraja la 2 kumekucha

**Na Shufaa Lyimo**

MABOSI wa Chama cha Netiboli Tanzania (CHANETA), wanafurahishwa na ushindani unaoonyesha katika mechi za Ligi Daraja la Pili katika mchezo huo inayoendelea kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano ya CHANETA, Lucy Sylvester, aliliambia gazeti hili jana ushindani katika ligi hiyo ni mkubwa na wachezaji wanaoshiriki wana umri mdogo.

"Ushindani ni mkubwa, kila timu imejipanga kufanya vizuri, sasa tunaona mchezo huu unavyozidi kushika kasi," alisema Lucy.

Kiongozi huyo aliongeza timu sita zitakazofanya vizuri katika ligi hiyo zitapandishwa daraja.

"Timu 15 zilithibitisha kushiriki ila zilizokuja kushiriki ni timu saba, nyingine zimekwama kwa sababu ya ukata," Lucy alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MARTINELLI ANUKIA BARCA

BARCELONA inamfuatilia winga wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Brazil, Gabriel Martinelli, mwenye umri wa miaka 21, huku wakiangalia uwezekano wa kumsajili wakati wa dirisha la Januari. ***(Sport)***

### BELLINGHAM SASA KUUZWA

KLABU ya Borussia Dortmund itakuwa tayari kumuuza kiungo wa Timu ya Taifa ya England, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19, kipindi cha majira ya joto kinachofuata kwa dau la pauni milioni 86 hadi 129. ***(Sky Sports)***

### PSG KUIBEBA DORTMUND

RAIS wa Paris St-Germain, Nasser Al-Khelaifi amesema "kila mtu" anataka kumsajili, Jude Bellingham na klabu hiyo ya Ufaransa itawafuata Dortmund kwanza kama wanataka kumsajili. ***(Sky Sports)***

### RONALDO NJIA PANDA

FOWADI wa Timu ya Taifa ya Ureno, Cristiano Ronaldo, mwenye umri wa miaka 37, bado hajaamua kufanya uamuzi kuhusu ofa ya kujiunga na klabu ya Saudi Arabian, Al-Nassr. ***(ESPN)***

### SPURS KUMSAJILI KESSIE

KLABU ya Tottenham Hotspur ina nafasi kubwa zaidi ya kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast kwenye umri wa miaka 25, Franck Kessie kutoka Barcelona. ***(Sport)***

### MOYES MAMBO MAGUMU

DAVID Moyes anakabiliwa na uwezekano wa kufukuzwa kama kocha wa West Ham wakati uhusiano wake na mwenyekiti mwenza wa klabu hiyo, David Sullivan, ukiendelea kudorola. ***(Football Insider)***

### MADDISON, TIELEMANS KUONDOKA

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya England, James Maddison, mwenye umri wa miaka 26, na kiungo wa Ubelgiji, Youri Tielemans (25), wamehusishwa na mpango wa kuondoka Leicester City, lakini klabu hiyo inasita kuwaachia kwenye dirisha la Januari. ***(Leicestershire Live)***

### MADRID YAMTAKA ENDRICK

REAL Madrid inapanga kuipiku Chelsea kumsajili fowadi kinda wa Palmeiras, Endrick mwenye umri wa miaka 16, ambaye anaweza kujiunga nao hadi atakapofikisha miaka 18 mwaka 2024. ***(UOL Sport)***

### VERRATTI KUBAKIA PSG

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Italia, Marco Verratti, mwenye umri wa miaka 30, atasaini mkataba mpya na Paris St-Germain. ***(Fabrizio Romano)***

### VESTERGAARD MAMBO SAFI

ASTON Villa itampa ofa mlinzi wa kati wa Leicester City na Timu ya Taifa ya Denmark, Jannik Vestergaard mwenye umri wa miaka 30, wakati wa dirisha la Januari. ***(Football Insider)***

### BALOGUS KURUDI ARSENAL

KLABU ya Arsenal haijaondoa uwezekano wa kumwita straika, Folarin Balogun mwenye umri wa miaka 21 anayecheza kwa mkopo katika klabu ya Reims ya Ufaransa, baada ya kuumia kwa Gabriel Jesus (25). ***(90 Min)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BUSQUETS HAFIKIRII KUSTAAFU HISPANIA

●●● Asema kutolewa na Morocco kumewapa 'usiku mgumu' lakini lazima...

**DOHA, Qatar**

SERGIO Busquets amesema sasa si wakati wa mjadala kuhusu mustakabali wake wa kimataifa baada ya Hispania kuondolewa katika Kombe la Dunia kwa "njia ya kikatili zaidi" kwa kushindwa na Morocco kwenye hatua ya penalti.

La Roja hao walipoteza kwa penalti 3-0 kwenye Uwanja wa Education City baada ya mchezo huo wa hatua ya 16 bora kumalizika kwa suluhu kwa dakika za kawaida na zile za nyongeza hapo juzi, huku Simba wa Atlas wakifuzu hatua ya robo fainali kwa mara ya kwanza.

Nahodha wa Hispania, Busquets, Pablo Sarabia na Carlos Soler walishindwa kufunga penalti zao, huku mlinda mlango wa Morocco, Yassine Bounou, akiibuka shujaa kwa kudaka penalti mbili.

Achraf Hakimi mzaliwa wa jiji la Madrid nchini Hispania ndiye aliyefunga penalti ya ushindi kwa Morocco.

Kikosi cha Kocha, Luis Enrique, kilitawala mpira, lakini kilikosa makali, huku Sarabia akigonga nguzo mwishoni mwa muda wa fidia.

Akiwa na umri wa miaka 34, imependekezwa Busquets anaweza kustaafu kuichezea Hispania, lakini kiungo huyo wa kati wa Barcelona hataharakisha kufanya uamuzi baada ya kuondoka Doha.

Aliliambia La1: "Sasa cha muhimu ni timu na sio mimi, ni usiku mgumu na itabidi tuamke na kutumia uzoefu huu, kuna vijana ambao watatufaa sana na lazima tuendelee."

Busquets alihisi Hispania ilikuwa na bahati mbaya kukosa nafasi ya kutinga robo fainali.

"Ilikuwa aibu, iliamuliwa kwa adhabu kwa njia ya kikatili zaidi. Ilikuwa ngumu, tulijaribu kuwavaa, kuwageuza, kutafuta nafasi. Tulikosa bahati kutokana na pasi ya mwisho," alisema nyota huyo.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,056,5
MECHI KALI
MALAGA
VERSUS
GRANADA
1 | 3.22
X | 2.97
2 | 2.31
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom | m-pesa
airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# SANTOS AFICHUA SABABU KUMWEKA BENCHI RONALDO



**DOHA, Qatar**

KOCHA wa Ureno, Fernando Santos, amesema uamuzi wa kutomwanzisha, Cristiano Ronaldo katika mechi ya hatua ya 16 bora ya Kombe la Dunia dhidi ya Uswisi haukuwa wa kibinafsi.

Habari zilienea mapema Jumanne fowadi huyo wa zamani wa Manchester United angeanzia benchi baada ya kuonyeshwa kutofurahishwa na kutolewa katika mechi ya mwisho ya makundi dhidi ya Korea Kusini.

Santos alieleza hakuwa shabiki wa tabia ya Ronaldo, lakini uamuzi wa kumwacha nje mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37 na nafasi yake kumpa Goncalo Ramos asiye na uzoefu, ilikuwa ni sehemu ya kawaida tu ya mabadiliko.

Ramos mwenye umri wa miaka 21 alifunga mabao matatu 'hat-trick' kwenye mchezo huo ambao walishinda magoli 6-1 Jumanne na kuiwezesha Ureno kutinga robo fainali.

"Cristiano na Ramos ni wachezaji tofauti. Hakuna tatizo na nahodha wa timu ya taifa," alisema Santos.

"Ilikuwa ya kimkakati. Wachezaji ni tofauti. Pia nilianza na (Diogo) Dalot, Raphael (Guerreiro) na (Joao) Cancelo ni mchezaji mzuri. Hiyo ndivyo nilivyofikiria kwa mchezo dhidi ya Uswisi, na katika mchezo mwingine inaweza kuwa tofauti. "

Santos alipobanwa zaidi alitoa maelezo ya kina zaidi nyuma ya uamuzi wake, akijibu: "Je, sikujibu swali hili tayari? Hakuna tatizo kati ya Fernando Santos (yeye) na nahodha wa timu ya taifa. Tumekuwa marafiki kwa miaka mingi."

# Arsenal kumkosa Jesus miezi 3

**LONDON, England**

MATUMAINI ya Arsenal kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England yalipata pigo kubwa Jumanne baada ya kuthibitishwa mshambuliaji, Gabriel Jesus amefanyiwa upasuaji wa goti huku vyanzo vya habari vikiambia ESPN kwamba, atakuwa nje ya uwanja kwa takribani miezi mitatu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 alipata jeraha la goti la kulia wakati Brazil wakifungwa bao 1-0 na Cameroon kwenye mchezo wa mwisho wa hatua ya makundi Ijumaa iliyopita na kuhitimisha ushiriki wake katika fainali hizo nchini Qatar.

Hapo awali Jesus alibaki na kikosi cha Brazil huku kukiwa na uhakika jeraha lake sio kubwa, lakini alirejea jijini London kwa uchunguzi zaidi, ambapo iliamuliwa alihitaji kufanyiwa upasuaji.

Taarifa ya klabu ilisema: "Gabriel Jesus amefanikiwa kufanyiwa upasuaji wa goti lake la kulia baada ya kuumia wakati wa mechi ya hatua ya makundi ya Kombe la Dunia wakati Brazil ikicheza dhidi ya Cameroon siku ya Ijumaa.

"Gabby sasa ataanza programu yake ya kupona. Kila mtu katika klabu anamuunga mkono Gabby na atapambana kwa bidii kurejesha uwanjani haraka iwezekanavyo."

Habari hizi zitakuja kama kikwazo kikubwa kwa kocha, Mikel Arteta na matumaini ya Washikabunduki hao kushinda taji la Ligi Kuu.



554,107/-

# GEITA GOLD FC, MPOLE WAFIKIA MAKUBALIANO

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE straika George Mpole na mabosi wake wa Geita Gold FC, wamefikia makubaliano ya kusitisha mkataba na sasa nyota huyo yupo huru kujiunga na timu yoyote itakayomhitaji, imefahamika.

Mpole, Mfungaji Bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita, hakuwa na mahusiano mazuri na mabosi wake na kusababisha aingie kwenye mzozo wa mara kwa mara.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo jana imesema wamefikia maridhiano ya kusitisha mkataba na nyota huyo ambaye pia anaichezea Timu ya Taifa baada ya mazungumzo ya muda mrefu.

"Klabu ya soka ya Geita Gold tumefikia maridhiano ya kusitisha mkataba na aliyekuwa mchezaji wetu, George Enock Mpole, kuanzia leo Desemba 7, 2022.

Uongozi umefikia hatua hii baada ya kuzungumza na mchezaji kwa kina na kufikia maridhiano hayo kwa maslahi mapana ya klabu na mchezaji mwenyewe. Mpole sasa ni mchezaji huru," ilimaliza taarifa hiyo.

Maridhiano hayo yamekuja wakati dirisha dogo la usajili linatarajiwa kufunguliwa Desemba 15, mwaka huu, hivyo atakuwa huru kujiunga na klabu yoyote itakayomhakikisha maslahi mazuri.

Straika huyo alimpita Fiston Mayele wa Yanga kwa bao moja, akifunga magoli 17 msimu uliopita, alihusishwa na mipango ya kujiunga na Simba baada ya Mnyama kuachana na mastraika wake, Chris Mugalu na Meddie Kagere, lakini dili halikufanikiwa.

Pia Azam FC ilitajwa kuhitaji huduma ya Mpole lakini mambo hayakwenda kama ilivyotarajiwa.




## Okwa aitabiria

INATOKA UK. 32

pobainika kuna upungufu.

Lihamwike alimtaja mwanachama mmoja ambaye amejitokeza kuchukua fomu ya kuwania Ujumbe ni Abubakar Zebo na kukumbusha mchakato huo utamalizika ifikapo Desemba 19, mwaka huu.

"Wachangamke kuja kuchukua na kurejea fomu ili hapo baadaye kusiwe na malalamiko juu ya watu kuonewa maana hadi sasa kuna mtu mmoja tu (Zebo) ambaye ameomba nafasi ya ujumbe," alisema Boniface Lihamwike.

Usaili kwa ajili ya wagombea watakaokuwa wamerudisha fomu utafanyika kati ya Desemba 22 hadi 24, mwaka huu wakati muda wa kupokea mapingamizi utakuwa ni Desemba 29, mwaka huu.

Kampeni kwa wagombea watakaokuwa wamepitishwa zitamalizika rasmi Januari 28, mwaka huu na siku itakayofuata ndio utafanyika uchaguzi huo.

## YANGA YAFUNGUKA

INATOKA UK. 32

bao na kuiweka timu kwenye nafasi salama.

"Tunatakiwa kuwa vizuri kila nafasi, tumepanga kuongeza nguvu katika idara ya ushambuliaji, tutakuwa na mechi ngumu za Ligi Kuu, tunaanza mashindano ya Kombe la FA na baadaye mechi ngumu za hatua ya makundi (Kombe la Shirikisho Afrika), ni lazima tuwe imara zaidi," Kaze alisema.

"Mayele (Fiston) anahitaji kupata msaidizi, mshambuliaji ambaye hatutakuwa na presha akianza, kwa sasa Mayele akikosekana tunalazimika kubadilisha mbinu, tunahitaji kujilinda zaidi, ligi ni ngumu na kila timu imeimarika ili kusaka matokeo mazuri," aliongeza kocha huyo.

Alisema anashukuru kuona wachezaji waliokuwa majeruhi afya zao zinaimarika, lakini hii haibadilishi mawazo ya kusajili mshambuliaji mwingine ambaye atakuwa na kiwango cha juu kitakachosaidia kupata ushindi kwenye mechi ngumu.

"Mara nyingi hatupati matokeo mazuri katika kipindi cha kwanza, tunatakiwa kubadilika, iwe tunacheza nyumbani au ugenini, washambuliaji pia wanatakiwa kuongeza umakini, tunatengeneza nafasi nyingi, lakini ushindi tunaopata ni mdogo, ni hatari huko mbele," kocha huyo raia wa Burundi alisema.

Timu tatu ambazo zimemaliza mzunguko wa kwanza zikiwa zinaburuza mkia ni pamoja na Ihefu SC yenye pointi 11 sawa na Ruvu Shooting wakati Polisi Tanzania iliyotangazwa kumwajiri Mkongomani Mwinyi Zahera imejikusanyia pointi tisa kutoka kwenye mechi 15 walizocheza.


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 10/12/22 | 18:00 | Blackpool vs Birmingham | 2.68 | 3.28 | 2.58 |
| 2. 10/12/22 | 18:00 | Swansea vs Norwich City | 2.37 | 3.38 | 2.88 |
| 3. 10/12/22 | 18:00 | Lincoln vs Wycombe | 2.83 | 3.28 | 2.46 |
| 4. 10/12/22 | 18:00 | Bristol Rovers vs Port Vale | 2.52 | 3.32 | 2.72 |
| 5. 10/12/22 | 18:00 | Oxford Utd vs Barnsley | 2.34 | 3.29 | 2.99 |
| 6. 10/12/22 | 18:00 | Grimsby vs Tranmere | 2.26 | 3.19 | 3.24 |
| 7. 10/12/22 | 18:00 | Salford City vs Walsall | 2.42 | 3.20 | 2.95 |
| 8. 10/12/22 | 21:00 | Villarreal B vs Tenerife | 2.74 | 2.83 | 2.88 |
| 9. 10/12/22 | 22:00 | England vs France | 3.04 | 3.24 | 2.43 |
| 10. 11/12/22 | 16:00 | Genclerbirligi vs Erzurum BB | 2.53 | 3.48 | 2.58 |
| 11. 11/12/22 | 16:00 | Gillingham vs Bradford City | 3.24 | 3.14 | 2.28 |
| 12. 11/12/22 | 16:00 | QPR vs Burnley | 3.08 | 3.33 | 2.27 |
| 13. 11/12/22 | 16:30 | Calcio Lecco vs Padova | 2.31 | 3.06 | 3.16 |
| 14. 11/12/22 | 16:30 | Feralpisalo vs Novara | 2.26 | 3.05 | 3.40 |
| 15. 11/12/22 | 16:30 | Roda Kerkrade vs Heracles | 2.59 | 3.43 | 2.59 |
| 16. 11/12/22 | 16:30 | De Graafschap vs FC Eindhoven | 2.41 | 3.43 | 2.79 |
| 17. 11/12/22 | 16:30 | Mantova vs Pro Vercelli | 2.60 | 3.05 | 2.90 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 08/12/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1199 | CD Rota vs Coria CF | 3.16 | 2.87 | 2.30 |
| 14:00 | 1952 | Atletico Baleares vs SD Logrones | 1.88 | 3.21 | 3.90 |
| 14:00 | 3219 | FC Malaga City vs CD Huetor Vega | 3.26 | 3.07 | 2.14 |
| 14:00 | 4934 | Tiddim Road Athlectic Club vs Minerva FC | 3.11 | 3.31 | 2.10 |
| 14:00 | 5124 | UD Almeria B vs Motril | 1.65 | 3.70 | 4.48 |
| 14:00 | 5393 | Conil CF vs Cordoba B | 3.44 | 3.05 | 2.07 |
| 14:15 | 1951 | Silva SD vs CSD Arzua | 2.06 | 3.11 | 3.40 |
| 14:15 | 3961 | Bali Utd Pusam vs Bhayangkara Surabaya Utd | 1.96 | 3.21 | 3.59 |
| 14:30 | 3179 | Parma vs Benevento | 1.88 | 3.42 | 3.92 |
| 15:30 | 4241 | Sur vs AL Etihad | 2.11 | 2.87 | 3.60 |
| 15:45 | 1423 | Smouha Club vs Aswan | 2.45 | 2.88 | 3.13 |
| 15:45 | 2295 | Enppi Club vs Haras EL Hodood | 1.98 | 3.03 | 4.17 |
| 16:00 | 1000 | Fgura United vs Vittoriosa Stars | 1.38 | 4.90 | 7.20 |
| 16:00 | 2165 | Attard FC vs St Andrews | 3.10 | 3.45 | 2.17 |
| 16:00 | 4706 | Burgos vs Eibar | 3.02 | 2.83 | 2.53 |
| 16:00 | 5062 | Ethiopia Bunna SC vs Hadiya Hosahina FC | 3.25 | 3.01 | 2.17 |
| 17:00 | 1830 | Cittadella vs Bari | 2.41 | 2.96 | 3.06 |
| 17:00 | 2020 | ATK Mohun Bagan vs Jamshedpur | 1.78 | 3.55 | 3.89 |
| 17:00 | 2372 | Genoa vs Sudtirol | 1.52 | 3.91 | 5.94 |
| 17:00 | 2554 | Modena vs Venezia | 2.30 | 3.12 | 3.07 |
| 17:00 | 2966 | Ararat Yerevan vs Bkma Yerevan | 1.71 | 3.50 | 5.00 |
| 17:00 | 3413 | Perugia vs Spal | 2.01 | 3.22 | 3.67 |
| 17:00 | 5544 | Reggina vs Frosinone | 2.46 | 3.02 | 2.92 |
| 17:00 | 5753 | Cosenza vs Brescia | 3.28 | 3.08 | 2.22 |
| 17:30 | 3453 | Manama Club vs Bahrain Club | 1.63 | 3.49 | 5.04 |
| 18:00 | 1253 | Cornella vs Real Murcia | 3.75 | 2.92 | 2.04 |
| 18:00 | 4093 | Coca Cola vs El Ittihad Alexandria | 1.88 | 3.18 | 4.38 |
| 18:15 | 5412 | Lugo vs Sporting Gijon | 3.18 | 2.93 | 2.36 |
| 18:30 | 3148 | Lija Athletic vs San Gwann FC | 2.40 | 3.55 | 2.70 |
| 18:30 | 3582 | Naxxar Lions vs Melita FC | 1.73 | 3.75 | 4.40 |
| 19:00 | 5497 | CD Choco vs Arosa SC | 4.67 | 3.60 | 1.64 |
| 19:30 | 1757 | Olimpija Ljubljana vs NK Mura | 1.85 | 3.70 | 3.46 |
| 19:30 | 5952 | CD Feirense vs Santa Clara | 2.87 | 3.01 | 2.38 |
| 20:00 | 2488 | Pisa vs Ascoli | 2.10 | 3.17 | 3.47 |
| 20:00 | 4403 | Ceramica Cleopatra vs Ismaily SC | 2.30 | 2.87 | 3.42 |
| 20:00 | 5893 | Alcoyano vs Athletic Bilbao B | 1.90 | 3.26 | 3.75 |
| 20:30 | 1743 | Levante vs Ponferradina | 1.47 | 4.16 | 6.34 |
| 20:30 | 3732 | UD Ibiza Eivissa vs Racing Santander | 2.41 | 2.87 | 3.17 |
| 20:30 | 4188 | Nazareth Ilit vs Bnei Yehuda | 3.60 | 3.20 | 2.09 |
| 21:00 | 1268 | Botosani vs Steaua Bucuresti | 2.78 | 3.12 | 2.38 |
| 21:00 | 1578 | CS Mioveni vs UTA Arad | 3.11 | 2.97 | 2.27 |
| 21:00 | 2698 | FC Otelul Galati vs Gloria Buzau | 2.34 | 3.15 | 2.81 |
| 21:00 | 4622 | ASEC Mimosas vs LYS Sassandra | 1.66 | 3.20 | 5.43 |
| 22:00 | 4545 | GD Chaves vs Porto | 7.17 | 4.68 | 1.39 |
| 22:00 | 5983 | CA Osasuna B vs Gimnastic Tarragona | 1.98 | 3.11 | 3.65 |
| 22:15 | 2914 | Gillingham vs Dagenham and Redbridge | 2.37 | 3.20 | 2.86 |
| 22:30 | 3986 | Palermo vs Como | 2.13 | 3.22 | 3.32 |
| 22:45 | 5575 | Falkirk FC vs Dundee FC | 3.86 | 3.56 | 1.79 |
| 23:00 | 1593 | Malaga vs Granada | 3.22 | 2.97 | 2.31 |
| 23:00 | 4031 | Real Madrid W vs Chelsea W | 3.79 | 3.50 | 1.82 |

18+ CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Alhamisi Desemba 8, 2022

Nipashe



UKURASA 29

## Busquets hafikirii kustaafu Hispania

MOROCCO HIYOOO....



Mashabiki wa soka wa Jiji la Rabat, Morocco waliojitokeza barabarani kushangilia ushindi wa timu yao ya taifa dhidi ya Hispania katika mechi ya Kombe la Dunia iliyochezwa nchini Qatar, juzi usiku. Morocco sasa itacheza robo fainali dhidi ya Ureno hapo keshokutwa. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA YAFUNGUKA HAITABWETEKA

## ●●●Kaze akiri haikuwa kazi rahisi kwa mabingwa hao watetezi kumaliza...

**Na Saada Akida**

VINARA na mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, wamesema walikutana na changamoto mbalimbali katika kila mechi ya ligi hiyo waliyocheza na wanaamini ushindani utaongezeka zaidi kwenye mzunguko wa lala salama.

Yanga ilikamilisha mzunguko wa kwanza ugenini mkoani Lindi kwa kuwavaa, Namungo, lakini ilikuwa kileleni kabla ya kushuka dimbani, ikijikusanyia pointi 35 sawa na Azam FC wakati Simba yenye 34 ikifuatia.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaze, alisema kikosi chao kilicheza kwa nguvu katika kila mechi na waliwaandaa wachezaji wao kutokata tamaa hadi watakaposikia filimbi ya mwisho.

Kaze alisema wanafahamu kila mchezo kwao ni sawa na fainali, hivyo hawataki kuona wanapoteza pointi kwa sababu wanahitaji kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambao wanaushikilia.

Kocha huyo alisema licha ya kucheza katika mazingira magumu, wachezaji wao walikuwa wanapambana kuhakikisha wanaendelea kuipa heshima timu kwa kushinda kila mechi au kugawana pointi na wapinzani.

"Tumepambana katika kila mechi tuliyocheza, tumefika hapa kwa sababu hatutudharau wapinzani, kila timu tuliipa heshima yake lakini tulisema hatutaki kupoteza pointi, tunashukuru tumemaliza mzunguko wa kwanza tukiwa juu.

Ni wazi mzunguko wa pili utakuwa mgumu pia, hapo kila mmoja atahitaji kuona anafikia malengo au anataka kujiondoa katika hatari ya kushuka daraja, ni wakati mgumu kuliko huu tuliomaliza," alisema Kaze.

Aliongeza katika kuhakikisha kikosi chao kinaimarika zaidi, wanatarajia kusajili mshambuliaji mpya ambaye ataungana na walioko kuhakikisha wanafunga ma-

INAENDELEA UK. 31

## Okwa aitabiria Simba makubwa

**Na Saada Akida**

WAKATI mchakato wa kuchukua fomu za kuwania nafasi mbalimbali katika uchaguzi mkuu wa klabu ya Simba, kiungo wa kimataifa wa timu hiyo, Nelson Okwa, amesema yeye bado ni mchezaji halali wa Wekundu wa Msimbazi na yuko tayari kuisaidia kutimiza malengo yake.

Okwa amerejea nchini juzi akitokea kwao Nigeria alipokwenda kwa ajili ya matibabu, tayari ameungana na wachezaji wenzake kuendelea na maandalizi ya mchezo wa Kombe la FA pamoja na mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Okwa, alisema hajapokea taarifa rasmi kutoka kwa uongozi wa Simba, hivyo anatambua bado mchango wake unahitajika ndani ya klabu hiyo.

Okwa alisema afya yake kwa sasa imeimarika na amerudi katika eneo lake la kazi ili kuhakikisha wanapambana na kusaka matokeo chanya kwenye mechi zote watakazocheza.

"Bila shaka nasoma kupitia vyombo vya habari, naona mitandaoni kama huna moyo mgumu hauwezi kucheza mpira, hakuna namna, sasa nimerejea na niko vizuri kuisaidia timu yangu ili kufikia malengo," Okwa alisema.

Aliongeza anahitaji kuongeza juhudi ili kupata nafasi zaidi ya kucheza na anafahamu Simba ni timu kubwa na yenye makocha wazuri ambao kwa pamoja wanatakiwa kuhakikisha wanasaka ushindi katika kila mchezo wanaocheza.

"Kwa sasa akili yangu inafikiria kucheza soka Ulaya na kurejea huko (Rivers United), nitakapokaribia kustaafu soka langu," alisema kiungo huyo.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya Simba, Boniface Lihamwike, amewataka wanachama wenye nia ya kugombea nafasi mbalimbali ndani ya klabu hiyo kujitokeza kuchukua na kurejesha fomu mapema ili kuepusha malalamiko hapo baadaye itaka-

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >